UTAMBULISHO WA MWANAMUME KATIKA METHALI ZA JAMII YA AGIKUYU

FRANCIS GICHINI GICHOHI

Ripoti hii Imewasilishwa kwa Shule ya Mafuzu kwa Madhumuni ya Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili Katika Kiswahili, Chuo Kikuu cha Egerton

CHUO KIKUU CHA EGERTON NJORO

APRILI 2018

UNGAMO NA IDHINI

Ungamo

Ripoti hii ni kazi yangu binafsi na asilia, na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu chochote kile.

Sahihi…… Tarehe……..

Gichohi Francis

AM12/2563/10

Idhini

Ripoti hii Imewasilishwa kwa kutahiniwa kwa idhini yetu sisi kama wasimamizi wa kazi hii, walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

Sahihi…… Tarehe……

Prof.. Furaha Chai (PhD)

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi

Chuo Kikuu cha Pwani

Sahihi …… Tarehe……..

Prof. James Onyango (PhD)

Idara ya Fasihi na Mawasiliano.

Chuo Kikuu Cha Laikipia.

.

HATILINZI

© 2018 Francis Gichohi

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili sehemu yoyote ya ripoti hii kwa njia yoyote au kuhifadhi kwa namna yoyote ile bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Egerton.

TABARUKU

Kazi hii naitabarukia mwenda zake mpendwa nyanyangu Hannah Njeri Githiomi na mwenda zake kakangu James Maina. Laiti Maulana angewajalia siku nyingi zaidi ili mpate kuushuhudia ukamilifu wa ndoto mliyosaidia kuagua. Subhana awape raha ya mbinguni na mwanga wa milele awaangazie, mpumzike kwa amani. Amina.

SHUKURANI

Shukurani zangu za dhati kwanza ni kwa Maulana aliyenikirimia kila aina ya baraka katika kipindi chote cha kazi hii. Pia shukrani zangu ni kwa Chuo Kikuu cha Egerton kwa kunipa nafasi ya kusomea shahada hii ya Uzamil. Kutoka kwa moyo wangu, nawapa kongole wasimamizi wangu wa kazi hii Prof. James Ogola Onyango na Prof. Furaha Chai. Hawa wawili ndio walionionyesha jinsi ya kushika makasia, na kunifunza kazi ya unahodha katika usomi. Rabana aibariki kazi ya mikono yenu.

Nawashukuru Bi. Juma, Dk. Taib na Dkt. Gwachi, ambao walinipa mkongojo nilipotetereka. Maelekezo yenu yalikuwa dira maasumu ya kuniongoza katika bahari ya usomi. Nawashukuru pia kwa dhati wahadhiri wa idara ya Fasihi Lugha na Isimu, hasa Prof. Aswani, Dkt. Nabea, Dkt. Wandera, Bw. Chacha, Bw. Muindi na marehemu Bi. Liguyani. Mashauri yenu yalikuwa mlizamu wa kunawirisha kazi hii.

Namshukuru bibi yangu, Mary Wanjiku, ambaye mbali na kuwatunza watoto wetu nilipokuwa nasoma, alinitia shime na kunishajiisha ari yangu ilipofifia. Wanangu Esther, Elizabeth, Maureen na Emily, nawashukuru kwa uvumilivu wenu. Mapenzi yenu yalinipa ghera na ilhamu ya kukamilsha kazi hii. Mama yangu mpendwa apokee shukrani za moyo wangu kwa kuniombea kila kuchao mpaka nikaikamilsha kazi hii. Nawapa kongole wahojiwa wangu wote. Hoja zenu zilikuwa amana muhimu kwa utafiti wangu. Nawashukuru wanafunzi tulioabiri nao dau moja la masomo, Grace Njeri, Samwel Kulu, Kipchumba na Ombati. Mijadala tuliyokuwa nayo ilinifaa sana.

Mwisho nawashukuru masahibu wote walionikongolea chembe ya hali na mali wakati wa uhitaji, Bw. Ngumo Wachira, Bw.Kinuthia Kiriro, Bw. Njuguna Githiri na Prof. Fr. Mbugua. Mikono yenu imebarikiwa. Kazi hii yote imepitia mikononi mwa bw. na bi. Kamau wa Executive Computers, ambao walipiga chapa tasnifu nzima. Maulana aibariki kazi ya mikono yenu.

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI....ii
HATILINZI....iii
TABARUKU....iv
SHUKURANI....v
ORODHA YA MAJEDWALI....ix
IKISIRI....x
ABSTRACT....xi
AKRONIMU NA VIFUPISHO....xii
SURA YA KWANZA....1
UTANGULIZI....1
1.1 Usuli wa Mada....1
1.2 Msingi wa Kihistoria wa Jamii ya Wakikuyu....4
1.2.1 Asili ya Mkikuyu Kulingana na Visasili....5
1.2.2 Asili ya Wakikuyu Kulingana na Ithibati za kihistoria....7
1.2.3 Maisha ya Kijamii....7
1.2.4. Kuzaliwa kwa Mtoto....8
1.2.5 Shughuli za tohara....12
1.2.6 Ada za ndoa....16
1.2.7. Swala la Uzee na Kifo....22
1.3 Mada ya Utafiti....23
1.4 Madhumuni ya Utafiti....24
1.5 Maswali ya Utafiti....24
1.6 Umuhimu wa Utafiti....25
1.7 Upeo na Mipaka....25
1.8 Maelezo ya Istilahi....26
MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA....28
2.1 Utangulizi....28
2.2 Chimbuko la Tofauti ya Nafasi ya Mwanamume na Mwanamke Katika Jamii....28
2.3 Maandishi Kuhusu Utambulisho wa Mwanamume....29
2.4 Maandishi Kuhusu Methali....34
2.5 Msingi wa Nadharia....37
2.5.1 Mkakati wa Urejelezi....38

2.5.2 Mkakati wa Nomino. 39
2.5.3 Mkakati wa Ubishi. 39
2.5.4 Mkakati wa Mkabala 39
2.5.5 Mkakati wa Kufifiza 40
2.5.6 Sifa Muhimu za Mkabala wa Kihistoria 41
MBINU ZA UTAFITI 43
3.1 Utangulizi 43
3.2 Mbinu za Utafiti 43
3.4 Uteuzi wa Sampuli. 44
3.7 Uchanganuzi wa data 46
SURA YA NNE 48
UCHANGANUZI NA UFASILI WA DATA 48
4.1 Utangulizi 48
4.2 Uchanganuzi wa data 48
4.2.1 Methali za mkabala wa kisiasa. 48
4.2.2. Methali Za Mkabala wa Kiuchumi 70
4.2.3 Methali za Mkabala wa Kijamii. 82
4.2.4 Methali za Mkabala wa Kimaumbile. 100
4.2.5 Methali za Mkabala wa Kisaikolojia 113
4.3 Majukumu ya Kimenke 126
4.3.1. Kiuchumi 127
4.3.2 Kisiasa/Uongozi/Utawala 128
4.3.3 Maisha ya Ndoa 129
4.3.4 Ulezi/Ujamiishaji 130
4.3.5 Ulinzi 131
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 132
5.1 Utangulizi. 132
5.2.1 Malengo na Makisio ya Utafiti. 133
5.2.2 Vikwazo 134
5.3 Mapendekezo 135
MAREJELEO 136
VIAMBATISHO 140
Kiambatisho I 140
Maswali ya Mahojiano Kwa Wasailiwa Kumi na Wawili (12) 140

Sehemu A **140**
Sehemu B **140**
Kiambatisho 2 ..... **141**
Methali Zinazomtambulisha Mwanamume **141**
Methali za mkabala wa kisiasa. **141**
Methali za mkabala wa kiuchumi **141**
Methali za mkabala wa kijamii **141**
Methali za mkabala wa kimaubile **142**
Methali mkabala wa kisaikolojia **142**
Kiambatisho 3 ..... **143**
Waliohojiwa **143**

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Uwepo wa Wanawake Katika Kazi Teule Kufikia 1978. 12

Jedwali 2: Mikakati Inayoelezea Nadharia ya U.H.U Mkabala wa Kihistoria 18

IKISIRI

Utafiti huu ulichunguza Utambulisho wa mwanamume katika methali za Agikuyu. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kudhihirisha jinsi jamii ya Agikuyu walivyomtambulisha mwanamume kupitia methali. Pia utafiti huu ulidhamiria kubainisha majukumu na nafasi ya mwanamume kama inavyodhihirika katika methali hizo. Msingi wa kinadharia alioutegemea mtafiti ulikuwa Nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi Mkabala wa Kihistoria. Nadharia hii inahusika na uchanganuzi wa miundo ya lugha inayodhihirisha ubaguzi. Nadharia hii ina mikakati mitano ambayo ndiyo iliyotumika kama mwongozo wa uchanganuzi wa data. Mkakati hiyo ni Urejelezi, Nomino, Ubishi, Mkabala na Kufifiza. Mbinu za utafiti huu zilikuwa utafiti wa kimaktaba na utafiti wa nyanjani. Data ya utafiti huu ilipatikana kutoka kwa methali teule arobaini na tano za jamii ya Agikuyu zilizochanganuliwa. Katika kuichanganua data mtafiti alitumia maelezo na majedwali kufafanua matokeo yaliyopatikana. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kukwezwa kwa mwanamume na kutambuliwa kwa njia ya kipekee na kutwezwa na kudhalalishwa kwa mwanamke. Kila mkakati ulichunguzwa kibinafsi na kudhibitisha kuwa matumizi ya lugha yalidhihirisha ubaguzi. Utafiti ulidhibitisha kuwa mwanamume amepewa majukumu yanayomsawiri kwa njia chanya na kuonekana kuwa nguli, ilhali mwanamke amefifizwa. Utafiti huu ni muhimu kwa watafiti wa lugha hasa katika uwanja wa isimu, ikizingatiwa kuwa ni utafiti wa kiisimu. Pia ni mchango muhimu katika uhifadhi wa Fasihi Simulizi ya Wakikuyu katika maandshi. Taasisi ya maswala ya kijinsia pia yatanufaishwa na utafiti huu. Mwisho utafiti huu ni mchango mpya katika tafiti za baadaye za uchanganuzi wa lugha na kuendeleza uwanja mpana wa isimu. Mtafiti amependekeza kuwa kuwe na usawa wa kimenke katika kugawanya majukumu na nafasi katika jamii. Pia mtafiti anapendekeza mahusiano ya uana yawe mazuri na yenye usawa. Nao watetezi wa usawa wa kijinsia wawajibike katika kuleta usawa wa kijinsia miongoni mwa wanajamii.

ABSTRACT

This research was on analysis of identity of man in Kikuyu proverbs. The aim of this research was to examine in details how language is used to identify a man in kikuyu proverbs. The theoretical framework of this research was Historical Discourse Approach. This theory has five discursive strategies that guided the researcher in data analysis. The strategies include Referential, Predicational, Argumentation, Perspectivation and Mitigation. Referential strategy looked at how persons are named and referred to linguistically. Predicational strategy looked at the traits, characteristics, qualities and features attributed to them. Argumentation strategy looked at argumentation schemes, that is, how persons try to justify and legitimize the exclusion and discrimination of others. Perspectivation strategy looked at point of view of these strategies. Finally the mitigation strategy focused on whether the utterance were articulated overtly or covertly. The main basis of this theory are positive self and negative other presentation. The research design and method of data collection was textual analysis. The data for this research was forty five (45) selected proverbs of the Agikuyu community. They were analysed on how they identified a man in the Agikuyu community and how they depicted gender roles. The identity and the gender roles were analysed on the basis of political, economical, social, physical and psychological aspects. The results were presented descriptively and in tabular form. The results ascertained that proverbs of Agikuyu community identifies a man as a superior being compared to a woman. The gender roles based on political, economical, social, physical and psychological aspects were also identified. The roles indicated that the male gender had more superior roles, hence, portraying him to be of a higher status than the female. The findings of this research are expected to be a major contribution in the preservation of the Kikuyu oral literature through documentation.The findings will also be of a great contribution to gender studies. They will be a new contribution in the field of discourse analysis and moreover they will form a basis for further research in this area. The researcher recommends for further research on the Agikuyu community and more documentations of their oral literature.

AKRONIMU NA VIFUPISHO

U.H.U -Uchanganuzi Hakiki Usemi

U.K - Uwezo Kiume

U.U - Uchanganuzi Usemi

T.Y.K - Taasubi Ya Kiume

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Methali, ngano , visasili, mighani na vitendawili ni usanii wa msemaji au sanaa ya usemaji. Haya ni maoni ya Bascom (1955:245) katika Finnegan, (1992:10). Methali ni sehemu ya lugha na hutumika kuyatafakari, kuyapima maisha na kufunzia jumuiya. Abdilatif (1978:1) katika Wandera (1996) anadai kuwa hakuna fasihi iliyochipuka na kuendelea kuishi katika ombwe tupu. Fasihi yoyote ile hupata uhai wake katika jamii. Jamii ya Agikuyu ina methali chungu nzima ambazo zimetumika katika mazungumzo tangu hapo jadi. Achebe **(**1960) anasema kuwa methali ni kama sharubati ya kulia maneno katika baadhi ya jamii za Kiafrika. Hii ina maana kuwa mawasiliano mema kupitia mazungumzo, maandishi na utendaji huhitaji usujudu wa methali. Methali huongeza utamu wa mawasiliano Amuka (1994), Katika Bukenya na wengine.

Kwa mujibu wa Wamitila , methali ni msemo unaojitosheleza, wenye maana, yenye nguvu na uzito, wenye muundo na sifa za kishairi, unaokusudiwa kuadibu, kuelimisha, na kushauri. Mohamed, Katika Wamitila **(**2001) anasema methali ni kama mafuta, hulainisha usemi. Hii ina maana kuwa kuna matamko ambayo ni laini na ya kupoza na kuburudisha. Inaaminika kwamba mtaalamu Taylor ndiye mwanzilishi wa taaluma ya "Paremiolojia" (*Elimu inayojishughulisha na methali*) (Wamitila: 2001).

Methali ya waswali inayosema, " *Mume ni mume, hata awe gumegume ana sifa ya mtume*", inadhihirisha ya kuwa katika jamii ya Waswahili, mwanamume alitambuliwa kama aliye na uwezo mkubwa na utukufu, hata akiwa mnyonge, maskini au mlemavu. Methali hii inatiwa nguvu zaidi na beti zifuatazo mbili za utendi wa Mwanakupona zinazodhihirisha nafasi ya mwanamume katika jamii ya Waswahili.

25. Siku ufufuliwao
Nadhari ni ya mumeo
Taulizwa atakao
Ndilo takalotendewa

26. Kipenda wende peponi

Utakwenda dalhini
Kinena wende motoni
Huna budi utatiwa. (Utendi Wa Mwanakupona)

Ingawa kazi hii ya Mwanakupona ni ya ubunifu tu, inaonyesha ya kuwa mwanamume alikuwa ametambuliwa kama kiumbe chenye uwezo mkubwa na kiumbe maasumu, hivi kwamba bwana ndiye angeamua hatima ya bibiye. Bwana akisema bibi aingie jahanamu, itakuwa hivyo, na akimua aingie paradiso, uamuzi wake utaheshimiwa. Hapa ni wazi kuwa jamii ya Waswahili huongozwa na mfumo wa taasubi ya kiume. Tafiti zilizofanywa zinazohusiana na methali zimeangazia maana na matumizi ya methali, chache zimegusia usawiri wa mwanamke katika methali za jamii tofauti. Utafiti huu ulitoa uhalisia baina ya methali na hali kamili ya utambulisho wa mwanamume katika methali za Wakikuyu.

Utambulisho au ujitambuaji ni ile hali ya kujihisi, kung'amua au kubaini kuwa sawa na wengine na kuwa tofauti na wengine kwa misingi ya lugha, utamaduni, siasa, rangi, na maisha ya kila siku kwa ujumla. Kuna utambulisho wa kibinafsi, wa kijamii na wa kitaifa. Utambulisho wa kitaifa ni pale ambapo jamii itajihisi kuwa na mawazo sawa, mitazamo sawa, hulka sawa na siasa sawa. Mambo haya wanayabaini kupitia kwa masomo, siasa, michezo na shughuli za kila siku. **(**Wodak na wengine; 1999: 4)

Utambulisho huelezea juu ya vitu viwili au zaidi ambavyo vinalingana. Hata hivyo, mfanano huu haudumu sana kwa sababu vitu na hata watu hubadilika kulingana na hatua za maisha – watu hubadilika kimwili, kisaikolojia na hata kijamii. Hivyo utambulisho utarejelea kitu kinachobadilika kiwakati, hii ni pamoja na utambulisho wa kijamii na utambulisho wa kibinafsi (Wodak na wengine: 1999:5).

Ricoer (1992:116) anabainisha aina za utambulisho zinazofanana, yaani utambulisho kama usawa au umoja na utambulisho kama ubinafsi. Anaendelea kugawa ule umoja au usawa katika utambulisho wa kiuwigidadi na wa kiudhamano. Utambulisho wa nafsi ndiyo nguvu inayomwezesha mtu kuelekeza tabia zake. Hii ni pamoja na uwezo wa kuelekeza majukumu ya kijamii na uwezo wa kufasili matokeo ya majukumu hayo.

Kulingana na Martin (1995), utambulisho wa mtu binafsi hujulishwa kwa wengine kupitia masimulizi, na kwa njia hii, inawezekana kupanga na kufasili, kupanga tena na kufasili tena matukio ya maisha ya mtu yaliyopita (Martin;1995;8). Mielekeo chanya

kuhusu mwanamume katika jamii ya Agikuyu inadhihirika wazi na kuendelezwa na asasi mbalimbali za kijamii kupitia methali, ngano, nyimbo vitendawili na hata miiko. Mwanamume ameendelea kutambuliwa kama kiumbe chenye uwezo mwingi katika jamii akilinganishwa na mwanamke. Jambo hili liko katika jamii nyingi za Kiafrika hata baada ya mikakati ya kitaifa na ya kimataifa ya kuleta usawa kati ya mume na mke (mkutano wa wanawake Beijin, China). Hii ni kwa sababu ya taasubi ya kiume ambayo huongoza jamii nyingi za Kiafrika. Jambo hili lilikuwa dira maasumu ya kushughulikia swala hili.

Katika Utendi wa Mwanakupona, mwanamume amerundikiwa sifa chungu nzima pale mama anapomshauri binti yake jinsi ya kuishi na mumewe. Kutoka ubeti wa 24 hadi 36, binti anashauriwa na kuonyeshwa kuwa mume ni kitu cha thamani kubwa kinachostahili kutunzwa vyema. Ingawa hii ni kazi ya kubuni, inaonyesha wazi kuwa hata katika jamii ya Waswahili wa Pwani, mwanamume alitambuliwa kama kiumbe bora kuliko mwanamke. Halliday (1978) anatoa kauli kuwa mtoto anapojifunza lugha huwa anajijengea picha ya uhalisia unaomzunguka. Utafiti huu ulichanganua utambulisho wa mwanamume katika methali za Wakikuyu.

Jamii ya wakikuyu huongozwa na mfumo wa itikadi wa kuumeni. Hii ni kwa sababu wanafuata mwelekeo wa Taasubi Ya Kiume. Utafiti huu ulijikita katika kuchambua utambulisho wa mwanamume katika methali za Kikuyu kwa kutumia mikakati mitano ya usemi. Methali ni usemi wa kisanii wa kimapokeo uanofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano, na huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yaliyotumiwa (TUKI 2004: 240). Ni muhimu kuchunguza amali zinazopitishwa kama mirathi kwani ni bayana kuwa hadhi ya mwanamke inatokana na jinsi alivyotambulishwa katika utamaduni uliosheheni Taasubi Ya Kiume. Utafiti huu ulikusudia kumwangalia mwanamume jinsi alivyotambuliwa kupitia kwa mitazamo ya wanajamii inayopitishwa katika methali za Wakikuyu. Tulibainisha kuwa mielekeo hiyo inamtukuza mwanamume na kumtambua kama mwenye uwezo na mamlaka. Matokeo ya utafiti huu yatawafaa sana wanafunzi na walimu wa Uchanganuzi Matini kuelewa zaidi kuhusu utambulisho wa mwanamume katika jamii ya Wakikuyu, kwa kutumia methali za Wakikuyu kama matini. Mwishoni, utafiti umetoa mwongozo wa jinsi ya kuwatambulisha watu wa jinsia mbili kwa njia sawa. Utambulisho ulifanywa katika sifa za kimaumbile, kijamii, kinafsia,

kisiasa na kiuchumi. Mbinu zilizotumiwa katika utafiti huu ili kupata data ni pamoja na mahojiano. Niliwahoji wazee kumi na wawili wenye umri wa miaka 70 hadi 80. Nilikuwa na mwongozo wa maswali niliyowauliza wasailiwa wangu. Mbinu ya kurekodi ilitumika. Pia nilitumia njia ya uchunguzi maktabani. Hapa nilichunguza maoni ya wataalamu wengi nipate kujua wanasemaje kuhusu utambulisho wa mwanamume. Nikiwa nyanjani, nilitumia kanda ya kunasa sauti ili ninase mahojiano yangu na wasailiwa wangu. Mbinu hii ilinisaidia baadaye kuyapata yaliyonipita pale katika mahojiano.

1.2 Msingi wa Kihistoria wa Jamii ya Wakikuyu.

Katika sura hii, mtafiti ataangalia kwa kifupi msingi wa kihistori wa jamii ya Wakikuyu, kisha ataangazia jinsi mwanajamii wa jamii ya wakikuyu anavyojamiishwa kutoka kuzaliwa hadi uzeeni. Methali za jamii ya wakikuyu huchota malighafi yake kutoka kwa utamaduni wa jamii yenyewe. Methali hizi huwakilisha maisha kamili katika uhalisia wake. Okindo (1995) anasema kwamba fasihi huimbuliwa na asasi mahususi za kijamii. Munene (1995) anaunga mkono kauli hii anaposema,

> *"Agikuyu Maturaga na ndundiro ciao cia ihooto ciitagwo thimo kuuma kiimerera kiao*",
> (Wakikuyu daima wanaishi wakiongozwa na ukweli unaopatikana katika methali kuanzia utotoni).

Hii ina maana kuwa methali za jamii ya wakikuyu zilijikita katika utamaduni na maisha kwa jumla ya jamii hiyo. Hivyo basi, ni muhimu kuuelewa utamaduni wa wakikuyu ili kuweza kuzielewa kwa undani methali husika. Jambo hili ni muhimu kwa sababu kila methali ilitungwa katika mkutadha wake.

Swala la uana linapewa nguvu na tajiriba na mielekeo ya watu kuhusu uwezo, siasa, utamaduni na maingiliano ya kila siku. Wanaume wamechukuliwa na jamii kuwa wenye uwezo kuliko wanawake. Pia, wanaonekana kama ndio walio na uwezo mkubwa kisiasa. Tukichukua mfano wa nchi yetu kisiasa, ni wazi kuwa mwanamume ametawala uwanja wa siasa kwa muda mrefu. Jambo hili limebidi kukawekwa kifungu katika katiba ya nchi yetu kinachosema ya kuwa thuluthi moja ya wale wote watakaochagulia kushika zamu popote pale lazima wawe wanaume au wanawake. Kifungu hiki kiliwekwa kwa sababu ya wanawake amabo hawakuwa wakipata nafasi

nyingi, hasa katika nyanja za siasa. Ili kuelewa kwa undani utambulisho wa mwanamume katika methali za jamii ya Agikuyu, ilimbidi mtafiti kuangazia nyanja zifuatazo za maisha ya mwanajamii mkikuyu kama ngazi ya kufafanua zaidi maana za methali katika utambulisho wa mwanamume mkikuyu.

1.2.1 Asili ya Mkikuyu Kulingana na Visasili

Mwanamume wa kwanza katika jamii ya Agikuyu aliitwa Gikuyu. Bibi yake aliitwa Mumbi. Waliamini ya kwamba waliumbwa na Mungu waliyemwita "*Ngai*". Waliamini huyu Ngai aliishi katika mlima Kirinyaga (mlima Kenya). Huyu Mungu walimwita "*Mwenenyaga".* Gikuyu na Mumbi walisafiri kutoka mlima Kirinyaga wakielekea upande wa kusini. Walipofika *Mukurwe Wa Nyagathanga*, walipiga kambi hapo na pakawa makao yao. Walikuwa na watoto wao wa kike kumi (10). Jambo hili la kukosa mtoto angalau mmoja wa kiume hal ikumfurah isha Gikuyu. Alimuomba Mwenyezi Mungu, waliyemwita *Mwenenyaga*, ampe wavulana wa kuwaoa wale wasichana wake.

Gikuyu alimtafuta mbuzi wa kiume, aliyekuwa wa rangi moja, akamtolea *Mwenenyaga* kafara, chini ya mti wa mugumo (mkuyu). Chini ya mti huu ndipo alipotengeneza madhabahu. Kutoka siku hiyo, kutoa sadaka chini ya mti wa mugumo ikawa desturi katika jamii ya Wakikuyu. Baada ya siku chache, mabarobaro kumi walitokeza na kuwaoa wale mabinti kumi. Tangu hapo, Jamii ya wakikuyu ikaanza kufuata mfumo wa itikadi ya kuukeni. Majina ya mabinti wale kumi yalitambulisha mbari za jamii ya wakikuyu. Mbari hizi ni:-

Mzazi	**Mbari (muhiriga)**
Wanjiku	Agaciku
Wangari	Angari (Aithekahuno)
Wambura	Ambura (Ethaga)
Wamuyu	Aichakamuyu
Wairimu	Airimu (Agathigia)
Wacera	Achera
Wambui	Ambui
Wangui	Angui (athiegeni)
Wanjiru	Anjiru
Wangeci	Angechi (aitherandu)

Mbari hizi zinaonekana kuwa kumi, lakini wakikuyu huamini kuwa wao wana mbari tisa wala sio kumi. Badala ya kusema mbari ni kumi, wakikuyu husema wao ni mbari "*Kenda muiyuru*" (tisa iliyokamilika). Ilikuwa muhali katika jamii ya wakikuyu kuhesabu hadi nambari kumi. Hata kama mkikuyu alikuwa na ng'ombe au mbuzi kumi, alihesabu hadi namba tisa halafu anaruka nambari ya kumi. Baada ya miaka mingi, jamii ya wakikuyu ilisambaa mbali mno. Inasemekana kuwa Wameru, Waembu na Wakamba ni baadhi ya wakikuyu waliohamia sehemu za mbali. Idhibati ya imani hii ni kuwa baadhi ya mila na desturi za jamii hizi hulandana na za jamii ya wakikuyu. Pia lugha za jamii hizi zinakaribia kwa kiasi kikubwa .

Kwa muda huu wote, jamii ya Wakikuyu ilikuwa ikiongozwa na itikadi ya kuukeni. Wanawake walikuwa na mamlaka makubwa kuliko wanaume. Desturi ilikuwa waume kuwatumikia mabibi zao. Kiongozi aliyeongoza jamii nzima alikuwa mwanamke aliyeitwa Wangu wa Makeri. Wanaume walidhalilishwa na uongozi huu wa wanawake. Wanaume walijaribu kijikomboa kutoka kwa dhuluma na unyanyasaji wa wanawake lakini juhudi zao ziligonga mwamba. Zana zote za vita zilikuwa katika himaya ya mwanamke. Baada ya kutafakari kwa muda, wanaume walijipa moyo kwa methali ya kikuyu inayosema;

> "*Kirema arume nikigariure",*
> (Wanaume hawashindwi kutatua jambo lolote lile, na litakalowashinda, huwa limeshughulikiwa kwa undani).

Hivyo, wakaamua kupanga mapinduzi ya amani.Walipanga ya kuwa kila mwanamume aliyekuwa na bibi ampachike mimba, na jambo hili litekelezwe sawia. Wanaume walijua kuntu kuwa mwanamke akiwa mja mzito hawezi kupigana kwa dhati. Walifuatia wasia wa methali isemayo,

> "*Mundu muka uri ihu na wi kironda no undu umwe*",
> (Mwanamke mjamzito ni sawa na aliye na kidonda au aliyejeruhiwa).

Walipofaulu kuwapachika mimba, walingojea hadi mwezi wa nane wa mimba hizo, kisha wakatekeleza mapinduzi yao yaliyofaulu fika. Kutoka siku hiyo hadi leo, itikadi ya kuumeni huongoza jamii ya wakikuyu. Wanajamii wanaamini sana visasili hivi kwa dhati. Mtafiti ameonyesha jinsi itikadi ya kuukeni ilivyobadilika na kuwa itikadi wa kuumeni.

1.2.2 Asili ya Wakikuyu Kulingana na Ithibati za kihistoria.

Wakikuyu ni mmjoawapo ya jamii zinazounda kundi la wabantu wa Afrika mashariki. Idhibati za kihistoria zinaonyesha kuwa wakikuyu ,wakamba, wadigo, waduruma, na wengine walighura kusini mwa kongo, wakapitia kusini mwa ziwa Victoria na kupiga kambi katika milima ya taita. Nadharia hii inakiri kuwa wengi walielekea upwa, wakapanda hadi nchi ya Somalia sehemu inayoitwa Shungwaya.

Kilichowavutia katika sehemu hii ya Shungwaya na kuwafanya wafanye makazi yao hapa ni mchanga wenye rotuba kwa Kilimo na lishe bora ya mifugo wao. Waliishi pamoja kwa muda, kisha mapigano yakazuka kati ya wabantu na wagalla kwa sababu ya malisho. Wabantu walihama, sio kama kundi moja, bali walitawanyika katika upwa wa Afrika mashariki katika karne ya 16. Idhibati za kihistoria zinatujuza ya kwamba mababu wa wakikuyu walitoka sehemu inayojulikana leo kama Tharaka na Igembe. Kuna wachache wanaodai kuwa walitoka Thigicu na Ithanga kule ukambani. Jamii ya wakikuyu iliteremka kutoka sehemu hizo hadi Sagana, wengine Mathira na Mukurwe-ini katika karne ya 18. Baadaye, jamii ya wakikuyu ilisambaa hadi Nyandarua, Kabete, Othaya na Aguthi. Leo, wakikuyu wako Muranga, Nyeri na Kiambu.

1.2.3 Maisha ya Kijamii

Wakikuyu waliishi kama jamii moja. Mkikuyu akitenganishwa na wenzake, maisha yake hayana maana. Watoto na vijana ambao walikuwa hawajaoa au kuolewa waliitwa kwa majina yao. Tangu kuzaliwa hadi kufa kwake, mwanajamii alipitia hatua mbalimbali ambazo zilimsaidia kuelimika kuhusu ushirikiano na watu. Mwanajamii alibidiika kutafuta ushauri kutoka kwa jamaa yake au rafiki kabla ya kufanya jambo lolote lile. Hii ni kufuatana na methali ya wanajamii inayosema;

> *"Ugi wa mundu umwe ndurimaga*" – yaani,
> Werevu wa mtu mmoja hauwezi kukamilisha kazi zote za shamba.

Methali hii ilitumiwa kuwaonya waliojiona werevu wasije wakatumbukia kwenye lindi la shida. Jamii ya wakikuyu ilitumia methali kama njia ya kupitishia amali mbalimbali za jamii. Ili kuonyesha kuwa ilibidi wanajamii washirikiane na asipatikane mmoja anayejitenga, wakikuyu walikuwa na methali iliyosema,

> "*Rurira rutithambagio rui*",- yaani
> Uhusiano wa watu wa jamii moja hauwezi ukaoshewa mtoni.

Kila mwanajamii ilibidi apitie hatua mbalimbali ambazo huwa ni kaida katika jamii, na anayekiuka kaida hizi alitengwa na kuchukuliwa kuwa muasi. Hatua hizi ambazo mwanajamii hupitia zitasaidia sana kupambanua na kudhihirisha mtazamo wa wanajamii hawa kuhusu mahusiano ya uana, jambo ambalo lilichunguzwa kwa undani kupitia kwa methali zilizochambuliwa. Kila hatua aliyopitia mwanajamii iliambatana na sherehe yake.

1.2.4. Kuzaliwa kwa Mtoto

Wakati wa kujifungua kwa mama ulipowadia, mkunga aliitwa, aliyeshirikiana na wanawake wengine kumuauni mama anayejifungua. Ikiwa mtoto aliyezaliwa ni wa kiume, wanawake walipiga vigelegele vitano (*Ngemi)*, ambavyo viliashiria mtoto wa kiume amezaliwa. Baba wa mtoto huyo naye alienda shambani na kukata miwa mitano. Maji matamu ya miwa yalimiminwa midomoni mwa mtoto huyo hata ingawa hakumeza. Hii ilikuwa ishara ya mwanzo mwema.

Ikiwa mtoto aliyezaliwa ni wa kike, wanawake walipiga vigelegele mara nne kuashiria ni mtoto wa kike. Baba wa mtoto aliyezaliwa alikata miwa minne na maji matamu ya miwa kumiminwa kwa midomo ya mtoto. Hii ni dhihirisho tosha la mtazamo wa jamii kuhusu tofauti za kiuana. Mvulana alithaminiwa zaidi kuliko msichana na uthamini huu uliendelea hadi mwisho wa maisha ya hawa wawili. Mwanamke aliyezaa wasichana tu bila kujaliwa mtoto wa kiume, alikejeliwa kwa kuitwa, "*nyina wa irigu*", yaani kurejelea kimadharau "mama wa wasichana ambao hawajapashwa tohara". Mume wa mama huyu hakurejelewa kwa jina lolote lile, ilhali yeye ndiye aliyehusika kuwazaa wasichana wale. Huu ndio mtazamo wa jamii.

Kwa upande mwingine, mama aliyezaa watoto wavulana pekee hakurejelewa kwa njia yoyote ile, lakini bwanaye ndiye aliyeonekana shujaa na jamii ilimshinikiza aoe mke mwingine ili apate watoto wa kiume zaidi. Jamii inaonekana kumpa mwanmume huyu kongole badala ya bibiye ilhali mwanamke ndiye hulaumiwa akizaa wasichana, taasubi ya U.K. Jamii ilimtazama mwanamke kama kiwanda cha kumtengenezea mwanamume warithi (*Aramati)*. Jamii ilikiuka sayansi ilipompima mwanamke kulingana na kizazi chake. Sayansi inaelezea kuwa mwanamume ndiye huamua jinsia ya mtoto atakayezaliwa. Kwa vile jamii ilimchukulia mtoto wa kiume kuwa bora zaidi kuliko wa kike, basi jamii ikatunga methali,

"Kahii ni ithigi ria mucii", kumaanisha,

(Mvulana ni ngao ya mboma).

Hii inamaanisha kuwa jukumu muhimu sana la ulinzi lilipewa wanaume. Baadhi ya majina ya wavulana wakikuyu yalipeanwa yakirejelea ubora na umuhimu wa mwanamume katika jamii; mfano:

Ndegwa - *Fahali, mwenye nguvu na hodari*

Njamba - *Shujaa*

Wang'ombe - *Mwenye ng'ombe na mali nyingi*

Gitonga - *Mwenye mali mengi*

Wangai - *Aliye karibu sana na Mungu*

Wang'ondu - *Mwenye kondoo wengi*

Munene - *Mtu mkubwa*

Watoto wa kike nao walipewa majina yaliyolenga kuwadunisha na kuwaonyesha sehemu yao katika jamii, mfano:

Wamucii - *Mwenye kukaa nyumbani*

Nyaguthie - *Asiyetulia mahali pamoja*

Waceke - *Mwembamba*

Nyakairu - *Mweusi*

Mapendeleo kwa upande wa mume yalidhihiri. Mafunzo ya kwanza aliyopewa mtoto yalipitishwa kwa bembelezi. Ingawa mtoto alikuwa mchanga sana na hakuelewa ujumbe uliokuwa katika bembelezi, jamii iliamini kuwa bembelezi zile zilikuwa na athari fulani katika maisha ya mtoto. Hali hii inaenda sambamba na maoni ya Khasiani na Njiru (1993:33) wanaposema,

> "*Katika jamii inayozingatia ubabeume, wanawake na waume wanajamiishwa kukubali nafasi yao, iwe duni au tukufu. Wake kwa waume waliitia hali hii mawazoni mwao. Wanaume wanahimizwa kuwa na ushari, Uwazi, uhuru na ushindani, ilhali wanawake hufunzwa kuwa watulivu, wategemezi, wasio na uwazi na watiifu*".

Watoto katika jamii walithaminiwa sana kwa sababu ni ishara ya uhai wa jamii na matumaini ya mustakabali wa jamii. Watoto wavulana walithaminiwa kwa kuwa ndio wariithi wa mali ya jamii. Methali ikatungwa;

Kahii koigi ta ithe kabaritaga ta migwi", kumaanisha,
(Mvulana mwerevu kama baba yake hupeperuka kama mshale).

Mzazi wa kiume hapa anapewa sifa ya werevu. Watoto watundu na mabwege walihusishwa na mama yao. Bibi aliyeolewa, halafu akakosa mtoto, alitafutiwa mke mwenza atakayempatia mume yule mrithi. Hii ni sawa na anavyosema Chacha (1997);

"...Semo, rafiki yangu yule ndiye aliyenipasulia ukweli, kwamba sikuwa na chochote cha kujivunia huku nyumbani nikiwa nimejaza genge la majike tu. Warithi wangu, kufuatana na ada na desturi za Ki-mara, ni akina nani?"

Hata ingawa huu ni mchezo wa kuigiza, twafahamu kuwa fasihi huchota malighafi yake kutoka kwa utamaduni wa jamii. Jamii ya wakikuyu ilimchukulia mwanamke kama chombo cha kutekeleza majukumu matatu muhimu. Kwanza, mwanamke kufanya kazi shambani ili familia yake ipate riziki ya kila siku. Pili, kumtoshelezea mumewe mahitaji ya kimwili. Mwisho, kuzaa watoto na kuwalea vyema hasa wa kiume, watakaoendeleza ukoo na kuwa warithi. Methali ya kikuyu isemayo;

"Mwana wa kairitu ni mutuga kwene",
(Mtoto wa kike ni mhudumu wa kwingine) ,

huonyeshe kuwa mtoto wa kike hakuthaminiwa kwa sababu akifikisha umri wa kuolewa, ataondoka kwao aende akaitumikie familia nyingine.Alipofikisha miaka sita au saba, mtoto wa kike alianza kumsaidia mama yake kazi za nyumbani kama vile, kuosha, kusafisha, kupika, na kadhalika. Mtoto wa kiume naye alimsaidia baba yake kulisha mifugo na yale majukumu mengine yaliyotengewa waume.

Mwendo wa jioni, watoto walikutanika kwa nyanya yao au babu yao kutambiwa hadithi, kutegewa vitendawili na kufunzwa nyimbo. Hapa ndipo mwanajamii huyu mchanga alipopata mafunzo kuhusu maswala ya jamii yao. Wasichana walifunzwa kupika, ususi, kutunza watoto na amali nyingine za nyumbani. Wavulana kwa upande wao walifunzwa kuhusu ufugaji, ukulima, uhunzi, usasi na uchongaji. Hapa ni bayana kuwa kazi za wanawake ni za kuwafunga nyumbani na hivyo wasipate nafasi ya kujumuika na wanawake wengine. Majagina wa hadithi walipewa majina ya wanaume. Majina ya wanawake yalitumika kwa wake wenza wenye wivu, na wale waliowaonea wivu watoto wa wenzao. Jambo hili lilimshushia hadhi mwanamke na kutilia mkazo

kuwa uwezo wa mwanamke ni pungufu. Hivyo basi, wakikuyu katika methali yao wakasema;

"*Mwaki wa mucii uthegeagwo ni mutumia",*
(Moto wa boma hupekechwa na mwanamke).

Hapa tunapewa wazo kuu kuwa sehemu ya mwanamke ni jikoni. Taasubi hii ya kiume ilikolezwa katika tafakuri za watoto kiasi cha kuwafanya waamini kuwa wanawake wanapaswa kuwa chini ya mamlaka ya mwanamume. Wavulana walipotimiza miaka kati ya kumi na minane (18) hadi arubaini (40), walipewa jukumu la kuilinda jamii dhidi ya adui. Hii ndio sababu kuu ya kuwathamini watoto wa kiume.

Msichana akiolewa anaiacha mbari yao na kujiunga na mbari ya mumewe, ndiposa ile methali;

"Mwana wa kairitu ni mutuga kwene,"
(mtoto wa kike ni mhudumu kwingine) .

Hii ni kwa sababu baada ya kuolewa, huendeleza mbari ya mumewe si yake.

Hatua itakayofuata ni kama daraja ya kuwavusha kutoka utotoni hadi utu uzima, pale wanapohitajika kuchukua na kutekeleza majukumu yao kwa wanajamii halisi. Kuzaliwa ndio hatua ya kwanza kwa mwanajamii. Yale yote yanayoendelezwa katika kipindi hiki huonyesha tofauti za kiuana huku yakimtambulisha mwanamumme kwa njia ya kumtukuza ni:

1. Mvulana alipozaliwa alipigiwa vigelegele (ngemi) vitano ilhali msichana alipigiwa vinne.
2. Baada ya kuzaliwa baba wa mtoto wa kiume alikata miwa mitano ilhali baba wa mtoto wa kike alikata miwa minne.
3. Mwanamke aliyezaa watoto wa kike bila mvulana alikejeliwa kwa kuitwa "*nyina wa Irigu"*(mama wa wasichana ambao hawajapashwa tohara) ilhali baba wa wasichana hao hakupewa jina lolote badala yake, alihimiza aoe mke wa pili atakayemzalia mrithi.
4. Mwanaume ambaye bibi yake alipata watoto wa kiume bila wa kike alipewa sifa na kuitwa hodari na alihimiziwa hata aoe mke mwingine azidi kupata watoto wa kiume wengi.

1.2.5 Shughuli za tohara.

Vijana hukumbushwa kaida zilizotawala jamii wakati wa tohara. Uwezo kiume wa kustahimili uchungu wa kisu cha ngariba ulikuwa jaribio la kuntu la kumweka mhusika makali na kumshujaisha kuyakabili maisha. Nyimbo zilizoimbwa wakati huu zilipitisha maadili ya kijamii kwa watahiriwa, hivyo kuwaelimisha na kuwahamasisha vijana kuhusu yanayoenziwa na jamii yao. Tohara ilisaidia kushamirisha uhusiano miongoni mwa watahiriwa. Ukweli huu unapigwa muhuri na methasli inayosema;

" Rika na nyumba itiumagwo"

(Rika na nyumba ni mambo mawili yasiyokimbilika).

Kenyatta 1978:133, anasema kuwa katika jamii ya wakikuyu, tukio hili la tohara lina umuhimu wa kidini, kijamii na kielimu kwa wanajamii wote. Wale wote waliotahiri wakati mmoja walipewa jina la rika hilo, na jina lilikuwa la kiume, mfano;

1650-1730- *rika ria Cuma*

1750 - *rika ria Ciira*

1790 - *rika ria Mathathi*

1829 - *rika ria Ndemi*

1841 - *rika ria Kamau*

1850 - *rika ria Maina*

1905 – *rika ria Mwangi*

(Murata : Marchi 1999)

Tohara ya wavulana na wasichana ilikuwa asasi muhimu kwa jamii ya wakikuyu. Kulitokea mvutano na mgongano mkubwa kati ya wamishonari waliopinga tohara ya wasichana na wakikiuyu walioshikilia mila hiyo kwa dhati. Ilionekana kuntu kuwa mwanajamii alizama fika katika utamaduni na mila za jamii yake kupitia kwa tohara. Kwa mkikuyu, tohara kwa wasichana na wavulana halikuwa jambo la kupingika. Wavulana ambao hawajakumbana na kisu cha ngariba walirejelewa kwa madharau kama *"ihii",* na wasichana waliitwa *"Irigu*". Asiyepitia hatua hii, hasa mwanaume, hata awe na miaka mingi, hakuheshimiwa katika jamii na lazima angeshikwa kwa nguvu na kupelekwa kwa ngariba. Hata leo jambo hili la kuwapeleka wazee ambao hawajatahiriwa kupatana na kisu cha ngariba linaendela, ndiposa methali ikatolewa; *" Kurua ni kwara itara".* Hii ina maana kuwa kutahiri ni sawa na kuyatayarisha ambako kutatumia kuhifadhia kuni ndani ya nyumba. Hii ni jazanda inayotumika kurejelea

majukumu ambayo mwanajamii anatarajiwa kuyatekeleza baada ya tohara. Huu ndio wakati ambapo vijana walipewa majukumu yao nao. Pia, walifunzwa matarajio ya jamii kutoka kwao. Wasichana wakiwa toharani walifunzwa jinsi ya kuwatumikia waume wao pidi watakapoolewa. Wavulana kwa upande wao walifunzwa jinsi ya kutamalaki na kulinda jamii dhidi ya uvamizi.

Mafunzo haya yalimtayarisha mwanamke kuchukua nafasi ya utumishi naye mwanamume kuchukua nafasi ya ubwana. Huu ndio mtazamo wa jamii kwa mwanaume. Oduyoye (1998:4) anaizungumzia hali hii anaposema;

> *"Katika Jamii za kiafrika, wanawake wanachukuliwa kama watu wa hadhi ya chini .Wanachukuliwa na kutumiwa na wanaume kama mali ya kibinafsi. Wanadhulumiwa na kubekuliwa na kutumikshwa".*

Utumishi wa wanawake haulazimishwi.Mfumo wa ujamiishaji hufanya mwanamke kuikubali hali hii bila manung'uniko. Sheria za jamii zilitiliwa mkazo zaidi katika hatua hizi za maisha. Ilikuwa mwiko kwa msichana ambaye hajatahiri kushiriki katika tendo la ngono, au hata kuolewa. Ilikuwa muhali jambo hili kutokea, lakini iwapo lingetokea mwanaume aliyehusika alifanyiwa matambiko yaliyoitwa, " *gutahikwo migiro*". Mwanamke kama huyu alionekana najisi na hakuna kilichofanywa kumtakasa, lakini mwanaume baada ya sherehe ya "*gutahikwo migiro*" alichukuliwa kama aliyetakasika. Wavulana ambao hawajatahiri hawakushirikishwa wakati wa kutembelea wakwe. Ndiposa tuna methali isemayo,

"Ihii itithiaga Uthoni"

(wavulana ambao hawajatahiri hawashiriki katika kuwatembelea wakwe).

Tohara ya wasichana ilikusudiwa kuwapunguzia nyege na hivyo kuwaepusha na ushawishi wa washerati. Dhana hii iliwanyima wanawake fursa ya kufurahia tendo la ndoa. Jamii ilipendelea mwanaume kufurahia tendo la ndoa na sio mwanamke. Imani hii ya jamii yaelekea kushahibiana na maandiko matakatifu ya mtume Paulo kwa wakorintho anaposema;

> "*Mke hana amri juu ya mwili wake,bali mumewe*", (1st kor. 7:4)
>
> Haya yalikuwa maonevu ya jamii kwa mwanamke.

Shughuli yote ya tohara ilikusudiwa kumfundisha mtahiriwa kaida, sheria, mila na utamaduni wa jamii yake. Baada ya tohara kuna baadhi ya mambo ambayo mtu

aliruhusiwa kufanya na hangefanya hapo mbeleni. Wakati wa sherehe za tohara, jamii ilikuja pamoja. Wanajamii wakapata nafasi ya kuingiliana na kusheherekea pamoja. Nyimbo zilizoimbwa wakati huu zilisheheni ujumbe uliokusudiwa kuwatayarisha vijana kuchukua majukumu yao kwa mujibu wa uana. Nyimbo ziliwachochea wavulana kuwa wakakamavu na wajasiri kwa minajili hasa ya kulinda jamii. Wasichana nao walishinikizwa wawe watiifu kwa waume wao na wawe na bidii kazini.

Kwa majuma mawili matatu hivi, watakaotahiriwa walilishwa kwa lishe bora. Msichana yeyote ambaye angepatikana na hedhi au ameivunja ubikira alitakaswa kwa taambiko lililoiitwa "*Gutahikio"*. Sherehe ya mkesha wa siku ya tohara iliitwa "*kuraria Murungu*" ambako pombe iliyotengezwa kwa miwa ilinywewa. Asubuhi na mapema, watahiriwa wa kiume walipakwa mchanga mweupe kwenye paji la uso. Mchanga huu ulitolewa mlima Kirinyaga (Mt.Kenya), makao makuu ya muumba wao. Watahiriwa wa kike walipakwa mafuta ya mmea wa "mbariki" (mbono) . Watahiriwa walikaribishwa kwa wimbo ufuatao:

"Ciana irogia thayu.
Thaai thathaiya Ngai thaai.
Ciana irogia thayu
Thaai,thathaiya Ngai thaai.
Tafsiri;
(Watoto wapate amani
Tumsifu Mungu (Ngai) atupe amani
Watoto wapate amani
Tumsifu Mungu (Ngai) atupe amani).

Baada ya sala,watakaotahiriwa walirudi kila mmoja nyumbani kwao. Wasichana walipiga dira na kurembeshwa kwa shanga walizopewa na wanawake jamaa zao, kama hidaya . Pia , walivikwa njuga mguu wa kulia. Msichana alisindikizwa kwa nyimbo na waimbaji katika msafara kuelekea ile nyumba watakaokaa baada tya kutahiriwa. Wanapokutana wote mahali pale panatakaswa na mganga (*mundu mugo*) na kurashiwa pombe ili kupata radhi za mababu .Wavulana nao waliposikia pombe imepulizwa, walipiga foleni, wakakimbia mpaka pale palipokuwa na mti wa mgumo. Pale palipo na mgumo paliaminiwa kuwa mahali patakatifu. Yule mvulana aliyefika

kwenye mugumo akiwa wa kwanza alishangiliwa na kufanywa kuwa kiongozi wa kundi lile. Wavulana wote walipanda ule mti na kukata matawi yaliyoangushwa chini. Hii ilikuwa ishara ya kuonyesha kuwa wale wavulana wa kiume wamekaribia muumba wao zaidi kimadaraka. Ndiposa wakikuyu wakawa na methali isemayo,

"Mundurume ni Ngai ya Keri",

(Mwanaume ni mungu wa pili).

Kuokota majani kwa wasichana kuliashiria kuwa watakuwa kazi yao ni kumtumikia mume na watoto,na jamii kwa jumla. Pia, ilikuwa ishara ya kuashiria jukumu la wanawake la kunadhifisha nyumba . Wakati wa kiapo, ulipowadia wavulana walikula yamini kuwa watalinda jamii yao na kutunza siri zote za jamii. Wasichana hawakulishwa kiapo cha aina yoyote. Jogoo wa kwanza alipowika alfajiri, wasichana walilishwa chakula maalum, na baadaye wakavua nguo zote. Walibaki na mkufu watakaoutoa kama tuzo kwa ngariba. Wasichana wote walipelekwa mtoni na kwa vile maji yalikuwa baridi waliingia mtoni hadi maji yakawafika kiunoni . Waliangusha matawi waliyokuwa wameyabeba majini, ishara kuwa wamefukuza tabia zao za utoto.

Maji baridi yalifanya sehemu zao za siri kufa ganzi na hivyo kupunguaza uchungu zitakapokatwa. Baada ya dakika thelathini hivi, walitoka majini na kuelekea mahali ambapo tohara ilifanyika. Nyimbo za huzuni ziliimbwa. Tohara ilifanyika mahali palipoitwa "*itiiri".* Wasichana waliketi juu ya ngozi ya ngombe huku wakizungukwa na wanawake jamaa zao. Walirashiwa maji baridi katika sehemu zao za siri. Gwiji wa tohara alijongea akiwa amevalia mavazi ya kuogofya yenye rangi za kutisha. Walitahiriwa mmoja baada ya mwingine huku wakirushiwa maziwa yaliyochanganywa na dawa yenye uwezo wa kuwaponya haraka. Kuanzia hapo, wakapata jina mpya la "*irui*" (yaani watahiriwa) . Walipelekwa kwa nyumba ambapo walilala sakafuni walikotayarishiwa. Kitanda kilikuwa majani maalum yenye harufu ya kuvutia (*mirereshwa*). Majani haya yalinuiwa kufukuza nzi na kuondoa harufu mbaya. Mgeni hakuruhusiwa kuwatembelea kwa siku nne. Wavulana pia walifika mtoni asubuhi na mapema. baadayewalitembea hadi mahali watakapotahiriwa palipoitwa "*itiiri"*. Kwa kutumia visu vyake vilivyotiwa makali vikapata, ngariba aliwatahiri wale wavulana mmoja baada ya mwingine. Iwapo wavulana walikuwa wengi, wangaliwaita ngariba wawili. Baada ya hapo wale watahiriwa waliingia katika chumba chao kiolichoitwa "*kiganda"*.

Malipo ya ngariba yalijadiliwa na akina baba wa wavulana wanaotahiriwa. Watahiriwa walikaa siku saba katika "*kiganda"* (kibanda). Hapa walipata mafunzo kutoka kwa wasimamizi wao walioitwa *"atiri*". Mafunzo yale yalisheheni mila na destui za jamii, matarajio ya jamii kutoka kwao na majukumu wanayotakiwa kuyachukua kama wanaume. Wale waliotahiriwa kwa sasa waaliitwa "*shiumiri*" . Wanawake walipika chakula kingi na kizuri pale nyumbani na kuwapelekea *"shuimiri*" na wasimamizi wao. Hawakukaribia mahali pale, bali waliweka chakula mbali, nao wasimamizi walikiendea kile chakula. Majani ya migomba yaliyoitwa "*machoya*," ndiyo yaliyotumika kama sahani.

Walifunzwa aina ya densi na wasimamizi wao iliyoitwa "*waine*". Siku ya nane asubuhi na mapema, kila mvulana na msimamizi wake walielekea nyumbani kwao, baada ya kukibomoa kibanda walimokaa. Nyumbani kila mvulana alikaribishwa kwa sherehe kubwa ambapo kondoo alichinjwa. Mvulana aliendela kujifunga shuka kwa siku kadhaa kwa vile hajapona kabisa.Siku ya kuondoa ile shuka na kuvaa suruali yake, kulifanywa sherehe kubwa iliyoitwa "*Thiga"* kuonyesha kuwa mvulana amevuka ngambo ya utu uzima. Basi mvulana akawa amejamiishwa kuwa mtu mzima.

Jamii ya wakikuyu ilichukulia sherehe ya tohara kwa umuhimu mkubwa. Sherehe hii iliwaleta watu pamoja, wakala na kunywa pamoja, na waliokuwa wamekosana walipata fursa ya kujumuika pamoja na kusameheana. Jambo hili liliendeleza umoja wa jamii. Kwa watahiriwa huu ndio uliokuwa wakati wa kufunguliwa milango ya siri za jamii, hasa kuhusu unyumba na utawala . Basi wakikuyu wakasema;

"*Kurua, kugurana na kuriha thiri gutiirigagwo*"

(Hakuna majuto katika kutahiri, kuoa na kulipa deni)

Shughuli zote zilizozunguka tukio zima la tohara zilimulika zaidi majukumu yatakayotekelezwa na vijana . Wavulana walitayarishwa kuchukua nafasi za juu na za heshima kama vile hatamu za uongozi, ilhali wasichana walitayarishwa kuchukua hatamu za utumishi.

1.2.6 Ada za ndoa

Jamii ya wakikuyu ilithamini sana ndoa. Ubasha, ukapera na useja ni mambo ambayo hayakujulikana katika janibu hizo. Mbari ziliendelezwa kupitia kwa ndoa. Jamii nzima ilihusika katika ndoa. Ndoa ilionekana kukamilika pale watoto walipopatikana.

Utasa na ugumba zilitazamwa na jamii kama laana kutoka kwa mababu au pengine dhihirishao la hasira za miungu. Ukosefu wa watoto katika ndoa unaweza ukatokana na udhaifu wa mwanaume au mwanamke, lakini jambo hili lilipotokea, lawama zote zilimrudia mwanamke. Methali ifuatayo inaibua ukweli huu;

"*Mutumia utari mwana akura ndonaga mutahiri mai."*

(Mwanamke asiyekuwa na mtoto anapozeeka hukosa wa kumchotea maji).

Hii ina maana kuwa mwanamke huyo hakupata wa kumsaidia kwa sababu jamii ilimtazama kama msababishi wa ukosefu wa watoto katika ndoa yao. Alipofikishwa umri wa kuoa au kuolewa mvulana alikuwa na uhuru wa kumchagua mchumba wake, hata ingawa, uamuzi wa mwisho ulikuwa na wazazi. Mvulana alipompenda msichana, na akakata shauri kuwa anamfaa kama bibi, siri hii aliwafichulia masahibu wake wa karibu.Wale wandani wake walichukua jukumu la kumchunguza yule msichana kama ana bidii kazini au la. Hapa ni bayana kuwa ufaafu wa msichana ulichunguzwa zaidi kuliko ule wa mvulana. Msichana hakupewa nafasi ya kumchunguza mvulana . Wale marafiki mara kwa mara walijificha karibu na mahali yule msichana alikuwa akifanyia kazi. Walifanya uchunguzi wa kina kwa sababu jamii iliamini kuwa msichana aliyetarajiwa kuwa mama baada ya kuolewa lazima awe na uwezo wa kuathirii mkondo wa maisha ya watoto wake na bwanaye. Wazo hili lilipitishwa kwa methali isemayo;

"*Kana ka ngari gakunyaga ta nyina".*

(Mtoto wa chui hukwaruza kama mama yake).

Iliaminika kuwa mwanamke muovu na goigoi aliipalilia hulka hii yake kwa watoto kupitia kwa malezi. Baada ya yule msichana kuchunguzwa na wale marafiki wa mvulana, walitoa uamuzi wao. Ikiwa waliridhika kuwa yule msichana ana jitihada kazini, basi walimtembelea msichana kumwambia nia ya mmoja wao. Iwapo walikubalika, mvulana aliwajulisha wazazi wake. Wazazi wa mvulana walitayarisha pombe ambayo ingepelekwa kwa wazazi wa msichana.Wazazi wa mvulana walipofika kwa wazazi wa msichana, msichana aliitwa na kuombwa ampe babake pombe kwa kutumia pembe maaluim (*ruhia*) iliyotengewa kazi ile. Kabla ya kumpa babake, msichana aliionja ile pombe kwanza, hii ikiwa ni ishara ya kukubali kuposwa na wale waliokuja. Baada ya sherehe hii fupi, wazazi wa mvulana walirejea nyumbani na

kuanza kusakanya mbuzi na kondoo watakaopelekewa wazazi wa msichana kama sehemu ya kwanza ya mahari (*ruracio).*

Malipo ya mahari katika jamii ya Wakikuyu ni jambo lililoendelea kwa kipindi chote cha uhai wa wahusika.. Hata ingawa, baada ya kulipa kwa muda mrefu kiasi kilichotakikana, kuna sherehe iliyojulikana kama " *gutinia kiande*" (kukata mguu wa mbele wa kondoo uliochomwa). Sherehe hii ilikuwa dhihirisho la ishara kuwa mwanamume amemaliza sehemu ile muhimu ya mahari waliyokubaliana na wakwe zake. Hata hivyo kuwatembelea wazazi wa msichana na kuwapelekea tuzo mara kwa mara ni jambo lililoafikiwa. Ulikuwa mwiko kulipa mahari yote wakati mmoja, hata ikiwa wazazi wa mvulana walikuwa na uwezo huo. Mahari yalitakiwa kulipwa kwa awamu nyingi, jambo ambalo mpaka sasa linaendelea. Hii ni kwa sababu sherehe hii ya ulipaji wa mahari iliwaleta pamoja, na hata leo huwaleta watu pamoja.

Baada ya waazazi wa mvulana kupeleka mahari kiwango fulani, waliruhusiwa kumchukua msichana. Ulipaji wa mahari ulitazamwa kama kumnunua msichana, na imani hii ilimfanya mvulana kuwa na mamlaka makubwa juu ya mke wake. Mvulana alimwona mke wake kama mali yake binafsi aliyoinunua. Familia ya mvulana pia ilimtarajia msichana aliyeolewa aitumikie familia hiyo na kufuata maadili yake.

Dhuluma kwa mwanamke ziliendelea kudhihirika katika mahusiano ya ngono. Ilichukuliwa kuwa ni haki ya mwanaume kushirikiana kimapenzi na mke wake wakati wowote apendao bila ya kuwekewa vikwazo vyovyote na mke wake. Hii iliendelezwa na dhana kuwa kwa vile mwanaume amemlipia bibi yake mahari, alikuwa na haki ya kumtendea apendavyo. Wachege (1992), akitafiti kuhusu mahusiano ya ngono miongoni mwa Wakuria anasema kuwa mwanaume wa Kikuria alikuwa na uhuru wa kumtoa mke wake akidhi mahitaji ya kimwili ya marafiki zake. Ingawa jambo hili lilibakia katika jamii husika, lililo dhahiri ni kuwa mwanamke alichukuliwa kama mali ya mwanamume, na hivyo mwanamume alikuwa na uhuru wa kumtoa mke wake awafurahishe marafiki zake.

Sherehe ya kumpeana msichana kwa mchumba wake iliitwa, "*guthenya ngoma*". Jamaa na marafiki wa pande zote mbili walijumuika pamoja. Kulikuwa na chakula na vinywaji kwa wingi. Kondoo kama watano au sita walichinjwa. Wazazi wa msichana wakiwa na uwezo, ndama pia alichinjwa. Msichana aliyeposwa alipewa figo za

kondoo aliyechinjwa. Mila za Wakikuyu hazimruhusu mwanamke kula sehemu fulani za nyama ya kondoo, ng'ombe au hata kuku. Pia, ilikuwa si halali mwanamke kumchinja mnyama. Ikiwa mwanamke ni mjane,mtoto wake mkubwa wa kiume ndiye huchinja. Ikiwa hana mtoto mkubwa wa kiume, limbidi kumtafuta mwanamume jirani amchinjie. Hapo ndipo wakikuyu walilipigia jambo hili kijembe kwa kudai kuwa,

"*Mutumia ndaaturaga mutwe*".

(Mwanamke hapaswi kupasua kichwa cha mnyama aliyechinjwa).

Upande wa mvulana ulitoa zawadi kwa wazazi wa msichana kufidia vifaa vyote ambavyo msichana alipoteza au kuharibu wakati wote yule msichana alipokuwa nyumbani.

Mvulana alitayarisha nyumba vilivyo. Kisha, aliwajulisha wale vijana marafiki zake walomchunguzia msichana kuwa sasa yuko tayari kumpokea mchumba wake. Wale marafiki walianza mara moja kuchunguza mienendo ya msichana. Baada ya siku sita, saba au nane,walipohakikisha alipokuwa yule msichana, walimvizia na kumwinua kimzegamzega hadi kwa nyumba ya yule mvulana. Msichana alijifanya kutokubali, hivyo alipiga mayowe ya kuomba msaada, huku akilia kwa machozi ya mamba. Jamii ilifahamu mayowe na kilio hicho, hivyo hakuna aliyejishughulisha sana, isipokuwa wanawake wachache waliojidai kutaka kumwokoa hata ingawa wao pia walielewa kilichokuwa kikiendelea.

Kitendo cha kumnyemelea mwanamke na kumnyanyua kilimshushia hadhi na kumfanya kama aliolewa bila hiari yake. Kitendo hiki pia kilialika dhana kuwa mwanamke wakati wote lazima ashurutishwe kufanya jambo. Pindi aolewapo,mwanamke huwa ametiwa shemere na mume wake. Alihitajika kumtii mume wake kwa heri na kwa shari. Wazo hili lilishadidishwa na methali isemayo:-

"Mumbia aume omburagwo na njuguma".

(Anayewakatalia wanaume jambo huadhibiwa kwa fimbo).

Akiwa kwa mume wake, marafiki, jamaa na majirani walimtembelea huku wakimpongeza na kumzawidi zawadi kochokocho. Mwanamke huyo hakuruhusiwa kuonekana ovyo ovyo na watu isipokuwa waliomtembelea tu. Kwa muda wa siku nane,alibaki kwa nyumba bila kutoka nje. Alipokuwa akienda mtoni kuoga, alijifunika uso, huku akisindikizwa na wasichana marafiki zake ambao walitumika kama kizibo.

Kwa sababu swala la ubikira lilithaminiwa sana katika jamii ya wakikuyu, kitanda kilitayarishwa na shangazi wa yule mvulana ule usiku wa kwanza. Ngozi maalum iliwekwa kitandani kwa maksudi ya kudhibitisha ubikira wa yule msichana. Siku iliyofuata asubuhi, mvulana alimpelekea shangazi yake ngozi ili aikague. Kama ile ngozi ilipatikana na damu, hii ilikuwa ishara tosha kuwa yule msichana alikuwa bikira. Msichana aliyepatikana kuwa bikira aliheshimiwa sana, na wazazi wake walipewa tuzo nyingi. Hapa tunaona thamani ya msichana inapimwa kwa mizani ya ubikira wake. Nafasi ya msichana kama binadamu wa kuheshimiwa ilidhalilika au kuimarika baada ya hali ya ubikira wake kujulikana.

Mvulana kwa upande wake hakuwa na kigezo chochote cha kupimia thamani yake kulingana na ubikira. Jamii ilichukulia kuwa mvulana hakuwa na dosari lolote na alikuwa sawa katika hali zote. Hapa tunaona jamii ikipendelea mwanamume. Mvulana angetambulika kuwa hakuwa bikira angetungisha mimba msichana kabla ya kumuoa. Kama hili lilitokea mvulana alihitajika kumuoa yule msichana, ndiposa wakikuyu wakalipigia vijembe jambo hili kwa methali isemayo;

"Wahira ihu wi kironda niwe ukagura",

(Ukimpachika mimba msichana aliye na kidonda ndiye utakayeoa).

Ikiwa mvulana alikataa kumuoa yule msichana basi alihitajika kulipa kiasi fulani cha kondoo au mbuzi kulingana na makubaliano yake na wazazi wa msichana. Shangazi ndiye aliyechukua jukumu la kumdadisi msichana aliyeolewa pamoja na mumewe kuhusu uwezo wao wa kuendeleza kizazi. Ikiwa kulipatikana kasoro jambo hili liliripotiwa kwa halmashauri ya wazee ambao walilijadili na kutoa ushauri wao kabla ya siku nane kuisha.Ikiwa mambo yote ya mvulana na bibi yake yalikuwa shwari, basi siku ya tisa kuliandaliwa hafla kubwa ya kumkubali rasmi yule msichana katika familia ya kina mvulana. Kuanzia hapo yule msichana akawa ameanza kujumuishwa katika ukoo wa mume wake. Katika hafla ile, kondoo mnono alichinjwa na msichana aliyeolewa alipakwa mafuta ya kondoo yule. Kwanzia siku ile alipata kibali rasmi cha kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za ukoo ule. Ikiwa familia ni tajiri mwanamumme alikubaliwa kuoa mke wa pili hata ingawa aghalabu pendekezo la kuoa mke wa pili lilitoka kwa mke wa kwanza ambaye alipewa heshima kubwa .Wake walioolewa baadaye walipaswa kumtumikia na kumheshimu yule bibi wa kwanza (alijulikana kama *nyakiambi*). Lolote ambalo bibi wa kwanza angewashauri wake

wenza wangemsikiliza na kuyakubali mashauri bila pingamizi lolote. Ilikuwa ni muhali na ukiukaji wa kaida kwa mwanamke kuolewa na zaidi ya mume mmoja (Hata leo ni hiivyo tu). Hapa tunaona jamii ikimpendelea mwanamumme na kumpa uhuru wa kuoa zaidi ya mke mmoja. Wakati mwingine, uhasama ulitokea kati ya wake wenza, ndiposa wakikuyu wakaibua methali isemayo;

"*Aka eri ni nyungu igiri cia urogi*",

(Mabibi wawili ni sawa na vyungu viwili vya sihiri).

Waandishi wengi wa kiafrika wamejitokeza kulishughulikia swala hili la uke wenza. Mmoja wa waandishi hao ni Chacha (1982) katika tamthilia yake ya "*Mke Mwenza*". Mwandishi huyu anatuonyesha athari za uke wenza kupitia kwa wahusika wawili, Boke na Robi. Boke anapofahamishwa na mumewe Chahe nia yake ya kumwoa Robi kama mke wa pili, anapanga jinsi ya kumwangamiza mume wake kwa sumu.Hata ingawa anafaulu katika mipango yake, yeye pia anapata madhara ambayo hakuyatarajia. Ingawa uke wenza unakubaliwa katika jamii nyingi za kiafrika unasababisha mafarakano, wivu na hata kifo miongoni mwa wahusika.

Swala la talaka katika jamii ya wakikuyu lilikuwa nadra sana. Talaka ilihalalishwa iwapo mambo yasiyokubaliwa katika jamii yangetokea. Mambo hayo ni kama vile uchawi, wizi na kiwango cha juu cha uzinzi kwa upande wa mwanamke. Ieleweke wazi kuwa mwanamume mzinzi hakupewa talaka na mkewe. Jamii ilichukulia kuwa uzinzi wa mwanamume ni jambo la kawaida na si kosa kubwa. Adhabu ilitolewa kama tu angezini na bibi ya mwanamume mwingine. Kuwepo kwa watoto katika ndoa kulikuwa kikwazo cha talaka. Watoto walikuwa kama kiunganishi cha maisha kati ya bibi na bwana, na mbari nzima kwa jumla. Iwapo lazima talaka itekelezwa, watoto walitunzwa na mama yao. Baada ya talaka, mume alikuwa na haki ya kudai nusu ya mahari aliyotoa. Iwapo yule mwanamke angeolewa na mwanamume mwingine, basi mahari yote ya mume wa kwanza yangerejeshwa. Hii ni kwa sababu mahari yalitazamwa kama gundi iliyoshikanisha na kudumisha uhusiana baina ya koo hizi mbili. Ni bayana kuwa asasi ya ndoa ni kipengele mojawapo cha jamii kilichompa mwanamke nafasi duni.

1.2.7. Swala la Uzee na Kifo

Wanaume wenye mali waliwaoa wake wengi, na walipozeeka walitunzwa na wake zao waliokuwa wa umri mdogo, na pia watoto, wajukuu na hata vitukuu. Wanawake walipozeeka walitunzwa na wakazamwana wao pamoja na wajukuu na vitukuu. Hata hivyo lilikuwa ni jukumu la jamii nzima kuwatunza wazee. Waliotaka ushauri wa wazee waliwatembelea. Wazee walitazamwa na jamii kama rasilimali kubwa kwa sababu umri huo ulishabihishwa na hekima na busara nyingi. Jamii ilifuata methali inayowasabilihisha wazee na jiwe kongwe ambalo halifunikwi na maji;

"*Kahiga gakuru gatiagararagwa ni mai*."

Methali inamaanisha kuwa busara ya wazee ni kubwa sana na imani yao haiwezi kutikisika.

Majira ya jioni wazee waliwatambia watoto ngano na kuwategea vitendawili huku wakiwashauri. Watoto kupitia elimu hii walijua historia ya jamii yao, mila na desturi na kaida zilizoitawala jamii yao. Makao ya wazee yaliitwa "*Thingira".* Mzee angejihisi kuwa umri wake umezidi mno na anachungulia kaburi aliwaita watoto wake wa kiume, hasa yule mkubwa. Pia aliwaalika wazee wengine wawe mashahidi wa wosia wake. Kila mtu katika familia alikuwa mwangalifu asije akamuudhi mzee na hivyo akakosa radhi zake. Kulikuwa na imani kuwa hasira za mzee zingeleta balaa kubwa na laana kwa wahusika na hata jamii zima kwa jumla. Methali iliyotumiwa kuwatahadharisha wanajamii wasiwaudhi wazee ni;

"*Kirumi kia mundu uri muoyo ni kiuru gukira kia mundu mukuu*";

(Laana ya aliye hai ni hatari kuliko ya aliyekufa).

Wakati wa kutoa wosia wake alieleza Kinagaubaga mipaka ya shamba lake. Aligawia watoto wake wa kiume kila mtu kipande chake. Mifugo pia aligawa kwa wavulana wale. Mke wake hakuwa na fursa ya kutoa maoni yake kuhusu urithi na wale watoto wa kike hawakuwa na haki ya kudai chochote. Jambo hili linadhihirisha nafasi duni aliyopewa mwanamke katika jamii ya wakikuyu. Baada ya kifo cha baba mtoto mkubwa wa kiume ndiye aliyechukua hatamu ya uongozi wa familia wala si mama yao.

Wakikuyu waliamini kuwa hata baada ya kifo, roho ya aliyekufa ilibaki katika familia na hivyo kutozingatia ushauri wa aliyekufa kungealika adhabu kutoka kwa pepo

wake. Baada ya wasia kutolewa, yule mzee alikuwa radhi kukumbana na mauti yake .Ilikuwa ni muhali kwa mtu kufia kwa nyumba . Jamii iliamini kuwa mzee angefia kwa nyumba , nyumba hiyo na eneo lote kwa jumla litamilikiwa na pepo za mauti . Hata hivyo mzee alipoonekana akiwa katika hali mahututi aliondolewa kwa nyumba na kupelekwa kichakani . Watu walisubiri hadi alipokufa kisha mwili uliliwa na wanyama mwitu. Ikiwa pengine mwili haukuliwa ilisemekana kuwa yule mtu alikuwa mchawi. Watoto na watu wa umri wa makamo walipokufa, jambo hili lilichukuliwa kuwa laana, uchawi au hasira za miungu. Kifo cha mzee kilitazamwa kama ada tu ya maisha na kilitarajiwa. Mtu aliyemuua mwanaume alilipa fidia ya kondoo mia moja. Aliyemuua mwanamke alilipa fidia ya mbuzi thelathini. Hapa tunaona thamani ya mwanaume ikiwa zaidi ya mara tatu ya mwanamke. Hili ni dhihirisho tosha la thamani inayoambatanishwa na maisha ya wanaume na yale ya wanawake. Ubaguzi huu unaendelzwa na jamii kupitia kwa methali zinazowatukuza wanaume kama vile.

"*Mundurume ni ngai ya keri*"
(mwanaume ni mungu wa pili)
"Maitho ma arume ti mambo);

Mambo ni mdudu mdogo kama sisimizi aliye na macho madogo. Tashbihi hii ikitumika kumpa mwanaume uwezo mkubwa wa kuona na kutambua mambo akilinganishwa na mwanamke.

Jamii hii ya wakikuyu pia ilinena kuwa;

"*Ugi wa arume utemaga ta kahiu*" .
(Werevu wa wanaume hukata kama kisu).

Itikadi ya kuumeni , sawa na methali nilizotaja hapo juu, husaidia kukoleza imani kuwa mwanamke ni kiumbe duni ilhali mwanaume ni mtukufu. Kasumba hii imezama kikiki katika mawazo ya wanajamii hawa kiasi cha kuwafanya waamini kuwa malipo ya aliyewauwa yanapaswa kuwa hivyo. Kifo, kama hatima ya maisha ya mwanajamii kiliibua mtazamo wa wanajamii kuhusu umilikaji wa mali.

1.3 Mada ya Utafiti

Jamii ya Agikuyu huongozwa na mfumo wa itikadi wa kuumeni. Mwanamume katika jamii ya Agikuyu hutambuliwa kwa njia fulani. Utafiti huu umejikita katika

kuchunguza jinsi mwanamume anavyotambuliwa katika jamii ya Agikuyu. Chomba (2005) anasema kuwa mwanamke katika jamii ya Agikuyu anasawiriwa kwa njia hasi isiyo ya heshima na inayomdhalilisha. Alitumia methali za jamii ya Agikuyu kama matini. Madai haya ndiyo yaliyochochea mtafiti na hasa ndiyo kitovu cha utafiti huu. Utafiti huu una lengo la kubainisha jinsi mwanamume anavyotambuliwa katika jamii ya Agikuyu, methali zikitumika kama matini. Kama anavyosema Kenyatta (1938), kazi za sulubu, zilizohitaji nguvu nyingi zilipewa mwanamume, kumaanisha mwanamume alitambuliwa kama kiumbe mwenye nguvu nyingi. Hivyo basi mtafiti akapata ari zaidi za kufanya utafiti huu. Utafiti huu unajibu swali:- je, mwanamume hutambuliwa vipi katika jamii ya Agikuyu kupitia kwa methali za jamii ya Agikuyu?

1.4 Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kudhihirisha jinsi mwanamume anavyotambuliwa katika jamii ya Agikuyu kwa kutumia methali kama matini. Uchunguzi umemulika hasa utambulisho wa mwanamume katika jamii ya Agikuyu kwa kutumia mikakati mitano ya usemi. Tumetimiza shabaha hii kwa:

i). Kutathmini na kubainisha mahusiano kwa mujibu wa jinsia katika jamii ya Wakikuyu.
ii). Kudhihirisha jinsi Wakikuyu wanavyomtambulisha mwanamume kupitia kwa methali
iii). Kubainisha majukumu na nafasi ya mwanamume kama inavyodhiririka katika methali za Agikuyu.

1.5 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali ya utafiti yafuatayo:

i). Methali za jamii ya Agikuyu huibua uhalisia wa mahusiano ya kijinsia kwa njia gani ?
ii). Methali za Agikuyu humtambulisha mwanamume kwa njia zipi ?
iii). Methali hubainisha nafasi na majukumu ya mwanamume katika jamii ya Agikuyu kwa kutumia mbinu gani ?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu unatarajiwa kuwa wa manufaa katika kupanua uelewa wa methali katika utamaduni wa jamii ya Agikuyu. Hii ni kwa sababu methali zimechanganuliwa kwa undani kwa kutumia mikakati mitano ya usemi. Methali hizo zimeorodheshwa katika matapo matano ambayo ni methali za kiuchumi, kisiasa, kijamii, kimaumbile na kisaikolojia. Utafiti huu pia utafaidi na kuchangia katika uwanja wa uchanganuzi usemi. Wanafunzi wanaotaalamia somo la Kiswahili katika viwango mbalimbali hasa vyuo vikuu watafaidi sana kwani ile mikakati mitano ya usemi imechanganuliwa kwa undani. Mikakati hiyo ni urejelezi, nomino, ubishi, mkabala na ufifizaji.

Watakao faidi pia kutokana na utafiti huu ni walimu wa somo la Kiswahili, uwanja wa Uchanganuzi Matini. Nadharia Iliyoongoza utafiti huu ya Uchanganuzi Hakiki Usemi, mkabala wa kihistoria imeelezwa kwa ufasaha.Vyuo vinavyofindisha lugha ya Kiswahili uwanja wa uchanganuzi hakiki usemi vitapata msaada kutokana na kazi hii. Kazi hii itachangia ufafanuzi wa kina wa nadharia ya uchanganuzi hakiki usemi mkabala wa kihistoria, waasisi wake, sifa muhimu za mkabala wa kihistoria na mikakati ya usemi.

Utafiti huu umejaza pengo lililoachwa na tafiti za hapo awali kama vile utafiti wa Chomba (2005). Chomba alitafiti kuhusu Usawiri wa Mwanamke Katika Methali za Agikuyu. Kazi ya Chomba ndiyo iliyochochea utafiti huu ili kutathmini na kubaini jinsi mwanamume anavyotambulika katika jamii ya Agikuyu. Ninatumai kuwa kazi hii itachochea utafiti zaidi katika nyanja hii.

1.7 Upeo na Mipaka

Kuna njia nyingi za kutambulisha mwanamume katika jamii ya Agikuyu. Utambulisho wa mwanamume unaweza kupitia kwa nyimbo, vitendawili, methali na hadithi. Utafiti huu ulijikita katika utambulisho wa mwanamume katika jamii ya Agikuyu kupitia methali. Methali zilichaguliwa kwa sababu kama anavyosema Nkweka (1978:97),"…… methali ni semi au kauli zenye busara na mafunzo kuhusu maisha na mahusiano ya watu. Ukweli na Umuhimu wa methali yoyote hutegemea mazingira inayotumika. Methali ni kauli za mkato (fupi) na zenye kufikirisha. Methali zadai ujuzi wa kuzifafanua, maana pengine huwa ni mfumbo. Hutumika ili kumjuza mtu ukweli fulani, au kumshitua apate kudadisi mambo au kujisahihisha anapokosa……..".

Wazo hili la Nkwera lilinielekeza katika juhudi za kutathmini ufaafu wa matumizi ya methali mbalimbali kwa kuzingatia muktadha ambamo zimetumika.

Mtesigwa (1989) anasema, methali huvutia zaidi iwapo itatolewa kwa maneno machache na hasa ikiwa, licha ya hayo, pia maneno hayo yanagonga ndipo katika kukisema kilichokusudiwa kusemwa. Kauli hii pia ilinichochea kutumia methali katika utafiti wangu ili nigonge ndipo katika utambulisho wa mwanamume katika jamii ya Agikuyu nikitumia methali kama matini. Uteuzi wa methali kama matini katika utafiti huu ilichangiwa zaidi na ukweli kwamba methali huwa hazibadiliki na hutumia maneno machache na ya busara kupitisha ujumbe uliokusudiwa. Kupitia kwa methali, tunafahamishwa, tunaelimishwa na kuburudishwa na hatimaye kutimiza lengo kuu la utafiti huu.

Methali arubaini na tano (45) zilitumika kutimiza malengo ya utafiti huu. Idadi hii iliafikiwa kwa kuzingatia uwezekano kuwa matini inayoshughulikiwa ikichunguzwa kwa methali kiasi hicho itaonyesha ruwaza kamili ya kilichoazimiwa ili kutoa rai zenye mashiko.

1.8 Maelezo ya Istilahi.

Jamii - Kundi la watu mahsusi waliounganishwa kwa misingi ya lugha, desturi na mila.

Methali - Huu ni usemi wa kisanii, uliotumia maneno machache na ya busara kuelezea hadithi ndefu. Methali huwa fumbo na huwa na maana fiche.

Mikakati ya usemi-. Matumizi mahsusi ya lugha yanayolenga kuonyesha tofauti za hali, kijamii, kisiasa na kiisimu. Mifano ya mikakati ni ule wa urejeleo, wa nomino, wa ubishi, wa mkabala na wa kufifiza.

Paremiolojia - Utaalam ambao unashughulika na yale yanayohusiana na methali.

Taasubi ya Kiume- Fikira iliyoko ndani ya wanaume kujihisi kuwa wao ni bora zaidi wakilinganishwa na wanawake. Wanaume kujihisi wenye maumbile bora wakilinganishwa na wanawake.

Usemi - Matamshi ya watu. Yale yanayosemwa na jamii, kikundi cha watu au mtu binafsi, kwa kutumia mdomo.

Uwezo Kiume - Hali ya mwanaume kujihisi na kujiona kuwa bora na wenye nguvu wakilinganishwa na wanawake. Hali ya wanaume kuwa na nguvu ya kufanya au kutenda mambo. Huu ni uwezo unaoambatanishwa na waume.

Uana - Hali ya kuwa mke au mume. Pia huitwa Umenke au Jinsia. Kawaida mwanadamu huwa mwanamke au mwanamume.

Ubabe - Hali ya kujihisi kuwa na nguvu zaidi kuliko wengine, hasa wanaume wanavyojihisi kuwa na nguvu kuliko wanawake. Kujihisi kuwa bingwa na shujaa. Ujanja na hila za kutumia nguvu. Mfumo wa ubabedume huzichukulia amali za kiume na mawazo yao kama kaida ya kufuatwa katika jamii nzima.

Utambulisho - Kuwa na jambo linalokufanya ujihisi kuwa tofauti na wengine au kuwa na uhusiano na wengine. Kuwa na kitu cha kukubainisha kutoka kwa wengine. Utambulisho waweza kuwa wa kibinafsi, wa kijamii au wa kitaifa.

Utamaduni - Maisha ya kawaida ya watu husika, mazoea yao kama vile dini, mila, siasa na mfumo wa kiuchumi.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDISHI NA MISINGI YA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Katika sura hii, utafiti uliangazia maandishi ya wasomi mbalimbali. Pia, utafiti ulishughulikia tafiti zilizofanywa awali kuhusu mada hii. Kwa uyakinifu, utafiti huu ulimlika machapisho yanayomhusu mwanamume na yanayohusu methali kwa mujibu wa upeo na mipaka ya utafiti.

Kwa kutumia mihimili ya nadharia iliyotumika katika utafiti huu, mtafiti alijadili kwa kifupi asili za tofauti za kiuana kulingana na historia. Utafiti huu ukiongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi mkabala wa Kihistoria, mikakati ya usemi ilitafitiwa, na ndiyo iliyokuwa mwongozo. Ufaafu wa nadharia iliyochaguliwa ulidhibitishwa.

2.2 Chimbuko la Tofauti ya Nafasi ya Mwanamume na Mwanamke Katika Jamii

Engels (1975) anasema kuwa hapo mwanzo, mwanamume na mwanamke walidhaminiwa sawa katika jamii. Jamii ziliishi maisha ya ujima. Mfumo wa utawala wa ubabeume ulianza pale jamii zilipoanza kubadilika na kuwa zenye ustaarabu. Hii ilitokea baada ya jamii kugundua kuwa kazi za waume za kuwinda na ufugaji zilikuwa na faida kubwa zikilinganishwa na kazi za nyumbani za wanawake. Mwanamume alipoendelea kupata mali zaidi, wazo la mali ya kibinafsi lilizuka. Hapa ndipo shughuli zote za mwanamume zikaonekama kuwa muhimu kuliko za mwanamke. Huu ndio ulikuwa mwanzo wa mwanamke kuanza kumtegemea mwanamume kiuchumi. Usawa wa mwanamume na mwanamke ukafikia kikomo.

Kwa kuchanganua methali za Kikuyu na matumizi yake, utafiti ulichunguza kama hali hii inajitokeza katika jamii ya wakikuyu. Mfano wa methali zinazoonyesha tofauti kati ya mwanamume na mwanamke ni kama vile:-

“Atumia matithiyaga ita”

Wanawake hawashiriki vitani

Mutumia ndaturaga mutwe na ndaikagia ndahi ndua

Mwanamke hapasui kichwa cha kondoo aliyechinjwa wala hachoti pombe kutoka kwa kitoma.

2.3 Maandishi Kuhusu Utambulisho wa Mwanamume

Upekuzi wa vitabu, majarida na tasnifu za walionitangulia ndiyo iliyokuwa dafina mwafaka ya utafiti huu. Nilizingatia tasnifu zilizoshughulikia utambulisho wa mwanamume katika jamii yoyote ile ili ziwe msingi wa utafiti wangu. Katika Utendi wa Mwanakupona, ambayo ni kazi ya kubuni, mwanamume amepewa nguvu za kiungu. Ubeti wa 26 na 27, Mwanakupona anamshauri bintiye kuwa ni sharti amheshimu na kumtii mumewe kwani mume ndiye atakayeamua hatima ya bibi yake baada ya kufa, kuingia Paradiso au Jahanamu. Kuna uwezekano wa upigaji chuku katika kazi hii, lakini ni yakini kuwa msanii yeyote huchota malighafi yake kutoka kwa jamii inayomkuza. Maoni haya ya Mwanakupona yanaafikiana barabara na methali ya kikuyu inayosema,

" *Mbu ya mundurume itikagwo ni muthamaki"*
(unyende wa mwanamume huitikwa na mfalme).

Methali hii inaashiria kuwa kimaumbile, mwanamume hajaumbwa kama mwanamke, na hivyo anapopiga kamsa lazima kuna jambo lisilo la kawaida lililotokea na jambo hilo litashughulikiwa na mtu mwenye mamlaka kama mfalme. Utafiti ulichunguza kama dhana hii inajitokeza katika methali za Kikuyu. Ligami na Barasa katika Njogu (2006) walifanya utafiti wa tahakiki ya methali za Kiswahili. Wanasema methali ni falsafa ya watu. Methali ni falsafa kwa njia mbili;-

(a) Uwezo wa methali kuzingatia na kuchambua maisha kwa kina, kuangazia sehemu nyingi za maisha kama vile maarifa, ujuzi, ndoa, serikali na hata maswala ya kiungu.
(b) Huweza kudadisi na kueleza mambo kwa njia inayoelekeza, kama vile;- " Usitukane wakunga na uzazi ungalipo." (Kimani na wengine2004; 115)

Walijikita katika uhakiki wa kijumla wa methali za Kiswahili.

Kingei (1982) alishughulikia methali za Kikamba kwa kufuata misingi ya methali za Kiswahili. Alijikita zaidi katika muundo wa methali. Utafiti huu ulipiga hatua zaidi kwa kuzingatia maudhui katika kuchunguza jinsi mwanamume anavyotambulishwa katika methali za Kikuyu.

Wandera (1996) alichunguza usawiri wa mwanamke katika ushairi wa Kiswahili wa karne ya 1800 hadi 1900. Aligundua kuwa picha ya mwanamke Mswahili imejengwa kwa mielekeo ya utamaduni wa wakati huo. Utamaduni huu haukugandamiza mwanamke au mwanamume, bali ulitenganisha majukumu na nafasi ya kila mmoja kwa misingi ya vigezo vya uana, maumbile, sheria ya dini ya kiislamu, mila, siasa na mfumo wa kiuchumi. Wandera aliangazia utanzu wa Fasihi Simulizi. Mimi niliangazia utambulisho wa mwanamume katika methali za kikuyu, utanzu wa U.H.U. mkabala wa Kihistoria.

Okindo (1995) na Chomba (2005) walifanya tafiti zilizokaribiana sana;- Sura ya mwanamke, Okindo akiangazia sura ya mwanamke katika methali za Ekegusii, naye Chomba katika methali za Kikuyu. Okindo alitumia tafsiri huru au tafsiri sabilia. Chomba alitumia tafsiri maana. Katika utafiti huu wa utambulisho wa mwanamume, tafsiri iliyofaa zaidi ni tafsiri ya kimawasiliano au tafsiri huru. Katika muktadha wa jamii za kiafrika, mkuu wa familia ni mwanamume. Kwa sababu hii, baadhi ya methali katika jamii nyingi humshusha hadhi mwanamke. Mfano wa methali za kikuyu zinazomshushia hadhi mwanamke ni:-

a) *Muici na mundu muka akenaga akua*
   (anayeshirikiana na mwanamke katika wizi hupata afueni huyo mwanamke atakapokufa).
b) *Cia atumia ciitikagio ciarara*
   (yaliyosemwa na wanawake si ya kuaminika).
c) *Mundu muka na iguru itimenyagirwo*
   (mwanamke ni kama hali ya anga, hatabiriki).

Baadhi ya methali huashiria jinsia, umri na hadhi.

Kulingana na Liyong (1986), matendo mengi ya kishujaa katika jamii ya Waluhya yalitendwa na wanaume. Liyong anasema utamaduni wa Wakikuyu uliegemea kumfanya mwanamume awe shujaa na kumdhalalisha mwanamke. Mwanamume aliyemwona mwanamke aliyembeba mtoto vibaya aliruhusiwa kumwadhibu yule mama hata kama hakuwa bwanaye (Liyong; 1986:80). Anaendelea Kusema kuwa ndoa ilikuwa kwa manufaa ya mwanamume wala sio kwa manufaa ya mwanamke. Kulingana na Liyong, Watu waliotambulika katika jamii ya wakikuyu walikuwa sita, wanaume watano na mwanamke mmoja. Wao ni:-

i). Mugo wa Kibiru - alikuwa nabii mashuhuri wa jamii ya Wakikuyu.

ii). Waciuri -Alikuwa Kiongozi mahiri wa jamii ya Wakikuyu.

iii). Demi na Mathathi -Vizazi vya kwanza katika jamii waliokuwa na nguvu sana.

iv). Wamugumo -Pandikizi la mtu katika jamii aliyekula mbuzi mzima katika kikao kimoja na kunywa mabuyu matano ya maziwa.

v). Mzee Jomo Kenyatta -Kiongozi wa Wakikuyu aliyekuwa na uwezo wa kuongoza na kuunganisha watu wa jamii ya Wakikuyu.

vi). Wangu wa Makeri - Mwanamke aliyekuwa kiongozi wa Wakikuyu. Katika enzi yake wanaume walidhulumiwa sana.

Utenzi wa Hati, ubeti wa kumi na tatu (13) unasema;

Upishi mwema kujua
Nna mume kumridhia
Nneno analokwambia
Kwako itakuwa taa.

Katika utenzi huu, binti anashauriwa kuwa ni muhimu awe na upishi mwema ili chakula chake kimridhishe mumewe. Kisha, yote atakayoambiwa na mumewe ayatilie maanani kwani hayo ndiyo yatakayomwongoza maishani (Jahadhmy: 1997:15)

Mwanamume anaonekana kuwekwa mbele ya mwanamke na jamii yake;

"...Kazija anamchukia mwanamume ... sababu amewekwa mbele, sijui na nani.…Daima atamchukia mwanamume kwa sababu hiyo." (Mohamed: 1980: 1).

Ni wazi hapa kuwa mwanamume kila wakati huwa anaonekana bora kuliko mwanamke.

Ubabe na ukike hujitokeza katika usemi wa kila siku katika tafsiri tofauti (Frosh na wengine; 2002:3). Kuna njia za kitamanduni zinazowapa wanaume na wavulana nafasi inayotilia mkazo ushupavu wao, kutaka kuchukua hatua, iwe ina madhara au haina au inawajibika (Uchendu; 2005). Uchendu alifanya utafiti wa wanafunzi wa chuo kikuu cha Nigeria kule Nkukka. Aligundua kuwa ubabe katika vijana wa kiume ulihusishwa na umbo la mwili, kisaikolojia na kibayolojia. Kwa umbo la mwili, wavulana walitamani kuwa na sauti nzito, nywele fupi, malaika mwilini na mavazi

yaliyokubaliwa na jamii. Pia walitilia mkazo jinsi miili yao ilivyoumbwa kama wanaume na walipenda mambo ya vita.

Kwa upande wa kisaikologia, walitamani kuwa jasiri, dhabiti, wenye maono shupavu, wenye misimamo, wenye kumiliki na shujaa. Walitaka kuwa na uwezo wa kuwalinda wanyonge, kujihatarisha, n.k. vijana wa kike waliwachukulia wale wa kiume kuwa wajeuri, wanaotumia nguvu, wavumilivu katika shida, wanaojisimamia, wema, wapole, na walio na upendo kama wa baba. (Uchendu:2005). Hii ndiyo sababu uwezo kiume umeelezwa kuwa ni uume unaowafanya wavulana na wanaume waelewe vile watakavyofanya ili wakubaliwe kama waume, na wale watu wahuzishwe na mvuto wa wanawake, ushupavu, nguvu, mamlaka, ushindani, n.k (Frosh na wengine; 2002:77).

Nadharia hii ndiyo aliyotumia Walibora alipoandika vitabu vya watoto vifuatavyo: *Mtu wa mvua , Ndoto ya Amerika*, *na Mgomba Changaraweni*. Katika hadithi zote tatu, inajitokeza bayana kuwa utawala wa wanaume katika mambo yote unawafanya wanawake waonekane kama vyombo vya kutumiwa na wanaume (Althauser katika Janks na Ivanic; 1992: 308). Utafiti huu ulichunguza kama ni kweli kuwa mwanamume amepewa zile nafasi muhimu katika jamii na kutunzwa na kumfanya mwanamke aonekane kama kiumbe duni katika jamii ya wakikuyu.

Chacha (1997:8), katika tamthilia ya *Mke Mwenza* anatuonyesha mzee Chahe akitaka kumwoa mke wa pili kwa sababu yule wa kwanza ameshindwa kumzalia mtoto wa kiume. Kitheka (2004), katika tamthilia ya *Natala* anadokezea swala la kurithi bibi. Natala anapokataa kuridhiwa anatishwa kunyang'anywa mali yake yote na kufukuzwa kutoka kwake. Mwanamke anachukuliwa kama mali alirithiwe. Mwanachofi (2003:14) anatuonyesha kuwa dunia ni himaya ya wanamume anapoandika maneno ya mamaye Tenge, baada ya Tenge kupachikwa mimba na mwanamume akiwa shuleni na baadaye kutupiliwa mbali. Mama anamwambia bintiye :-

> *"Eee Tenge mwanangu, dhiki mke kuzaliwa*
> *katika ulimwengu, sisi hatukubaliwa*
> *kuepuka machungu! Ndo' yetu majaaliwa*
> *katika dunia ya wawi, dunia ya waume*."

Mugo (1982) anasema; "Mwanamume alipendelea kuoa mke mchanga katika uzee wake ili yule mke mwenye "damu moto" ya ujana amhudumie na kumsisimua mzee.

Katika kufanya hivi, mzee yule anakuwa anasisimka kila wakati na kuchangamka, na hivyo kuonekana mchanga kila uchao". Hii ni kuonyehsa kuwa wanawake waliumbwa ili wawastareheshe wanaume.

Ngugi (1975) ana kauli kuwa lugha hutumiwa kuendeleza taasubi ya kuwadunisha wanawake. Anasema lugha ni chombo kinachotumiwa kutoa taswira za mwanamke katika jamii. Ndungo (1985) ameangalia swala la mwanamke. Ameangalia mabadiliko ya mwanamke katika nyakati mbalimbali za kihistoria kulingana na mabadiliko katika mazingira yake. Picha ya mwanamke inayojitokeza ni ya kiumbe duni ambacho kimeshurutishwa na mifumo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kuchukua nafasi ya nyuma baada ya mwanamume.

Mello (1999) aliangalia majibu ya watoto kuhusu majukumu ya kimenke katika ngano zilizotambwa kimaongezi. Aligundua kuwa mashujaa wa kiume walipendelewa kwa ujasiri wao, nguvu na ushujaa ilhali mashujaa wa kike walipendwa kutokana na jukumu lao la ulezi na uvumilivu. Kulingana na Keller (1975:145), utafiti uliofanywa Marekani kuhusu majukumu ya kijinsia ulionyesha kuwa hii leo, wanawake zaidi wanajitokeza kufanya kazi za kuajiriwa na zile zilizodhaniwa kuwa za wanaume, ikilinganishwa na awali. Utafiti huo uligundua kuwa mnamo mwaka wa 1965, kati ya wanafunzi ishirini na watano waliojiunga na chuo cha sheria, mmoja tu ndiye alikuwa wa kike. Mwaka wa 1979, wakawa wanawake watatu kwa kila wanafunzi ishirini na watano. Kijumla ilonekana kuwa idadi ya wanawake wanaopata shahada za uzamifu inaongezeka kadiri miaka inavyoendelea. Mwanamke wa kisasa anapendelea kuwa na majukumu sawa na ya mwanamume.

Nchini Marekani kuna dai kuwa japo wanawake wengi zaidi wanaajiriwa katika sekta mbalimbali, kwingi wanafanya kazi ya kijungujiko ikilinganishwa na waume. Kazi nyingi za kifahari zinafanywa na wanaume. Jedwali lifuatalo linabainisha takwimu hizo.

Jedwali 1: Kielelezo cha uwepo wa wanawake katika kazi teule kufikia 1978.

Kazi	Asilimia ya wafanyakazi wa kike
1. Upigaji chapa na uhazili	98.6
2. Wauguzi	96.7
3. Walimu wa shule za msingi na upili	71.0
4. Wahadhiri wa vyuo vikuu	33.8
5. Madaktari	11.3
6. Majaji na mawakili	9.4
7. Uhandisi	2.8

Asili : Blum : 1991

Kulingana na Blum (1991) Margaret Mead alifanya utafiti wa majukumu ya kijinsia katika jamii ambazo hazijastaarabika wala kuathiriwa na usasa. Aligundua kuwa jamii ya Mudugumor, ambayo sasa inaitwa Biwat, wanawake hawakuwa na thamani. Wanaume na wavulana ndio waliopewa hadhi ya juu.

2.4 Maandishi Kuhusu Methali

Methali ni utanzu wa Fasihi Simulizi. Methali zimehifadhiwa katika maandishi, jambo ambalo ni tofauti na ilivyokuwa hapo zamani ambako zilihifadhiwa katika utamaduni wa jamii. Wafasili tofauti wametoa fasili tofauti kuhusu methali kutegemea lengo la mfasili na pia ule mkabala unaouchukua. Wamitila (2001) anaeleza; "Methali ni msemo unaojitosheleza, wenye maana yenye nguvu au uzito, wenye muundo au sifa za kishairi na unaokusudiwa kuadibu au kuelekeza, kuelimisha na kushauri". Ligami na Barasa katika Njogu na wengine (2006) wanaeleza kuwa "methali ni misemo inayotumiwa kueleza jambo kwa njia ya taswira na kwa ufupi ili kutoa maadili au onyo. Methali hudhimilisha maisha kwa kutumia tamathali, taswira na istiari. Kulinga na Finnegan (1970**),** methali ni lugha fiche iliyofumbwa, yenye mpigo, iliyofanyiwa uteuzi wa maneno wa hali ya juu. Saidi, katika Njogu (2006) anatujulisha kuwa methali ni semi zenye busara, zitoazo maadili mbalimbali katika maisha ya mwanadamu na hutumiwa kueleza kitu kwa njia ya picha na kwa ufupi ili itoe maadili au onyo fulani.

Kati ya tanzu zote za lugha,methali ndiyo tanzu inayotumika sana katika mazungumzo ya kawaida. Umuhimu wa methali katika mazungumzo haupuuziki kwa sababu methali hutumiwa na jamii nyingi ulimwenguni. Jamii ya wakikuyu hufahamu umuhimu wa methali na ndio sababu kuu ya wao kusema;
"*Ciunagwo rukomo, kimenyi akamenya ikiunwo*".
(Methali hutumiwa ili werevu waweze kung'amua yanayoendelea).

Munene (1995:48) anasema,"

> *"Thimo ni ndundiro cia kihoto ina ngarango nyingi thiini wacio na itari irathimurwo ndungihota kumenya ndeto cia cio. Thimo ni cia kuhoreria kana kuhe mundu irio cia meciria. Cii bata muno kuri mugikuyu tondu nicio igina cia kugereka ngerakano cia mugikuyu ndakae kwera maundu-ini make no arungiririe ta mugwi mugereke ni mwathi…* *maundu maria mekagwo ni mugikuyu ekaga atongoretio ni thimo ni getha athingate nuti ya ruriri rwa Agikuyu".*

Tafsiri: "Methali ni hazina ya ukweli yenye mambo mengi ndani yake na bila kufasiriwa hazieleweki. Methali hutumika kutuliza au kumpa mtu chakula cha fikra. Kwa mkikuyu, methali hutumika kama dira ya kumwelekeza ili asitetereke bali alenge ndipo kama mshale wa msasi**…** Mambo anayotenda mkikuyu huongozwa na methali ili kufuata mila za jamii ya wakikuyyu".

Jamii nyingi ulimwenguni hukubaliana na ukweli huu kuhusu methali. Mineke (1992) alitoa kauli zifuatazo kuhusu methali kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu.

1. Methali ni pambo la uzungumzi. Kauli hii yatoka kutoka kwa jamii ya nchi ya Iran.

2. Methali ni farasi wa Usemi. Maneno hayo yatoka katika nchi ya Nigeria, Jamii ya Yoruba.

3. Methali mia moja, ukweli mia moja. Madai haya ni ya wahispaniola.

4. Uzungumzi usio na methali ni kama chakula kisichokuwa na chumvi. Wanaoshikilia madai haya ni jamii ya Amharic kutoka nchi ya uhabeshi.

> Mbali na kuwa mirathi ya kitamaduni, methali huwa kama kitambulisho kwa wanajamii kama ilivyo lugha. Methali husaidia katika kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii. Ifahamike wazi kuwa utamaduni wa jamii huchangia falsafa ya jamii hii na mtazamo wake wa maisha. Methali huhusishwa na miktadha inazotumika na hudhihirisha kaida za amali za jamii husika. Wanaathropolojia hutoa kauli kuwa kujua methali za jamii huzika ni kujua jamii yenyewe (Mineke 1992).

Nketia, akizungumzia kuhusu methali katika jamii ya Akan katika Finnegan(1970:389 -390**)** anasema kuwa thamani ya methali miongoni mwa wanajamii haitokani na ufunuo wa mawazo ya zamani. Anagundua kuwa methali ni kielelezo cha lugha yenye nguvu zaidi. Finnegan 1970, akitafiti kuhusu Fasihi Simulizi miongoni mwa Waafrika aligundua kuwa methali huyapa uhalisia mawazo dhahania. Finnegan alishughulikia uwanda mpana wa Fasihi Simulizi. Utafiti huu ulishughulikia U.H.U mkabala wa Kihistoria, ukijikita katika methali kama matini. Nilijikita katika methali za jamii ya Wakikuyu.

Kipury (2002) anasema methali hutumika katika mawasiliano ya aina yote- hugusia juu ya tabia, ndani ya nyumba, kwenye hadhara ya watu, n.k. Anaendelea kusema kuwa methali huweza kuashiria kile kinachothaminiwa na jamii husika katika utamadani wao. Ndalu **(**1997) anasema methali au mithali ni kifungu cha maneneo, mara nyingi sentensi nzima, yatumiwayo pamoja kisanii, kwa njia ya kupigia mfano au kufumba na huchukua maana ndefu na pana kuliko maneno yaliyotumiwa. Madumulla (2005: 18) katika utafiti wake miongoni mwa Wahehe anaeleza kuwa methali ni sentensi za ukweli utokanao na ujuzi, sheria na tabia za jamii ambazo kwa kawaida hushauri hatua za kuchukua, au kupitisha uamuzi kuhusu kitendo fulani.

Kulingana na Rodgers (1981), methali zilianza kutumika kama miaka elfu kumi (10,000) iliyopita, hata igawa dai hili ni la kubahatisha tu kwa vile hakuna idhibati tosha iliyotolewa (Madumulla; 2005:20). Baadhi ya methali ni hojaji, nyingine ni ya dharau na kuna zilizo za kufanyia dhihaka, mfano, "Ana macho ya nje", hii ni tafsiri ya methali ya Kihehe isemayo, "*Munya miho mataali*", kumaanisha mwanamke anayeshiriki kitendo cha ndoa na wanaume wengi. Methali hii hairejelei mwanamume anayetembea na wanawake wengi. Katika utafiti wake, Madumulla anasema miongoni mwa wahehe, hakubahatika kukutana na watoto waliotumia methali. Watu wazima tu

ndio waliotumia methali katika usemi wao. Hii ni sawa na jamii ya wakikuyu. Watoto katika jamii ya wakikuyu walishiriki katika vitanza ndimi na vitendawili lakini sio methali. Hii ni kwa sababu kulingana na paremiolojia ya Waafrika, methali ni himaya au umiliki wa watu wazima. (Madumulla;2005:41). Ndulute anadhibitisha jambo hili anaposema methali katika jamii ya wahehe hutumiwa na watu wazima kwa sababu tofauti za usemi, pamoja na kutia adabu.

Okpewho (1992) aliziweka methali, vitendawili na vitanza ndimi katika kundi moja. Methali moja ya maneno mawili matatu hivi huenda ikawa muhtasari wa hadithi ndefu mno. Methali husema maneno mengi kwa kutumia maneno machache na kwa njia ya busara. (Madumulla;2005:42). Schipper (1991) anaeleza kuwa methali na misemo ni nukuu zinazotumiwa kumpa mzungumzaji utambulisho na imani. Taylor (1962) na Parker (1970) waliepuka kutoa maelezo ya methali wakidai kuwa ni vigumu kutosheleza fasili hiyo. Hivyo basi, utata wa methali katika utambulisho, fasili na umbo bado haujatatuliwa (Madumulla; 2005:25)

Akichunguza matumizi ya methali katika jamii ya Wahehe, Madumulla aligundua kuwa methali katika jamii hiyo hutokea kutoka kwa muktadha. Alichunguza methali zote za Wahehe huku akitathmini maana na matumizi yake. Alizigawa methali za Wahehe katika matapo arubaini na matano (45). Katika utafiti wangu, nilitathmini methali zinazohusu utambulisho wa mwanamume katika jamii ya Agikuyu. Nilizigawa methali zangu katika matapo matano (5).

2.5 Msingi wa Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya U.H.U mkabala wa kihistoria. Waasisi wakuu wa nadharia hii ni Ruth Wodak na Martin Reisigl (1999). Nadharia hii ilianza kutumika mwaka wa 2001. Nadharia hii ni Changa, na ni zao la nadharia ya U.H.U (CDA) ambayo iliasisiwa na Norman Fairclough. Kulingana na Wodak na Meyer (2001), nadharia ya Fairclough inahusika na uchanganuzi wa miundo ya lugha inayodhihirisha utawala, ubaguzi na uwezo miongoni mwa watumizi wa lugha. Harberman (177:259) anadai kuwa lugha hutumika kudhihirisha utawala na nguvu katika jamii. Nguzo tatu muhimu za U.H.U ni uwezo, uhakiki na itikadi (Wodak na Meyer 2001).

Lengo kuu la Wodak kuanzisha nadharia hii lilikuwa kuchanganulia matumizi ya lugha miongoni mwa watu weusi wanaoishi pamoja na wazungu. Nia yake ilikuwa ni kupambanua iwapo kuna vipengele vya lugha vinavyoakisi ubaguzi. Mkabala huu wa kihistoria ulitokana na haja ya kuchunguza mielekeo ya kibaguzi iliyojitokeza katika kampeni za uraisi za Austria mwaka wa 1986. Wodak, akishirikiana na wengine walipiga kambi katika mji wa Kurt Waldheini, Astria. Walichunguza midahalo ya kisiasa, kupitia matumizi ya lugha katika miktadha ya kijamii, wakagundua jinsi ubaguzi unavyojitokeza.Walichunguza matumizi ya lugha katika miktadha ya kijamii kwa kuangalia vile inavyotumika katika utangazaji wa habari katika runinga na pia katika ripoti za magazeti. Kwa upande wa pili, walichunguza matumizi ya lugha katika mikutano ya kampeni. Matokeo ya uchunguzi wao yalionyesha matumizi ya aina tofauti za leksia katika midahalo na katika matini zinazoendeleza viwango tofauti vya ubaguzi, ukiwemo ubaguzi wa rangi, wa kitaifa na wa kikabila.

Nchini Romania, U.H.U mkabala wa kihistoria ulitumika kuchunguza ubaguzi wa rangi miongoni mwa wahamiaji. Sajili tofauti zilitumika kama matini, kama vile mazungumzo ya kawaida, lugha ya siasa na matamshi mbalimbali. Matokeo yalionyesha matumizi ya lugha ya ubaguzi wa rangi. Tafiti hizi ziliwezesha kupambanua sababu za kuwepo kwa tofauti za matumizi ya lugha hasa yanayoonyesha usawa na utofauti (Wodak. 2001: 72). Wodak aliitumia nadharia hii kuchanganulia matumizi ya lugha miongoni mwa watu weusi walioishi pamoja na wazungu, kuwa madhumuni ya kutambua na kupambanua vipengele vya lugha vinavyoakisi ubaguzi, hasa wa rangi, kikabila na kitaifa.

Utafiti huu ulinuia kuchunguza iwapo kuna usawiri wowote wa kibaguzi wa kijinsia kutokana na matumizi ya lugha katika methali teule za jamii ya Agikuyu. U.H.U mkabala wa kihistoria ikawa ndiyo nadharia mwafaka itakayokidhi majukumu ya utafiti huu.Wodak (2001:73) anasema nadharia hii ina mikakati mitano ya usemi.

2.5.1 Mkakati wa Urejelezi.

Huu ni urejelezi wa wahusika katika matini. Kilichoangaliwa hapa ni majina waliyopewa wahusika iwapo kuna dhana yoyote ya ubaguzi wa kimaumbile, kihadhi, kikabila au kirangi. Swali kuu tunalojiuliza hapa ni, wahusika wamepewa majina gani na yana maana gani? Na sifa gani zinazoambatanishwa na majina haya, na

wanarejelewa vipi kiisimu. Mkakati huu pia humchunguza mhusika kama mwanajamii. Ikiwa jina lake lina maana hasi, huenda anayerejelewa si yeye binafsi, bali ametumiwa tu kama kiwakilishi cha kundi analotoka, au jamii. Mtafiti aliutumia urejelezi kuangalia jinsi wanaume wanavyotambuliwa katika jamii ya Agikuyu kupitia kwa methali.

2.5.2 Mkakati wa Nomino.

Kuna uwiano mkubwa kati ya mkakati huu na ule wa urejelezi. Wodak (2001:54) anapendekeza kuchunguzwa kwa mielekeo inayoambatanishwa na wahusika, sifa chanya na hasi za lugha zinazotumiwa kuwaakisi wahusika. Je, kuna sifa au vipengele vya kitabia vinavyoambatanishwa nao, vinavyochangia katika uhasi au uchanya wa usawiri wao? Mkakati huu pia huangalia sifa maalum bainishi, bainifu, pambanuzi na tabia zinazohusishwa na wahusika. Mkakati huu huonyesha maana inayoambatanishwa na urejelezi fulani. Pia, maana halisi ya neno inalinganishwa na maana rejelezi hivyo basi kupambanua ubaguzi.Vipengele vya lugha kama ishara na tashibihi vinatumika katika kurejelea aina tofauti za ubaguzi.

2.5.3 Mkakati wa Ubishi.

Mkakati huu unahusika hasa na kufafanua ubaguzi unavyodhihirika katika matini teule. Swali ni, je, ni kupitia mbinu gani za mabishano ambapo watu maalum au makundi ya kijamii, hujaribu kudhibitisha na kuhalalisha ubaguzi, na kutetea unyanyasaji kwa wenzao? Mkakati huu unafafanua sababu za kuwepo kwa ubaguzi na usawiri. Mkakati huu unaelezea jinsi ubaguzi umejitokeza katika matini teule. Mkakati huu utamsaidia mtafiti kudondoa vipengele mahsusi vya lugha vitakavyothibitisha uwepo wa ubaguzi. Vipengele kama vile sentensi, nomino, virai na vishazi vinavyoakisi utambulisho wa mwanamume katika methali za jamii ya Agikuyu. Topoi mbalimbali kutoka kwenye matini zitatumika kama ushahidi wa ubaguzi.

2.5.4 Mkakati wa Mkabala

Katika kufafanua mkakati huu, swali la kujiuliza ni hili; ni katika mkabala upi ambapo urejelezi, upachikaji wa majina na mabishano unaoegemea katika kusawiri ubaguzi? Maelezo, ufafanuzi, utoaji wa idhibati za ubaguzi ndipo yanapofikia kilele. Mkakati huu hujadili vitendo au uneni unaoonyesha ubaguzi. Katika utafiti huu, mtafiti

alidondoa vipengele vinavyotofautisha majukumu ya wake na waume. Hapa mtafiti alibainisha utambulisho wa mwanamume katika methali za Kikikuyu.

2.5.5 Mkakati wa Kufifiza

Mkakati huu huchunguza kama matamko haya ya ubaguzi yalitolewa kimaksudi au kisadfa tu, (Wodak: 2001:73). Uakisi huu ulikusudiwa au uliotokea bila kutarajiwa? Jamabo hili mtafiti afaa kulitafiti kutokana na lugha ambayo wahusika walitumia katika methali. Tabia za wahusika, matamshi na maumbo yao yanajenga vipi wanavyosawiriwa? Nadharia ya U.H.U. mkabala wa kihistoria ya Wodak (2001), ndiyo iliyoteuliwa kuwa dira mwafaka ya kuongoza utafiti huu. Sababu kuu ya kuichagua nadharia hii ni kuwa inasisitiza uwezo na mamlaka ya lugha. Fairclough na Wodak (1997) walisema kuwa lugha ni tendo la kijamii. walichosisitiza ni umuhimu wa muktadha wa matumizi ya lugha. Usemi huongozwa na tofauti za kimajukumu ambazo ni sehemu ya jamii. Usemi na utambulisho wa wahusika kutoka kwa methali za Agikuyu zilizoteuliwa ulichunguzwa ili kuonyesha majukumu ya kimenke.

Jedwali 2: Kielelezo cha Mikakati Inayoelezea Nadharia ya U.H.U Mkabala wa Kihistoria

Mkakati	**Swali**
1. Urejelezi	Watu hupewa majina yapi na vipi, na hurejelewaje Kiisimu?
2. Nomino	Ni sifa gani au vipengele vya kitabia vilivyoambatanishwa na wahusika, sifa chanya au hasi?
3. Ubishi	Ni kwa njia ipi ya ubishi, na utaratibu upi wa mabishano ambao watu bayana hujaribu kudhibitisha na kuhalalisha ubaguzi, ukandamizaji na unyonyaji wa wenzao?
4. Mkabala	Upachikaji majina, Uhusisho na ubishano huelezwa vipi?
5. Ufifizaji	Matamshi yenyewe hutamkwa kimaksudi au kisadfa? Huwa matamshi hayo yameongezwa au yamepunguzwa makali?

2.5.6 Sifa Muhimu za Mkabala wa Kihistoria

i) Mkabala huu huhusisha nyanja nyingi.

ii) Nyanja hizi huwa katika viwango kama vile nadharia, kazi yenyewe, vikundi na katika mazoezi.

iii) Mkabala wenyewe haujikiti katika dhana fulani ya kiisimu bali ni wa kusuluhisha matatizo yaliyomo.

iv) Nadharia na utaratibu zimefungamana, jambo ambalo husaidia kuelewa na kuelezea kuhusu lile linalochunguzwa.

v) Uchunguzi hushirikisha kazi za nyanjani na ethnografia kutalii kinachochunguzwa.

vi) Mkabala wenyewe ni nyakuzi, kurejelea kwake nyuma na mbele katika nadharia na data jarabati ni muhimu.

vii) Sanaa nyingi na nafasi nyingi za umma huchunguzwa na uhusiano wa mwingilianomatini na mwingilianomazungumzo pia huchunguzwa.

Marejeleo ya kimuktadha ni mfanyiko muhimu katika kuunganisha sanaa, mada na madahili.

viii) Muktadha wa kihistoria kawaida huchanganuliwa na kuunganishwa katika ufasili wa usemi na matini.

ix) Kategoria na vyombo vya uchunguzi huainishwa kulingana na hatua hizo zote na utaratibu, na pia kutegemea swala linalochunguzwa.

x) Nadharia kuu hutumika kama msingi. Katika uchanganuzi maalumu, nadharia za kati hutimiza malengo ya uchanganuzi vyema.

xi) Lengo huwa ni mazoezi. Matokeo yapewe wataalam katika nyanja mbalimbali, na hatua ya pili itumike kwa njia ya kubadilisha mazungungumzo na mazoezi ya kijamii.

Katika usemi wa ubaguzi, utafiti huu utaongozwa na maswali matano (5) yafuatayo:

i). Watu hupewa majina vipi na hurejelewa vipi kiisimu?

ii). Ni sifa gani, tabia, ubora na sura zinazohusishwa na watu?

iii). Ni kwa njia ipi ya ubishi, na utaratibu upi wa mabishano ambao watu bayana, ama makundi ya kijamii hujaribu kudhibitisha na kuhalalisha utengaji, ubaguzi, ukandamizaji na unyonyaji wa wengi?

iv). Utambulisho, uhusisho na ubishano huelezwa vipi?

v). Matamshi yenyewe hutamkwa au huelezewa hadharani? Matamshi hayo huwa yameongezwa au yamepunguzwa? (wodak na wengine; 1999 :72-73).

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ameelezea kwa undani hatua alizofuata na mbinu alizotumia kukusanya data yake. Sehemu hii imegawanywa katika sehemu tatu muhimu – kwanza ni mbinu za utafiti, pili ni uteuzi wa sampuli na tatu ni uchanganuzi wa data.

3.2 Mbinu za Utafiti

Mbinu ya utafiti iliyotumika ni uchanganuzi wa matini. Hii ni mbinu ya kutafuta ufahamu kwa kutambuliwa sifa bainifu za matini mbalimbali. Utafiti wa kimaktaba ulifanyika ili kupekua vitabu, majarida na tasnifu mbalimbali zilizogusia methali. Pia upekuzi huu ulikuwa na lengo la kupata yaliyoandikwa kuhusiana na nadharia iliyoongoza utafiti huu. Udurusu wa utambulisho wa mwanamume na kuhusu majukumu ya kimenke pia ulifanywa. Utafiti wa kimaktaba ulifanywa katika maktaba ya chuo kikuu cha Egerton, maktaba za umma za mjini Nakuru na Naivasha. Mtandao wa tovuti pia ulisaidia kupata data muhimu kuhusu historia na utamaduni wa jamii ya Agikuyu, lugha na jinsia. Utafiti wa Nyanjani ulifanywa ili kupata ufafanuzi zaidi kuhusu methali zinazomtambulisha mwanamume kwa njia moja au nyingine. Utafiti wa nyanjani ulikusudia kifidia ule wa maktabani. Njia hii ilitumika kutokana na ufaafu wake katika kutimiza lengo kuu la utafiti huu.

3.3 Mahali pa Utafiti

Mtafiti alijikita nyanjani kwa sababu data iliyotarajiwa kufanikisha utafiti huu ilipatikana nyanjani. Mtafiti alisafiri hadi kaunti ya Nyandarua katika kata ndogo la Kanyagia. Mtafiti alipiga kambi kwa muda wa mwezi mmoja. Aliwahoji wasailiwa kumi na wawili wa rika la Mwangi na Irungu. Kulingana na Kenyatta (1938: 130), marika haya mawili ya Mwangi na Maina ni baadhi ya marika yaliyokuwa maarufu sana katika jamii ya Agikuyu.

Mtafiti pia aliingia maktabani ambako alisoma vitabu, tasnifu na majarida yaliyokuwa na maelezo kuhusu mada aliyokuwa akishughulikia. Maktaba ya chuo kikuu cha Egerton, maktaba za umma za Nakuru na Naivasha zilikuwa za msaada mkubwa

katika utafiti huu kwa sababu zilikuwa na matini mwafaka iliyokidhi na iliyotosheleza mahitaji ya utafiti huu.

3.4 Uteuzi wa Sampuli.

Uteuzi wa sampuli ulikuwa muhimu sana katika utafiti huu. Hii ni kwa sababu jamii ya Agikuyu ina methali chungu nzima zinazomtambulisha mwanamume kwa njia moja au nyingine. Haingewezekana kuzichanganua methali hizi zote kwa sababu ya uhaba wa muda. Uteuzi wa sampuli ulitumia hatua zinafuatazo. Hatua ya kwanza ilikuwa kusikusanya methali zote za jamii ya Agikuyu zinazomtambulisha mwanamume kwa njia moja au nyingine. Methali zilikusanywa katika lugha ya asili ya jamii ya Agikuyu. Hatua ya pili ilikuwa ni kutumia sampuli azimwa kuchagua ni methali zipi zilizofaa zaidi. Methali arubaini na tano(45) zilichanguliwa kuwa zinafaa zaidi .

Hatua ya tatu ilikuwa ni kuziweka methali hizo katika matapo matano ambayo ni methali zinazomtambulisha mwanamume kisiasa, kiuchumi, kimaumbile, kijamii na kisaikolojia. Hatua ya nne ilikuwa ni kutafsiri methali hizo kutoka lugha ya kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili. Methali hizo arubaini na tano ndizo mtafiti alionelea zitatosheleza kupata data kamili ya kufanikisha utafiti huu. Wasailiwa walioteuliwa walikuwa kumi na wawili. Idadi hii iliafikiwa kwa sababu kama asemavyo Milroy (1987:84), kundi ndogo la sampuli humwezesha mtafiti kupata habari za kina kuhusiana na mada yake.

Uteuzi wa sampuli uliongozwa na madhumuni ya utafiti ambayo ni kudhihirisha jinsi Wakikuyu walivyomtambulisha mwanamume kupitia methali, kubainisha majukumu ya kimenke na kutathmini mahusiano kwa mujibu wa uana katika jamii ya Wakikuyu.

Pale nyanjani, niliwahoji wasailiwa kumi na wawili. . Wazee wa rika la Maina na Irungu ndio waliolengwa. (Kwa mujibu wa Muriuki katika Ogot 1983:126), haya ni marika kongwe katika jamii ya Wakikuyu, wenye umri wa miaka kati ya 70-80, na waliopashwa tohara kabla ya 1952. Wake kwa waume walisailiwa bila kuzingatia kiwango cha elimu.

Kupitia kwa mbinu hii, nilitarajia kupata data kuhusu:-

a) Historia ya wakikuyu
b) Methali zinazohusu wanaume.
c) Maoni juu ya maana za methali
d) Maana juu ya utambulisho wa mwanamume katika methali.

Kuhusu historia na utamaduni wa Wakikuyu, niliamua kuchunguza kwa undani utamaduni ambao unahusu utafiti wangu. Hapa mtafiti alichunguza vipengele vya utamaduni wa Wakikuyu ambavyo vinamtambulisha mwanamume kwa njia moja au nyingine. Vipengele hivi ni kama vile:

i). Kuzaliwa – Mtafiti alichunguza jinsi mtoto wa kiume alivyoshangiliwa baada ya kuzaliwa na ada zote alizofanyiwa akilinganishwa na mtoto wa kike. Hii ilimsaidia mtafiti kugundua kama ubaguzi wa kijinsia ulianza mara tu mtoto alipozaliwa, au ulionekana kujitokeza baadaye mtoto alivyoendelea kukua.
ii). Ulezi – Mtafiti alichunguza kwa undani kipengele hiki cha ulezi ili kubainisha jinsi mtoto alivyolelewa. Mtafiti alifahamu kuwa ulezi wa mtoto wa kiume ulikuwa tofauti na ule wa mtoto wa kike. Hapa mtafiti alijizatiti kuyafahamu majukumu yaliyotunukiwa mtoto wa kiume na yale ya mtoto wa kike.
iii). Upashaji tohara – Katika kipengele hiki mtafiti aliazimia kujua jinsi upashaji tohara ulivyotekelezwa, na baadhi ya mambo yaliyotiliwa umuhimu zaidi. Mtafiti ailiyafahamu majukumu anayotunukiwa mtoto wa kiume baada ya tohara na yale anayotunukiwa mtoto wa kike.
iv). Kuoa/kuolewa – Mtafiti alidadisi jinsi mwanamume alivyoshughulikiwa wakati wa kuoa. Kuna yale mwanamume alitakikana atimize na yaliyotimizwa na jamii. Msichana pia kuna jinsi alivyoshughulikiwa na aliyotarajiwa kutimiza.
v). Mazishi – Baada ya mwanamume kufariki jamii ilichukulia vipi tukio hilo? Mwanamume alizikwa wapi na alizikwa vipi? Je, mwanamke naye akitupa mkono wa buriani, yapi yaliyotendeka?

3.5 Vifaa vya Utafiti

Vitabu, majarida, tasnifu na mtandao ni baadhi ya vifaa vilivyotumika katika utafiti huu. Vifaa hivi vilikuwa na ujumbe uliosaidia kutimiza malengo ya utafiti wangu. Vifaa hivi vilimpa mtafiti matini tosha. Vifaa hivi vilipatikana maktabani. Nikiwa

nyanjani nilitumia kifaa cha kurekodi sauti. Kifaa hiki kilinisaidia wakati wa jioni nilipokuwa nimepumzika kwani niliweza kusikiliza tena mahojiano niliyokuwa nayo wakati wa mchana. Hii ilinisaidia kuupata ujumbe ule kwa njia bora zaidi kwa mara ya pili. Wasailiwa kumi na wawili ndio walikuwa chanzo muhimu cha data ya utafiti nyanjani.

3.6 Ukusanyaji data

Data ya utafiti huu ilijikita katika methali 45 zilizoteuliwa. Data iliyolengwa katika utafiti huu ilijumuisha mikakati mitano ya usemi, iliyoasisiwa na Wodak (2004). Mtafiti alipitia methali moja baada ya nyingine akizingatia jinsi mikakati hiyo mitano inavyojitokeza katika kila methali. Uchanganuzi wa kina ulifanywa na hapo ndipo mtafiti aliweza kudhihirisha kuwa mikakati mitano ya usemi ilijitokeza wazi katika methali zote 45. Hapo ndipo utafiti huu uliweza kutimiza malengo yake. Ilikuwa bayana jinsi mwanamume katika jamii ya Agikuyu anavyotambuliwa.

3.7 Uchanganuzi wa data

Data iliyokusanywa kutokana na upekuzi wa methali 45 ziliorodheshwa. Kisha data hiyo ilichanganuliwa kwa kiasi kikubwa kwa kuzingatia nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi, mkabala wa kihistoria. Mkabala huu wa kihistoria una mikakati mitano ya usemi ambayo ni urejelezi, nomino, ubishi, mkabala na ufifizaji. Mikakati hii ndiyo iliyosaidia kuchanganua methali teule 45. Mugenda na Mugenda (1999), wanasema kuwa katika utafiti wa kiuthamo, data huweza kuwa matini au picha ambazo huelezea matukio. Uchunguzi huu ulijikita katika matini ambapo methali zilichanganuliwa moja baada ya nyingine nikiongozwa na madhumuni ya utafiti.Mugenda na Mugenda (ibid) wanasema kuwa mara nyingi katika utafiti wa kiuthamano, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wake hufanywa kwa mwambatano wa moja kwa moja. Kwa kutilia maanani wazo hili, data iliyokusanywa ilipangwa katika viwango vitano mathalan methali za kiuchumi, kisiasa, kijamii, kimaumbile na kisaikolojia.

Kama hatua ya kuchunguza utambulishaji wa mwanamume katika zile methali kwenye yale makundi matano, mikakati ya usemi ndiyo iliyotumika kuchanganua methali hizo. Dira ya uchanganuzi huu ilikuwa ni madhumuni ya utafiti. Hata ingawa huu ni utafiti wa kiuthamano mbinu za uchanganuzi wa kiwigidadi zilihuzishwa kwa kiasi kidogo tu. Majedwali machache yalitumika. Kufikia mwisho wa uchanganuzi, utafiti ulikuwa

umelenga ndipo madhumuni yote matatu yaliyokusudiwa. Mbinu ya utafiti ilikuwa uchanganuzi wa matini. Dhana ya matini hapa imechukuliwa kwa msingi wa Schiffrin (1994) aliposema; "Nitalitumia neno matini ili kutofautisha dhana za kiisimu (kwa mfano, kile kinachosemwa katika usemi) na muktadha wa ule usemi..."

Matini yanaweza kuwa maandishi au matamshi. Katika utafiti huu matini ni maneno ya methali yaliyoandikwa na mtafiti. Matumizi ya lugha yalichunguzwa, iwapo yalidhihirisha majukumu kwa mujibu wa jinsia. Majukumu hayo na utambulisho ziliangaliwa kwa mikabala mitano; ya kijamii; kisiasa, kiuchumi, kimaumbile na kinafsia. Data iliyopatikana kutokana na uchanganuzi wa matin ilichanganuliwa kwa njia ya maelezo. Mtafiti alichukua hatua ya kwanza ya kuzitafsiri methali hizo ambazo zilikuwa katika lugha ya kikikuyu. Pia, data iliyopatikana nyanjani ilitafsiriwa kutoka lugha ya kikikuyu hadi lugha ya Kiswahili. Mtafiti alitumia tafsiri ya kimawasiliano (Tafsiri huru).

SURA YA NNE

UCHANGANUZI NA UFASILI WA DATA

4.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ameshughulikia mambo mawili; Kwanza methali zilitafsiriwa kutoka lugha chanzi hadi lugha ya Kiswahili. Pili, methali hizo zilichanganuliwa na kuwasilishwa kwa mujibu wa data iliyokusanywa.

4.2 Uchanganuzi wa data

Mtafiti alikusanya methalii arubaini na tano (45) kutoka kwa jamii ya Agikuyu. Data iliyokusanywa ni vipengele vya lugha vinavyoakisi utambulisho wa mwanamume katika mehali za Agikuyu. Data imechanganuliwa kwa njia tatu. Kwanza mtafiti amedhihirisha jinsi wakikuyu walivyomtambulisha mwanamume kupitia kwa methali, pili, amebainisha majukumu na nafasi ya mwanamume katika jamii, na mwisho, ametathmini na kubainisha mahusiano kwa mujibu wa uana katika jamii ya Wakikuyu.

Utafiti huu ulizingatia nadharia ya U.H.U. mkabala wa kihistoria, iliyoasisiwa na Wodak na Reisigl. Nadhara hii ni zao la U.U. Nadharia ya U.H.U mkabala wa kihistoria ilitumika katika utafiti huu kuchanganua utambulisho wa mwanamume katika methali za kikikuyu. Mtafiti pia alilenga kubainisha iwapo kuna vipengele vya lugha ilivyotumika kudhihirisha majukumu ya kimenke katika methali teule.

Ili kutimiza malengo hayo, methali zilikusanywa na kuchanganuliwa na mtafiti. Methali zilizokusanywa na kuchanganuliwa zinapatikana katika sehemu ya mwisho ya ripoti hii, kiambatisho cha tatu. Methali zote arubaini na tano zilichanganuliwa kwa kufuata utaratibu wa mikakati mitano ya usemi, ambayo ni, mkakati wa urejelezi, wa nomino, wa ubishi, wa mkabala na ule wa ufifizaji. Methali zote arubaini na tano ziliwekwa katika mikabala mitano kama ifuatayo:

4.2.1 Methali za mkabala wa kisiasa.

1) *Mari guoya mainukagira nyina, nao mari urume mainukagira ithe.*
   (Mwenye uwoga hurejelea mama zao, nao wenye ujasiri huwarejelea baba zao).
2) *Hari athuri hatitangagwo mai*

(Palipo na wazee usilete mzaha).

3) *Kahii kogi ta ithe kabaritaga ta migwi.*

(Mvulana mwerevu kama baba yake hujua kutumia mishale kama baba yake).

4) *Kahii ni ithigi ria mucii.*

(Mtoto mvulana ndiye ngao ya familia)

5) *Kahii ka mwathi kamenyaga kugereka.*

(Mtoto mvulana wa msasi hujua kulenga).

6) *Mbu ya arume itikagwo ni muthamaki*

(Mayowe/masiahi ya wanaume hujibiwa na mfalme)

7) *Maitho ma arume ti ma iranga*

(Macho ya wanaume huona mbali).

8) *Mwana mukuru na ithe ni hamwe.*

(Mtoto mvulana wa kwanza ni sawa na baba yake).

9) *Mwana ndahuragwo ithe ari ho.*

(Mtoto wa kiume hachapwi na mamaye baba akiwa karibu).

10) *Njamba ni ithaga ria rika.*

(Mwanaume hodari ni amana kwa rika lake).

11) *Ugi wa arume utemaga ta kahiu.*

*(*Werevu wa wanaume hukata kama kisu chenye makali*).*

12) *Wa kahii ti wa kairitu*

*(*Mtoto wa kiume si sawa na wa kike).

13) *Mundu wa muka umwe ni tuhu wa kanyenje.*

*(*Mwanamume wa bibi mmoja ni dubwasha).

Methali zilizo hapo juu zikiwa kumi na tatu zote ni za mkabala wa kisiasa; zinamrejelea mwanamume kwa misingi ya kisiasa. Mikakati ya usemi inajitokeza kama ifuatayo:-

4.2.1.1 Mkakati wa urejelezi

Katika methali ya kwanza, wanaume wamerejelewa kama "*mari"* yaani "wenye". Kiwakilishi "wenye" kinarejelea wanaume wote, waoga au hodari. Kiwakilishi hiki kimetumiwa kwa njia chanya kinapowarejelea wanaume walio na ujasiri.Vijana wanaume wenye ujasiri wanahusishwa na baba yao. Methali inatujulisha kuwa wao baada ya vita hurejelea nyumbani kwa baba zao. Vijana wanaume waoga

wanarejelewa kwa njia hasi, yaani "wenye uoga". Hawa wanasemekana kuwa kwa kuogopa vita, wao hurejea nyumbani kwa mama zao wala si kwa baba. Wenye uoga wanashirikishwa na mama, nao wenye ujasiri wanashirikishwa na baba. Sifa waliopewa wahusika hawa, yaani, "wenye uoga" na " wenye ujasiri" inarejelea kundi zima la vijana wanaume katika jamii. Vijana wanaume ndio walioshiriki katika vita. Jamii ilichukuliwa kuwa na ujasiri. Walioonyesha dalili za uoga, waliambiwa kuwa wao ni wa mama.

Katika methali ya pili, wanaume wamerejelewa kama "*Athuri",* yaani wazee. Hili ni neno la heshima sana katika jamii. Neno hili "*Athuri*" hurejelewa wakati wa kuwataja wazee walioheshimika. Neno hili linarejelea wanaume wote walioheshimika na limewarejelea kwa njia chanya. Wanaume ndio waliongoza jamii kisiasa na hivyo, methali inatahadharisha kuwa palipo na wazee, ulileteе mzaha. Palipo na wazee, mambo huwa mazima. Methali hii inashabihiana na ile ya Kiswahili inayosema, "*Palipo na wazee hapaharibiki neno".*

Methali ya tatu inarejelea mtoto mvulana kama "*kahii"*. Neno hili linamaanisha mtoto mvulana mdogo ambaye hajapashwa tohara. Mvulana huyu amerejelewa kwa njia chanya, huku werevu wake ukimithilishwa na ule wa baba yake. Mvulana huyu, aliyemwerevu kama babake, hujua kutumia mishale kama baba yake. Methali hii imetumiwa maneno kijazanda. Methali ina maana kuwa mvulana huyu hufuata nyayo za baba yake kwa kila hali. Mtoto hasa wa kiume anapokuwa mwerevu, jamii ya Wakikuyu huchukulia kuwa werevu huo umetokana na baba mzazi wala si mama.

Methali ya nne imetumia neno "*Kahii",* kama ile ya tatu. Urejeleo huu ni chanya. Methali ina maana kuwa mtoto wa kiume huwa ngao ya familia. Mtoto huyu ndiye atakayetwaa uongozi wa familia atakapokua, na pia atatoa ulinzi wa familia. Maelezo yake ni sawa na yale ya methali ya tatu. Methali ya tano ni sawa na ile ya tatu.

Methali ya sita inawarejelea wahusika kama "*Arume*". Jina hili lina maana ya "wanaume wenye ujasiri". Hapa, wanaume wanarejelewa kwa njia chanya. Jina hili "*arume"* limetumika kuwarejelea wanaume kuonyesha uwezo wao mkubwa na ujasiri walio nao. Methali inatuarifu ya kuwa ikiwa wanaume watapiga ukemi, basi atakayefika kuwashugulikia ni mfalme. Methali inaashiria kuwa haikuwa kawaida ya

wanaume kupiga mayowe, na ikiwa watafanya hivyo, basi kuna jambo lisilo la kawaida ambalo limetokea. Upigaji kamsa ni jambo linalohusishwa na wanawake sio wanaume. Hivyo basi, mayowe yakitoka kwa wanaume, huwa ni jambo lililokiuka kaida, ni hivyo litashughulikiwa kwa njia isiyo ya kawaida. Methali inaashiria kuwa ni kawaida kwa wanawake kupiga siahi. Methali hii inarejelea kundi lote la wanaume katika jamii ya wakikuyu.

Methali ya saba imewarejelea wanaume kwa njia chanya kwa kuwaita "*Arume*" inayomaanisha "wenye ujasiri". Methali inatuarifu kuwa macho ya wanaume yana uwezo wa kuona mbali. Methali hii imetumia maneno ya mafumbo yaliyofichika, ikiwa na maana kuwa wanaume wanauwezo kujua na kutabiri yale yatakayotokea baadaye. Wao huona mbali, huwaza kuhusu mambo ya leo, kesho na yatakayotokea baadaye- mustakabali.

Methali ya nane imetumia nene*"mwana*" yaani "mtoto". Mtoto hapa inarejelea mtoto wa kiume wala si wa kike. Jamii ya wakikuyu iliamini kuwa ndoa iliyobarikiwa na watoto wa kike pekee ilikuwa bado haijapata mtoto. Mtoto alichukuliwa kuwa yule wa kiume. Methali hii ilikuwa na maana kuwa yule mtoto wa kiume wa kwanza alikuwa sawa na babake. Hii ni kwa sababu baba atakapoaga dunia, jukumu la uongozi wa familia na umiliki wa mali huchukuliwwa na mtoto yule, wala si mama yake. Nomino hii "*mwana"*inawakilisha kundi zima la watoto wote wa kiume katika jamii. Watoto wa kiume wanarejelewa kwa njia chanya huku wakilinganishwa na baba zao. Hii ni kwa sababu uongozi na umiliki wa mali zilitwaliwa na watoto wa kiume. Wale wa kike hawakuridhi chochote na hawakuwa na haki ya kudai chochote.

Methali ya tisa inamrejelea mhusika kama "*Mwana*" yaani mtoto. Maelezo ni sawa na yaliyotolewa katika methali ya nane. Maana ya methali hii ni kuwa ilikuwa muhali kwa mama kumwadhibu mtoto wa kiume baba yake akiwa karibu. Ikiwa lazima amwadhibu, basi ilimbidi mama angoje mpaka bwana yake atakapoondoka kisha atekeleza ile adhabu kwa mwanawe. Pili, ilikuwa si kawaida kwa mama kupata nafasi ya kuingiliana na mtoto wa kiume kwa sababu mtoto anapotimiza umri wa kama miaka saba au minane, wakati wote wako pamoja na baba yake katika shughuli za uchungaji na usiku, wanaketi pamoja katika nyumba ya baba iliyoitwa "*Thingira*". Hivyo, haikuwa rahisi kwa mama kutangamana kwa urahisi na mtoto wa kiume.

Methali ya kumi inamrejelea mwanamume kwa njia chanya kwa nomino "*Njamba*", linalomaanisha "shujaa". Mwanamume amepewa sifa hii ya shujaa kwa sababu jamii inamuenzi sana mwanamume na humchukulia kuwa mtu mabruki. Methali ina maana kuwa mwanamume shujaa ni amana kwa rika lake. Mwanamume huyu huwaletea wanaume wa rika lake furaha na wote humwonea fahari. Pia, mwanamume huyu ni tuzo kwa jamii nzima. Hii ni kwa sababu atailinda jamii kwa ushujaa wake dhidi ya mahasidi wao. Kulingana na historia na itikadi za jamii ya wakikuyu, hakuna mwanamke aliyekuwa shujaa, ila mmoja tu kwa jina Wangu wa Makeri. Wangu alikuwa kiongozi wa jamii ya wakikuyu lakini, uongozi wake haukudumu. Wanaume walipanga mizengwe na kumng'oa Wangu mamlakani. Tangu hapo, hakujakuwa na mwanamke mwingine shujaa katika jamii ya wakikuyu.

Methali ya kumi na moja imewarejelea wanaume kama"*Arume*" yaani "wenye ushujaa na ujasiri". Huu ni urejelezi chanya. Methali ina maana kuwa wanaume wana werevu mwingi sana ambao hukata kama kisu chenye makali. Hivi ni kusema kuwa wanaume wana uwezo wa kutatua matatizo yote, hata yale yanayoonekana kuwa magumu. Hakuna linalomshinda mwanamume. Hii ndiyo sababu halmashauri zote katika jamii ya wakikuyu, zinazotoa mwongozo kwa jamii na kutatua matatizo ya jamii na kuamua kesi, huwa wahusika wote ni wanaume. Hapa tena tunaona wanaume wakihusishwa na werevu. Mwelekeo huu wa kuwaakisi wanaume kama werevu unaakisi jinsi jamii inavyomtambulisha mwanamume.

Methali ya kumi na mbili inarejelea watu wa jinsia zote mbili, "*wa kahii*," ikiwa na maana ya mtoto wa kiume, na *"wa kairitu*", ikiwa na maana ya mtoto wa kike. Watoto wote wawili wa kiume na kike wamerejelewa kwa njia chanya na majina waliyopewa pia ni chanya. Lakini maana ya methali inaakisi mwelekeo wa jamii kwa wanawake. Methali ina maana kuwa mtoto wa kiume si sawa na yule wa kike. Hapa maana ni kuwa yule wa kiume ni aula akilinganishwa na yule wa kike. Mtoto wa kike amedhilishwa. Hii ina maana kuwa ubora wa mwanamume dhidi ya mwanamke huanza pale wanapozaliwa. Hata zile ada anazofanyiwa mtoto wa kiume baada ya kuzaliwa ni tofauti na zile za mtoto wa kike. Mtoto wa kiume hukua na kujamiishwa huku akijua kuwa yeye ni bora kuliko yule wa kike, hivyo hujifaragua anapoendelea kupewa malezi.

Methali ya kumi na tatu inamrejelea mwanamume kwa njia ya kipekee. Hapa mwanamume amerejelea kwa njia chanya sana kwa kuitwa "*Mundu"* ikiwa na maana ya "binadamu" au "mtu". Naye mwanamke katika methali hii amerejelea kwa njia hasi na ya madharau kwa kuitwa "*Muka*." "*Muka"* ni jina la kudharau la kurejelea "bibi ya mtu" yaani mwanamke aliyeolewa. Mwnamke hapa amerejelewa kwa njia isiyo na heshima kamwe, huku mwanamume akirudikiwa heshima zote kwa kuitwa binadamu au mtu. Hii inaakisi mwelekeo wa jamii kwa mwanamume na kwa mwanamke. Methali ina maana kuwa mwanamume anayeoa bibi mmoja ni mwanamume ovyo na bure. Methali inawapa wanaume changamoto na kuwapa motisha wa kuoa bibi zaidi ya mmoja. Haki za wanawake hapa zinakiukwa. Jamii ina sababu nzuri za kutoa mwongozo huu.

Kwa muhktasari, methali hizo kumi na tatu za mkabala wa kisisasa zimeutoa mkakati wa urejelezi kwa kina. Tumeona jinsi wahusika walivyorejelewa katika methali na majina waliyopewa. Mtafiti amegundua kuwa baadhi ya majina waliyopewa wahusika yalirejelea kundi fulani katika jamii anamotoka. Mtafiti pia amegundua kuwa majina haya hayakutolewa kisadfa bali yalikusudiwa. Majina yote yanayorejelea wanaume yana sifa za kumpendelea mwanamume kwa njia chanya. Wanawake nao wamerejelewa kwa njia hasi, isiyo na heshima, na ya kuwadunisha. Mwanamke amekandamizwa kwa kupewa sifa mbaya.

4.2.1.2 Mkakati wa nomino

Mkakati wa nomino una uwiano mkubwa na ule wa urejelezi. Kulingana na Wodak (2001:54), mkakati wa nomino huchunguza mielekeo inayoambatanishwa na wahusika, sifa hasi au chanya za lugha kuwaakisi wahusika. Madhumuni makuu ya mkakati huu ni kuonyesha maana inayoambatanishwa na urejelezi fulani.

Katika methali ya kwanza, nomino "*Nyina*" imetumika ikiwa na maana ya "mama wa…". Pia nomino "*Ithe*" imetumika ikiwa na maana ya "baba wa"... Nomino hizo mbili zimetumika kuwarejelea wazazi wa kike na wa kiume. Nomino zimetumika kuwarejelea wazazi kwa njia chanya. Nomino hizi mbili hutumika katika jamii ya wakikuyu kuwarejelea wazazi kwa njia ya heshima. Badala ya kumwita mzazi kwa jina lake, anaitwa kwa kuambatanishwa na jina la mtoto wake, mfano:-

"*Nyina wa kamau* – mama Kamau

"*Nyina wa Wanjiku*- mama Wanjiku

"Ithe wa Kimani – baba Kimani

"*Ithe wa Njoki* – baba Njoki.

Ilikuwa marufuku katika jamii kumwita mwanamume aliyeoa au mwanamke aliyeolewa kwa jina. Ilibidi aitwa "baba wa…" Au "mama wa …". Hata ikiwa hawajabarikiwa na mtoto, majina yao yaliambatanishwa na jina la mtoto mtarajiwa. Uhasi unaopatikana katika methali ya kwanza ni kuwa uoga unaambatanishwa na mwanamke nao ujasiri unaakisi uanaume. Yule mtoto mwoga anasemekana ni wa mama na yule jasiri ni wa baba. Huu ni uonevu kwa mwanamke. Huu ndio uliokuwa mwelekeo wa jamii kwa wanawake.

Methali ya pili inawarejelea wahusika kama "*Athuri*", kumaanisha wazee. Nomino hii "*athuri*" ikiwa na maana ya wazee inarejelea kundi zima la wazee katika jamii. Nomino hii imetumika kuwarejelea wanaume kwa njia ya heshima sana. Katika jamii ya wakikuyu, nomino hii huwa na maana ya mtu ambaye ni mtulivu, anayechunguza mambo kwa undani na kwa makini, na aliye na uwezo wa kuyatenganisha mema na maovu. Nomino hii imetokana na kitenzi "*guthura*" inyomaanisha "kuchagua". Hii ina maana kuwa wana uwezo huo wa kuchagua, hivyo wanaweza kuwa waamuzi wema katika daawa. Methali inatoa ushauri kuwa palipo na wazee hapatakikani mzaha.Hii ni kwa sababu wazee huzungumzia yaliyo ya maana, na yenye manufaa kwa jamii nzima.

Methali ya tatu imetumia nomino mbili – "*Kahii*" ikiwa na maana ya mtoto wa kiume na "*Ithe"* ikiwa na maana ya "baba ya …", Nomino hii "*ithe*" mtafiti ameielezea katika methali ya kwanza. Nomino "*kahii*" (mtoto wa kiume) imetumika kumtaja mtoto wa kiume ambaye hajapashwa tohara. "*Kahii"* ni jina la heshima ambalo pia lilitumika kuashiria mvulana wa umri mdogo. Nomino hii inamsawiri mtoto wa kiume kama mtu mpole, anayetii na mnyenyekevu. Nomino hii inawakilisha kundi zima la wavulana wadogo katika jamii nzima ya wakikuyu. Nomino "*migwi*", ikiwa na maana ya mishale imetumika kijazanda kumaanisha shughuli za kila siku. Methali inatoa wazo kuwa mvulana mpole, mnyenyekevu na mtiifu huwa mwerevu kama baba yake, na huweza kutenda mambo yote kwa njia inayofaa kama baba yake. Hapa tunapata

taswira ya mwanamume kuwa kila wakati hutenda yaliyo mema na yanayokubalika na kuisaidia jamii.

Methali ya nne na ya tano zina maelezo sawa na ile ya tatu. Methali ya nne inatujuza ya kuwa mtoto wa kiume huwa kama ngao au mlinzi wa familia yao. Utamaduni wa mkikuyu ndio humjusurisha mtoto wa kiume na kumfanya kuwa shujaa na asiye na woga katika maisha. Kulingana na methali, familia ambyao haijafanikiwa na mtoto wa kiume huonekana kama isiyokamilika, isiyo na mlinzi au mtetezi. Nomino "*ithigi*" katika methali ya nne imetumika kumaanisha lango kuu. Kazi ya lango kuu katika boma huwa ni kuwafungia mahasidi nje wasije wakaivamia familia. Mtoto mvulana anamithilishwa na lango hilo katika jamii. Yeye ndiye anayetegemewa na jamii katika kutoa ulinzi na kuihakikishia jamii yake ulinzi.

Methali ya sita imetumiwa nomino " *Arume*," ikiwa na maana ya wanaume. Nomino "Arume" imetumika kwa njia ya kuwapa wanaume sifa ya kuwa na ujasiri. Methali inatupa taswira kuwa mwanamume amejusurishwa tangu utotoni na ndiyo sababu ya kuitwa "Arume" kumaanisha wenye ujasiri. Nomino nyingine iliyotumika katika methali hii ni , "*muthamaki*" kumaanisha kiongozi au anayetawala. Mtawala ni mtu aliyeheshimika katika jamii, hasa na wote walio chini ya himaya yake. Mtawala alichaguliwa kutokana na ujuzi wake au tajiriba yake. Mtawala au kiongozi anayo majukumu aliyotarajiwa kuyatekeleza kwa watu wa himaya yake. Majukumu haya ni pamoja na kutoa uamuzi wa mambo muhimu, kutoa ushauri kwa watu wake na kutoa mwongozo mwema kwa jumla. Methali hii inatuarifu kuwa iwapo wanaume wangepiga mayowe, mfalme ndiye angefika kuitika au kuwaletea msaada. Hili ni fumbo kuu ambalo linahitaji wenye hekima kulifumbua. Katika jamii, ilikuwa muhali kwa wanaume kupiga kamsa. Wanawake ndio waliojulikana kupiga mayowe wanapojikuta kwenye shida. Walipiga kamsa kuitisha msaada kutoka kwa wanaume. Ikiwa basi ilibidi mwanaume au wanaume wapige kamsa, basi jambo lisilo la kawaida huwa limetokea, na msaada ambao huwa wanaitisha sio kutoka kwa wanawake, bali ni kutoka kwa wanaume wenzao au kutoka kwa utawala wa juu wa himaya yao. Mwanamke alichukuliwa kuwa kiumbe duni ambaye hangetoa msaada wowote kwa mwanamume. Mwanamume ndiye angemuauni mwanamke wala sio mwanamke kumuauni mwanamume.

Methali ya saba imetumia nomino " *Arume"*, kumaanisha wanaume wenye ujasiri. Mtafiti ameelezea nomino kwa undani katika methali ya sita. Nomino hii imetumika kuwarejelea wanaume kwa njia chanya na kwa sifa ya kuwapendelea. Si kweli kuwa wanaume wote wa jamii ya wakikuyu ni wajasiri, lakini methali inatoa taswira kuwa wanaume wote ni jasiri. Methali inatujuza kuwa macho ya wanaume huona mbali, kumaanisha wanaume wana uwezo wa kujua yale yatakayotokea baadaye. Wao huwaza kuhusu leo na kesho. Wanawake kwa upande wao huchukuliwa kuwa hufikiria tu kuhusu yalioyoko sasa, na hawana uwezo wa kufikiria yatakayotokea kesho. Hii ni kumaanisha wanawake hujishughulisha na mambo madogo madogo nao wanaume hujishughulisha na yaliyo makubwa. Wanawake wananasibishwa na watoto wadogo nao wanaume hunasibishwa na watu wazima.

Methali ya nane inatujulisha kuwa mtoto wa kiume aliye wa kwanza huwa sawa na baba yake. Hii ni kwa sababu baada ya baba kuaga dunia, mtoto huyu, bila kuangalia umri wake, ndiye huchukua uongozi wa familia wala sio mama yake. Hii ni kwa sababu urithi na uongozi zote huchukuliwa na wanaume sio wanawake. Wanawake hawakurithi chochote na hawakuwa na haki ya kudai chochote. Nomino "*Mwana*", ikiwa na maana ya mtoto imetumika hapa kurejelea mtoto wa kiume sio wa kike. Ubaguzi mkubwa unajitokeza hapa ambapo nomino "*mwana*" (mtoto) ni kwa mtoto wa kiume tu. Yule wa kike hakurejelewa kama mtoto. Urejelezi huu wa mtoto wa kiume ni chanya na unaonyesha upendeleo kwa mtoto wa kiume. Bila kujali umri, huyu mtoto wa kwanza wa kiume ananasibishwa na baba yake. Nomino "*ithe*" imetumika kumaanisha "baba". Hii ni nomino ya heshima ya kumrejelea mzazi wa kiume. Nomino hii inaakisi kiongozi wa familia yake. Kulingana na jamii ya wakikuyu, mama hahusishwi kamwe katika uongozi wa jamii au familia. Mzazi wa kiume huifanya kazi ya uongozi akisaidiana na watoto wa kiume. Mama na watoto wa kike huchukuliwa kama baadhi ya mali pale nyumbani.

Methali ya tisa imetumia nomino "*Mwana"* yaani mtoto na nomino "*Ithe",* yaani "baba". Matumizi ya nomino hizi ni sawa na kama alivyoeleza mtafiti katika methali ya nane.Methali hii inatujuza kuwa mtoto wa kiume haadhibiwi na mama yake baba yake akiwa karibu. Ilikuwa muhali kwa mama kumwadhibu mtoto wa kiume mbele ya baba yake. Haikuwa rahisi mama kumpata huyu mtoto wa kiume kwa sababu anapofikisha umri wa miaka saba au minane, yeye huandamana na baba yake kwenda

machungani kila kuchao hadi machweo. Wakati wa usiku, yule mtoto huketi na baba yake katika "*Thingira"* ambako huendelea kupokea mafunzo kuhusu jamii yake na maisha kwa jumla kutoka kwa baba yake. Ilikuwa nadra sana kwa mama kupata nafasi ya kuwa na mtoto wake wa kiume. Watoto wa kike ndio walikuwa na mama yao kila wakati. Ikiwa ilibidi mama amwadhibu mtoto wa kiume, basi alingoja hadi atakapopata nafasi na ahakikishe baba hayuko karibu.

Methali ya kumi inatupa ujumbe kuwa mwanamume jasiri alikuwa amana kwa wanaume wa rika lake. Mwanamume barobaro aliyekuwa jasiri aliheshimiwa sana kutoka kwa Mungu. Wanaume wa rika lake walimwonea fahari na walijivunia kuhu sishwa naye. Mwanamume huyu ndiye aliyeongoza katika vita na aliwajusurisha wenzake. Chini ya uongozi wake, walishinda mahasidi wao. Aghalabu alichaguliwa kuwa kiongozi wa rika lake na baadaye kiongozi wa jamii nzima. Aliijasirisha jamii nzima wakati wote. Wavulana waliopashwa tohara waliwekwa katika kundi moja na wakapewa jina la rika hilo. Hata wasichana waliopashwa tohara wakati mmoja na wale wavulana walichukua jina la rika ya wavulana. Majina yaliyopewa marika yalikuwa kama vile:-

"*Rika ria mathathi*"- rika la mathathi"

"*Rika ria Ndemi*" – rika la Ndemi

"Rika ria Kamau" – rika la Kamau

"*Rika ria Maina*" – rika la Maina

"*Rika ria Mwangi*" – rika la Mwangi. (Murata; machi 1999)

Majina yote ya marika yalikuwa ya kiume. Hakuna rika lililopewa jina la kike. Hapa tunawaona wanawake wakibaguliwa. Nomino "*Njamba"* ikimaanisha " shujaa," imetumika kumrejelea mwanaume kwa njia chanya na ya kumtukuza na kumtwaza. Nomino hii imetumika kusimamia kundi zima la wanaume katika jamii ya wakikuyu. Wanaume wamerejelewa kama "*Njamba"* (Shujaa) kwa sababu wao ndio hushiriki katika vita. Wanawake hawakuhusika katika vita pamoja na watoto. Pia wakati wa vita wanawake na watoto hawakuuawa. Badala yake, jamii ya wakikuyu iliwateka wanawake, hasa wa kimaasai, na kuwapeleka kwao. Wamaasai ndio waliopigana sana na jamii ya wakikuyu. Jina "*Nyokabi*" ni la mwanamke, na asili yake ni wale wanawake waliotekwa kutoka kwa Wamaasai na kuletwa upande wa wakikuyu.

Pia, nomino hii "*Njamba*" ilitumika kuonyesha ushujaa na ujasiri wa mwanamume aliyetarajiwa kuwa ngao ya jamii kwa jumla. Usalama wa jamii ulitegemea wanaume. Wanaume walitarajiwa kukabiliana na hatari zozote zile, au janga lolote lile ambalo lingeikumba jamii. Wanawake hawangeitwa "*Njamba*" kwa namna yoyote ile. Walitakikana watosheke na kulindwa wala sio kulinda.

Methali ya kumi na moja inatoa hoja kuwa werevu wa wanaume hukata kama kisu. Methali hii ina maana kuwa wanaume wana uwezo wa kutatua hata yale matatizo yanayoonekana kuwa makubwa. Hakuna linalomshinda mwanamume, na litakalomshinda, atakuwa ameng'ang'ana nalo kabisa, ndiposa jamii ikawa na methali inayosema,

"*Kirema arume nikigariure*"

(Kinachowashinda wanaume huwa kimeshughulikiwa vilivyo).

Pia, methali inatoa wazo kuwa wanaume kwa hekima yao huweza kutoa uamuzi wa mambo yanayokubalika na kwa njia sahihi. Wanaume wana suluhu kwa kila tatizo. Nomino "kisu" imetumika katika methali kuelezea jinsi hekima ya wanaume inavyofanya kazi. Kisu ni kifaa kinachotumika nyumbani kwa njia mbalimbali, mfano; kuchinja, kukata nyama, kukata viazi na kazi nyingi za jikoni. Hii ina maanisha jinsi kisu kinavyotumiwa kutekeleza kazi nyingi, ndivyo mwanamume anavyotekeleza majukumu mengi, mazito na mepesi.

Methali ya kumi na mbili yatueleza kuwa mtoto wa kiume si sawa na yule wa kike. Mtoto wa kiume hujamiishwa akiwa na ufahamu kuwa yeye ni aula kuliko yule wa kike. Yule wa kike naye hukua akijua sehemu yake katika jamii. Mtoto wa kike hujua majukumu yake na haki zake. Haya yote anayapata katika ulezi wake kutoka kwa wale wanaomjamiisha.Nomino "*Kahii"* kumaanisha mtoto wa kiume na "*Kairitu*" ikimaanisha mtoto wa kike zimetumika kwa njia chanya na yenye upole ya kutaja mtoto wa kike na wa kiume. "*Kahii"*, ni jina la heshima la kumtaja mtoto mdogo wa kiume ambaye bado hajafikisha umri wa kupashwa tohara. Pia, nomino "Kairitu" ni jina la heshima la kumtaja mtoto wa kike mdogo ambaye pia hajafikisha umri wa kupashwa tohara. Nomino zote mbili, "*Kahii*" na "*Kairitu*" zimetumika kujumuisha wote walio katika rika hilo katika jamii. Dhana hii ya kuwa mtoto wa kiume ni bora zaidi kuliko yule wa kike inashikiliwa na jamii nyingi za kiafrika. Hata hivyo, dhana hii haina mashiko.

Methali ya kumi na tatu inatoa wazo kwamba mwanamume anayeoa bibi mmoja ni bure. Jamii iliamini kuwa mwanamume halisi huwa na bibi zaidi ya mmoja. Bwana kama huyu aliheshimiwa sana katika jamii, na hata ndiye aliyechaguliwa kuiongoza jamii. Kama mtafiti alivyoeleza hapo awali, jamii iliwapa wanaume motisha ya kuoa wake zaidi ya mmoja. Unominishaji katika methali hii unadhihirika kutokana na matumizi ya nomino zinazoakisi uchanya na uhasi wa wahusika. Kwanza, mwanamume amepewa jina la "*Mundu"* inayomaanisha binadamu. Huu ni ubaguzi kwa sababu kulingana na methali mwanamume ndiye binadamu, na mwanamke je, ataitwa aje? Mwanamume amerejelewa kwa njia chanya kwa kuitwa binadamu – jina la heshima la mtu – mwanamke naye amerejelewa kama "*muka*" – kumaanisha "bibi wa". Nomino hii "*muka*" ni jina lisilokuwa na heshima la kumrejelea mwanamke aliyeolewa. Hii ni njia moja ya kumdhalalisha mwanamke. Mwelekeo hasi wa jamii kwa mwanamke unadhihirika wazi. Methali inaendelea kuelezea kuwa mume wa bibi mmoja hana maana yoyote na anamithilishwa na mende. Mende ni mdudu anayejulikana kuishi katika mazingira duni na machafu. Mume aliyeoa bibi mmoja ndiye anayelandanishwa na mende – kuonyesha kuwa jamii inamchukulia bibi kama mali. Jisni mwanamme alivyo na wake wengi, ndivyo alivyyo na mali mengi na heshima kuu kutoka kwa jamii.

4.2.1.3 Mkakati wa Ubishi.

Mkakati huu huhusika hasa kufafanua ubaguzi unavyodhihirika katika matini teule. Mkakati huu ulimsaidia mtafiti kufafanua na kudhihirisha uwepo wa ubaguzi katika methali teule za wakikuyu. Mtafiti aliangalia jinsi ubaguzi ulivyodhihirika katika matini teule. Swali kuu ambalo mtafiti alizingatia ni, je, ni kupitia kwa mbinu gani za mabishano ambapo watu maalum au makundi ya jamii hujaribu kuhalalisha ubaguzi? Iwapo mhusika fulani wa kike au wa kiume anasawiriwa kwa njia fulani, anasawiriwa hivyo kibinafsi, au anawakilisha kundi la watu? Dhana ambazo hasina ukweli, yaani falasia, pia zilichunguzwa na mtafiti.

Katika methali ya kwanza, ubaguzi unajitokeza wazi pale ambapo wavulana wenye uoga wamehusishwa na mama zao, nao wale wenye ujasiri wanahusishwa na baba zao,. Hapa mwanamke anasawiriwa kama binadamu mwoga, naye mwanamume anasawiriwa kama jasiri. Ubaguzi huu unonyesha kuwa jamii ilimchukulia mwanamke

kama asiyejiweza na ambaye lazima kila wakati awe chini ya ulinzi wa mwanamume. Mwanamke hutegemea mwanamume katika hali ya usalam na uongozi.

Katika methali ya pili, ubaguzi pia unajitokeza pale tunapoarifiwa kuwa palipo na wazee hakuna mzaha. Kinyume chake ni kuwa mzaha hupatikana pale palipo na akina mama. Mambo yasiyo na maana huhusishwa na akina mama nao wazee huhusishwa na mambo yenye utu uzima. Huu ni ubaguzi a kimenke. Ubaguzi huu ndio unaomweka mwanamke chini ya utawala na uongozi wa mwanamume.

Methali ya tatu inaashiria ubaguzi pale inapotaja "*Kahii kogi ta ithe*.." Yaani mvulana mwerevu kama babaye. Hii ina maana kuwa baba ndiye mwerevu sio mama. Hapa ubwege umehusishwa na wanawake. Hii ni kumshushia mwanamke hadhi kabisa. Hapa baba ametumika kusimamia kundi zima la wanaume katika jamii ya wakikuyu. Hivyo ni kusema, wanaume wote ni werevu nao wanawake ni mabozi. Ubaguzi unadhihirika wazi hapa.

Methali ya nne pia inaashiria ubaguzi inapotoa kauli kuwa mtoto wa kiume ni ngao ya familia. Hapa kuna maana kuwa familia ambayo haina mtoto wa kiume haina ulinzi au usalama. Hapa mwanamke pia amesawiriwa kama kiumbe mwenye udhaifu. Mkakati wa ubishi haujajitokeza wazi katika methali ya tano. Mkakati huu wa ubishi umejitokeza kwa njia ya wazi katika methali ya sita. Methali inatoa kauli kuwa mayowe ya wanaume hujibiwa na mfalme. Hii ina maana kuwa mwanamume akipiga kamsa, atakayefika kumsaidia si mtu wa kawaida, bali aliye na cheo cha juu katika jamii. Huu ni ubaguzi unaomchukulia mwanamume kama kiumbe aliye na utukufu fulani, mwenye cheo cha juu katika jamii. Ukemi wa mwanamke unachukuliwa kama kitu cha kawaida tu, na atakayefika kumsaidia mwanamke ni mtu yeyote yule wa kawaida, awe mwanamke au mwanamume. Wanawake wameshushiwa hadhi sana. Mwanamke anapopiga kamsa, inachukuliwa kuwa jambo la kawaida na lisilokuwa na umuhimu wowote ule. Kwa kawaida, katika jamii ya Wakikuyu, wanaume hawakutarajiwa kupiga kamsa. Upigaji kamsa ilikuwa kawaida ya wanawake. Hivyo basi kama mwanamume au wanaume wangepiga kamsa, kulikuwa na maana kuwa jambo lisilo la kawaida limetokea na hivyo, hatua za dharura lazima zichukuliwe na kila mtu.

Ubaguzi unajitokea pia katika methali ya saba inayosema macho ya wanaume yana uwezo wa kuona mbali. Hapa mwanamume anapendelewa kwa kupewa sifa ya kwamba ana uwezo wa kuyatabiri yatakayotokea katika siku zijazo. Ubaguzi huu ni wa kumtwaza mwanamume na kumdhalilisha mwanamke. Mwanamume anapopewa sifa hii, anapata nafasi nzuri ya kumtawala na kumwongoza mwanamke.

Methali ya nane inatujuza kuwa mvulana wa kwanza katika familia ni sawa na baba yake. Ubaguzi unaojitokeza wazi ni kuwa methali inapomtaja "mtoto", inarejelea yule wa kiume wala si wa kike. Hivi ni kusema kuwa jamii ilimrejelea mtoto wa kiume kama "mwana" yaani mtoto. Mtoto wa kike hakuitwa mtoto. Ndoa iliyobarikiwwa na watoto wa kike tu ilisemekana kuwa bado hawajabarikiwa na mtoto ila wasichana tu. Mtoto wa kike aliitwa msichana. Huu ni ubaguzi wa kumpendelea mtoto wa kiume dhidi ya yule wa kike. Ubaguzi mwingine wa kijinsia ni pale yule mtoto anamithilishwa na babake wala si mamaye.

Tukumbuke kuwa baba ndiye kiongozi wa familia, aliye na uongozi na mamlaka yote. Huyu mtoto wa kiume amemithilishwa na baba yake kwa sababu endapo baba angefariki, yule mvulana, bila kujali umri, alitunukiwa uongozi na utawala wa familia ile na kurithi mali yote kutoka kwa baba yake. Mamaye hakurithi chochote kutoka kwa mwendazake. Mwanamke hapa anabaguliwa. Mwanamke, licha ya umri mkubwa, mbele ya macho ya jamii ni dhalili na kwa upande mwingine, mvulana licha ya kuwa wa umri mdogo, mbele ya macho ya jamii, ndiye aliye na busara na uwezo wa kuongoza jamii.

Methali ya tisa, ina ubaguzi kama ule ulioko katika methali ya nane. Ubaguzi huu ni wa kumwita mtoto wa kiume "*mwana*" yaani mtoto. Pia methali inatuarifu kuwa huyu mtoto hawezi kuadhibiwa na mama yake baba yake akiwa karibu. Hii ina maana kuwa mama hakuwa na haki ya kumwadhibu mtoto wa kiume hasa mbele ya baba yake. Huu ni ubaguzi. Jamii haikupinga mtoto wa kike kuadhibiwa ila yule wa kiume.

Methali ya kumi haikudhihirisha kwa njia ya wazi mkakati wa ubishi. Mkakati huu wa ubishi unadhihirika wazi katika methali ya kumi na moja inayotujuza kuwa werevu wa wanaume hukata kama kisu chenye makali, ikiwa na maana kuwa hakuna linalowashinda wanaume. Wanaume wana hekima na busara ya kuyatatua matatizo yote bila kushuhudia ugumu wowote. Ubaguzi unadhihirika wazi pale ambapo sifa

zote nzuri zinamiminiwa mwanamume. Huku ni kumpendelea mwanamume na kutoa wazo kuwa mwanamke hana hekima wala busara.Mwanamume anatwazwa huku mwanamke akitwezwa.

Mkakati wa ubishi unajitokeza wazi katika methali ya kumi na mbili.Methali inatujuza kuwa mtoto wa kiume si sawa kabisa na yule wa kike. Methali hii inaashiria kuwa mtoto wa kiume ni muhimu sana kuliko yule wa kike. Jamii ya Wakikuyu huongozwa na taasubi ya kuumeni, hivyo, mwanamume hupendelewa tangu kuzaliwa, kulelewa, kupashwa tohara, kuoa na hata wakati anapofariki (kama ilivyoelezwa katika 4.2). Ubaguzi wa kumpendelea mtoto wa kiume ulionekana wazi katika jamii ya wakikuyu. Hii ina maana kuwa mtoto wa kike na wa kiume walijamiishwa wakijua nafasi na majukumu watakayotekeleza ukubwani mwao.

Kusisitiza umuhimu wa mtoto wa kiume, ndoa ambayo haikubarikiwa na mtoto wa kiume ilionekana kama yenye laana na isiyokamilika. Mume alishawishiwa aoe mke mwingine atakayemzalia mtoto wa kiume ambaye angekuwa mriithi wa mali ya familia. Hii ni kwa sababu mama na watotot wa kike hawakuwa na haki ya kuriithi chochote baba anapofariki.

Methali ya kumi na tatu ina ubaguzi unaojitokeza kwa mbali. Methali inasema kuwa mwanamume aliyeoa mke mmoja ni bure. Methali inatoa wito wanaume waoe wake zaidi ya mmoja. Hapa, mwanamke anachukuliwa kama mali. Jinsi mwanamume alivyo na wake wengi, ndiyo alivyoonekana kuwa tajiri na aliheshimiwa katika jamii. Mwanamke anabaguliwa kwa sababu yeye hapewi nafasi ya kuamua kama mumewe ataoa wake wengine au la. Ni wazi kuwa mume aliyekuwa na wake wengi hakuwatosheleza wake wale haja zao za kimwili kindakindaki. Ilibidi wale wake wavumilia kwa sababu mila haikuwaruhusu kulalamika. Jamii ilimjali mwanamume tu, akitosheka na afurahie maisha, basi kila kitu kilionekan kuwa shwari. Starehe na furaha ya mwanamke haikutiliwa maanani.

4.2.1.4 Mkakati wa Mkabala

Mtafiti alitumia mkakati wa mkabala kuangalia ni kwa mkabala upi ambapo urejelezi, upachikaji wa majina au mabishano ulizingatiwa katika kusawiri ubaguzi wa kimenke katika methali za wakikuyu. Katika methali ya kwanza, mkabala uliochukuliwa ni wa kumsawiri mwanamume kama nguli au shujaa naye mwanamke anasawiriwa kama

mwoga. Methali inatujuza kuwa wavulana wanaoshiriki vitani, walio na ujasiri huwarejelea baba zao baada ya vita, nao waoga huwarejelea mama zao baada ya vita. Hapa ni wazi kuwa wanaume wamesawiri kama mashujaa wenye ujasiri nao wanawake wanasawiriwa kama waoga. Wanaume ni mihimili ya wanawake ambao wanachukuliwa kuwa hawawezi kujisimamia. Mwanamume aliye na uoga anamithilishwa na wanawake. Jamii inaamini kuwa wanaume wanatarajiwa kuwa wenye ujasiri na ndio wanaotoa ulinzi wa jamii nzima. Usalama wa jamii dhidi ya uvamizi wowote husimamiwa na wanaume. Kwa jamii yoyote ile inayongozwa na taasubi ya kiume, mwanamume hatarajiwi kuwa mwoga, na hata wale wanaume waoga, hawaruhusiwi kuonyesha dalili za uoga. Wanawake wamesawiri kuwa waoga, viumbe duni, ambao wako chini ya uongozi na mamlaka ya mwanamume. Tayari wamechukua nafasi ya pili baada ya mwanamume.

Methali ya pili inatuarifu kuwa palipo na wazee hapatakikani mzaha. Methali hii imechukua mkabala wa kuumeni. Mkabala huu unaonyesha kuwa wanaume wako juu sana, hivi kwamba palipo na wazee, hapatakikana mzaha. Kinyume chake ni kuwa mzaha hupatikana pale palipo na wanawake. Jamii imemweka mwanamume kuwa mbele sana akilinganishwa na mwanamke. Hii ndiyo sababu, mhusika mmoja kwa jina Khazija, katika riwaya ya utengano anawachukia wanaume, nukuu inasema;-

> "*Kuna mengi ambayo Khazija anayachukuia. Ndiyo anachukia… kwanza anachukia mwanamume. Mwanamume anamchukia kwa sababu dhahiri, nayo ni kuwa amewekwa mbele, ingawa Khazija hajui na nani. Daima atamchukia mwanamume kwa sababau hiyo."* (Mohamed 1980:1).

Utamaduni wa Mkikuyu umemtwaza mwanamume na kumtweza mwanamke. Kisiasa, mwanamume ako juu ya mwanamke. Utawala na uongozi umepewa wanaume. Mwanamke kazi yake ni kutawaliwa. Watawala huwa hawana mzaha. Mambo yao hutendwa kiungwana bila mzaha .Methali ya Kiswahili inayotia nguvu methali hii ya kikikuyu ni inayosema palipo na wazee hapaharibiki neno.

Methali ya tatu inachukua mkabala wa kumsawiri mwanamume kama kiumbe mwerevu. Methali inaarifu kuwa mvulana mwerevu kama baba yake hujua kutenda mambo yote kama inavyotakikana. Mwanamume hapa amepewa sifa ya werevu. Werevu huu wa mwanamume ndio unaomfanya awe kiongozi wa jamii, anayeamua

mambo yote ya familia yake. Wanawake wameachiwa majukumu yale duni, yanayowafanya kila wakati wawe nyumbani. Methali hii inatoa wazo kuwa akina mama huwa si werevu na pia watoto wasichana pia si werevu. Dhana hii ni falasia na ni potovu ya kuwadhalilisha wanawake.Utamaduni wa mkikuyu humchukulia mtoto mvulana na baba kuwa sawa. Ingawa mama na baba huwa katika nafasi sawa katika ulezi wa watoto wao, kimamlaka, mama hana nafasi kamwe. Watoto wa kiume ndio hupewa nafasi sawa na baba yao. Mama na watoto wasichana huwekwa katika kundi moja la kutawaliwa.

Mkakati wa mkabala haujajitokeza kwa njia ya moja kwa moja katika methali ya nne na ya tano. Katika methali ya sita, mkabala uliochukuliwa ni wa kumsawiri mwanamume kama shujaa, ambaye kila wakati anatenda matendo ya kishujaa na si rahisi kwake kuitisha msaada. Methali inatoa wazo kwamba ni vigumu kwa mwanamume kupiga kamsa kuitisha msaada. Iwapo mwanamume angepiga kamsa, ilikuwa na maana kuwa jambo lisilo la kawaida limetokea, na hivyo, angepata msaada sio kutoka kwa wanawake bali kutoka kwa watu wa ngazi ya juu kihadhi. Ilikuwa nadra sana kwa wanaume kupiga kamsa. Hii ni kwa sababu mwanamume alitarajiwa kuvumilia hata yale mazito au ya uchungu. Mwanamume hapa amepewa taswira ya kiumbe mkakamavu ambaye kwanza angepambana kufa kupona na lolote lile ambalo lingetokea, na angeitisha msaada iwapo angeona maji yamezidi unga. Methali hii inatuchorea taswira ya ubinafsi na ubaguzi pale ambapo msaada kwa wanaume haungetoka kwa akina yakhe, bali ungetoka kwa watu wenye cheo na wa hadhi ya juu kimaisha au kiuchumi. Utamaduni wa mkikuyu unamweka mwanamume juu kila wakati, huku mwanamke akichukua nafasi ya pili.

Methali ya saba inachukua mkabala wa kuumeni, ambao husisitiza ubora wa mwanamume akilinganishwa na mwanamke. Methali inatujuza kuwa wanaume wana uwezo wa kuona mbali, yaani kuyatabiri yatakayotokea siku za usoni. Mwanamume anapendelewa na kupewa sifa hadi kuonekana kama asiye binadamu wa kawaida, huku mwanamke akidhalilishwa.Dhana hii ni falasia kwa sababu sio wanaume wote walio na uwezo huu. Methali hii inachukulia kundi lote la wanaume katika jamii wana uwezo huu.

Methali ya nane pia inachukua mkabala wa kuumeni. Methali inatuarifu ya kuwa mtoto wa kiume, aliye mkubwa kuliko wale wengine ni sawa na babake. Methali hii imetoa mawazo haya kutoka kwa utamaduni wa mkikuyu ambao unatoa mwongozo mwafaka kuhusu urithi na uongozi. Baba anapofariki, mtoto wa kiume wa kwanza ndiye huridhi uongozi wa familia kutoka kwa baba na hata mali yote ya familia, bila kujali umri wake. Mama huwa hana lolote wala chochote. Utamaduni haukumruhusu yeye na watoto wa kike kurithi chochote kutoka kwa marehemu baba yao. Hawakuwa na haki kabisa ya kudai chochote. Mama na watoto wasichana wote waliwekwa chini ya himaya ya yule mtoto mvulana aliyemrithi baba yake bila kujali umri au kimo. Mwanamke anadhalilishwa hivi kwamba licha ya umri wake, na kuwa kiwango kimoja cha uzazi na bwanaye, utamaduni bado ulimwona kama mtoto na mtu wa hadhi ya chini. Mamlaka na uongozi yanapewa mtoto mdogo wa kiume badala ya mama yake.

Mkakati wa mkabala haujajitokeza wazi katika methali ya tisa na ya kumi.Methali ya kumi na moja inachukua mkabala wa kuumeni, unaomweka mwanamume katika nafasi ya kwanza na kumpa sifa za kumtwaza. Methali inasifu werevu wa wanaume na kuumithilisha na kisu kilichotiwa makali kikapata. Mwanamume imekuwa ada kwake kusifiwa na kuwekwa mbele. Methali inatudokezea kuwa kwa sababu ya werevu wake, hakuna linalomshida mwanamume. Ana uwezo wa kutatua matatizo yote na huweza kupata suluhu kwa shida zote. Mwanamume anachukuliwa kama asiyekuwa binadamu wa kawaida . Mwanamume anasawiriwa kama mtu mwenye uwezo mkubwa kiakili. Binadamu asiyeshindwa kutatua tatizo lolote. Dhana hii inakiuka kaida kwa sababu mwanamume sio mkamilifu vile methali inaeleza. Kuna uwezekano mwanamume kushindwa kuyatatua baadhi ya matatizo yanayomkumba. Huo ndio ukweli na kawaida ya maisha.

Methali ya kumi na mbili inachukua mkabala wa kumsawiri mwanamume kama kiumbe bora akilinganishwa na mwanamke. Methali inasema kuwa mtoto mvulana si sawa na mtoto wa kike. Huu ni ubaguzi wa wazi. Utamaduni wa mkikuyu ulimbagua mtoto msichana tangu utotoni. Mtoto wa kiume alipendelewa katika ada na matambiko yote yaliyofanywa kwa ajili ya mtoto aliyezaliwa Mtoto wa kiume alichukuliwa na kutunzwa kama tuni. Mambo yote aliyofanyiwa yalikuwa bora yakilinganishwa na ya mtoto wa kike. Ndoa iliyobarikiwa na watoto wa kike pekee ilisemekana kuwa bado hawajabarikiwa na mtoto. Jamii ilichukuliwa kuwa mtoto ni yule wa kiume wala si wa

kike. Dhana hii ya kumpendelea mtoto wa kiume iko katika jamii nyingi za Kiafrika. Waliamini kuwa ilikuwa ni kupoteza pesa na muda na pia kumharibu msichana anapopelekwa shuleni. Jamii nyingi zilipendelea kuwaelimisha wavulana pekee. Msichana alingojewa afikishe umri wa kuolewa. Hata wengine waliozwa na baba zao wakiwa bado wadogo. Jamii iliamini kuwa kazi ya mwanamke ni kuzaa, kulea watoto, kupika na kumtimizia bwana yake haja za kimwili. Kuna jamii zilizowachukulia wanawake kuwa baadhi ya mali yao, hivi kwamba anapohesabu mali yake, atahesabu bibi na watoto wa kike pamoja.

Methali ya kumi na tatu imechukua mkabala wa kumsawiri mwanamume kama jimbi au dume shujaa. Methali inaarifu kuwa mwanamume aliyeoa bibi mmoja ni bure kabisa. Methali hii inawapa wanaume motisha wa kuoa wanawake wengi. Methali hii inaashiria ubaguzi. Mwanamume ndiye anayetiwa shime aoe wake wengi, bila kujali hisia za bibi yake. Baada ya huyu mwanamume kuoa wake wengi huenda akashindwa kuyatekeleza majukumu yake ya ndoa kwa wake wote kikamilifu. Jambo hili linachukuliwa na jamii kwa urahisi. Jamii inatosheka tu iwapo mwanamume anatosheka kikamilifu. Jamii haimjali mwanamke kabisa. Mke anachukuliwa kama chombo cha kumtumikia mwanamume na kuchangamsha. Mwanamume anapofurahi na kutosheka, jamii nayo inatosheka. Huu ni udhalimu na udhalilishaji wa wanawake.

4.2.1.5 Mkakati wa Kufifiza

Wodak (2001: 73) anaeleza kuwa mkakati wa kufifiza huchunguza iwapo matamko ya ubaguzi yalitolewa kisiri au kwa uwazi, kimaksudi au kisadfa. Mtafiti aliangalia na kuchunguza, kisha akalinganisha jinsi wahusika wa kike na wa kiume walivyosawiriwa, huku akitilia mkazo wanaume ili kubaini jinsi wanaume wanavyotambuliwa katika jamii. Katika methali nyingi, wanawake walitaka kuhusishwa na ufanisi, lakini wanaume walitaka kusababisha kufaulu.

Katika methali ya kwanza, vijana wanaume walio jasiri walihusishwa na baba yao, ilihali wale waoga walihusishwa na mama yao. Hivi ni kusema kuwa wanawake wamesawiriwa kuwa waoga wakilinganishwa na wanaume waliohusishwa na ujasiri. Methali inatoa wazo kuwa wanaume hutenda matendo ya kijasiri au kishujaa. Huu ni ubaguzi wa wanawake wanapewa taswira ya kuwa waoga. Kufifiza kunajitokeza kwa jinsi ambavyo mume amekwezwa naye mwanamke anadhalalishwa. Mwanamume

ametunukiwa taswira ya ujasiri. Methali hii inamchora mwanamke kwa njia ya uhasi naye mwanamume kwa njia chanya. Mwanamume anapewa sifa nzuri naye mwanamke amepewa sifa mbaya. Huu ni ubaguzi wa jinsia. Mtafiti uligundua kuwa kumpa mwanamke sifa mbaya yenye unyonge ya woga ni kipengele kimoja cha mkakati wa ufifizaji.

Mkakati wa kufifiza haujajitokeza kwa njia ya wazi katika methali ya pili. Mkakati wa kufifiza umejitokeza vyema katika methali ya tatu na maelezo yake ni sawa na yale mtafiti ameeleza katika methali ya kwanza, yaani ya kuwahusisha wanaume na werevu. Mkakati huu wa kufifiza unajitokeza katika methali ya nne. Methali inatujuza kuwa mtoto mvulana ndiye ngao ya nyumba yao. Hivi ni kusema kuwa familia ambayo haina mtoto wa kiume haina kinga dhidi ya mahasidi wake. Methali hii inampendelea mwanaume na kumsawiri kwa njia chanya. Tunapata wazo kuwa mwanamke hawezi kuishi bila ulinzi wa mwanamume. Lazima kuwa na mwanamume katika familia ili familia hiyo ifurahie usalama. Hapa mwanamke amechorwa kama mtu mnyonge ambaye hawezi kujisimamia, ni lazima amtegemee mwanamume. Huu ni ufifizaji. Mkakati wa kufifiza unajitokeza pale mwanamke anaonekana kuwa hana uwezo wa kujisimamia. Nomino “Ngao” imetumika kijazanda kusimamia mlinzi. Mwanamume kupewa sifa ya ngao ni kumweka mbele sana. Ngano hufanya kazi nzuri ya kimkinga anayeitumia dhidi ya silaha za hasidi wake. Hivyo mwanamume ataikinga familia yake dhidi ya madhara yote ya adui.

Mkakati wa kufifiza haujajitokeza kwa njia ya moja kwa moja katika methali ya tano. Methali ya sita inatuarifu kuwa mwanamume anapopiga kamsa, anayefika kumsaidia ni mfalme.Nomino mfalme imetumika kujizanda kumaanisha mtu wa ngazi ya juu, kijamii, kiuchumi au kisiasa. Ilikuwa nadra kwa mwanamume kupiga mayowe akiitisha msaada, na kama ingefanyika, basi jambo lisilokuwa la kawaida huwa limetokea. Methali hii inampa mwanamume taswira ya mtu aliyejitosheleza na asiyehitaji msaada wowote kutoka kwa mtu yeyote, na kama angehitaji msaada, basi haungetolewa na mtu wa kawaida. Dhana ya kufifiza inajitokeza wazi. Mwanamume hapa anasawiriwa kama mtu anayetoa msaada lakini siye anayepokea, na iwapo ilibidi apokee msaada, sio kutoka kwa akina yakhe. Mwanamke ndiye aliyetarajiwa kuitisha msaada wakati wowote na angeupata kutoka kwa mtu yeyote yule.

Mkakati wa kufifiza haujajipambanua katika methali ya saba, lakini umejidhihirisha katika methali ya nane. Methali inasema kuwa mtoto wa kiume wa kwanza ni sawa na babake. Hii ni kwa sababu baba akifariki dunia bila kujali umri au kimo, yule mvulana ndiye hurithi mali na uongozi wa familia kutoka kwa baba. Mama yake licha ya umri wake mkubwa na hekima yake, hapewi nafasi kamwe ya kurithi chochote au ya kuiongoza familia. Huu ni ubaguzi uliodhamiliwa hadharani wa kumdhalilisha mwanamke. Matamshi haya ya ubaguzi ya kumlinganisha mtoto mvulana na babake yalitolewa kimaksudi wala si sadfa. Uakisi huu ulikusudiwa hivyo. Kwa kawaida, katika mazingira ya kila siku, baba na mama wako kiwango sawa cha kuwa wazazi. Wote wana majukumu ya kutekeleza ikiwa ni pamoja na kuwalea watoto wao. Hivyo basi, wanatakiwa kuwa na haki sawa katika uongozi wa familia yao; lakini methali inamweka mama kando, na kumchukua mtoto wa kiume na kumweka katika kiwango kimoja na baba yake bila kujali umri. Katika hadithi ya "*Bombe mlezi wa mamba"* ya kipokomo, mhusuka mkuu Bombe alinukuliwa akisema;

"*Wanawake watatoa ushauri gani, afadhali nijadiliane na mwanangu wa kiume Kore angalau atakuwa na maoni ya maana*…"(Habuko:2013)

Sentensi hii inadhibitisha wazi kuwa mwanamume amemdharau mkewe hadharani. Kwa upande wa pili, anamthamini mwanawe wa kiume. Kwa jumla, mwanamke amefifizwa kwa sababu amewekwa chini ya manamwe wa kiume. Ni dhahiri kuwa katika methali hiyo, mwanamke amefifizwa naye mwanamume amekwezwa pale ambapo mtoto wa kiume analinganishwa na babake.

Mkakati wa kufifiza unadhihirika pia katika methali ya tisa inayosema kuwa mtoto wa kiume haadhibiwi na mamaye baba akiwa karibu. Hii ina maana kuwa mama hakuwa na haki ya kumwadhibu mtoto wa kiume mbele ya babake. Ikiwa lazima adhabu itolewe,basi mama angengoja mpaka baba aondoke, na asipoondoka, ile adhabu haitolewi kabisa. Licha ya mama kuwa mzazi wa mtoto yule ananyimwa haki ya kumwadhibu mwanaye . Mwanamke anafifizwa kwa njia ya moja kwa moja. Haya matamko yalikusudiwa wala si yaliyotokea kisadfa. Watoto wa kiume walikua wakijua kuwa mama hakuwa na haki ya kuwaadhibu.

Mkakati wa kufifiza haujajidhihirisha katika methali ya kumi. Kwa kiasi kidogo tu, mkakati huu unajipambanua katika methali ya kumi na moja inayodai kuwa werevu wa wanaume hukata kama kisu kilichotiwa makali kikapata. Hapa, mwanamume anawekwa mbele sana kwa kurudikiwa sifa ya werevu, huku mwanamke akionekana kuwa mjinga. Huu ni ufifizaji unaotokana na uwezo wa jinsia hizi mbili.

Mkakati wa kufifiza unajitokeza wazi katika methali ya kumi na mbili. Methali inasema kuwa mtoto wa kiume si sawa na mtoto wa kike. Mtoto wa kike anabaguliwa moja kwa moja.Yule wa kiume amepewa umuhimu mkubwa na jamii kiasi kwamba ndoa isiyokuwa na mtoto wa kiume ilisemekana kuwa haijabarikiwa na mtoto bado. Matamshi haya ya kumpendelea mtoto wa kiume na kumbagua yule wa kike yametolewa hadharani bila hata kupunguzwa makali. Jamii inaonekana kutompenda mtoto wa kike. Hata baada ya kuzaliwa, ada alizofanyiwa mtoto wa kiume zilikuwa tofauti na zile za mtoto wa kike. Hivyo, ufifizaji wa mwanamke ulianza tangu kuzaliwa hadi uzeeni na hata katika kifo.

Methali ya kumi na tatu inadhihirisha mkakati wa kufifiza kwa njia ya wazi sana. Methali inasema kuwa mume wa mke mmoja ni bure. Kwanza, mke amerejelewa kwa jina la kikikuyu, "*Muka"*, ambalo ni jina la madharau la kumrejelea bibi ya mtu, au mwanamke aliyeolewa. Mwanamume naye amerejelewa kama *"mundu"* ambalo ni jina la staha la binadamu. Mwanamke anabaguliwa kwa kurejelewa kwa jina la kuonyesha dharau, huku mwanamume akirejelewa kwa jina la heshima. Ufifizaji wa mwanamke pia unajitokeza pale mwanamume anahimizwa kuoa wake wengi ili asionekane mnyonge. Mwanamume mwenye nguvu, hadhi na shujaa alijulikana kwa kuoa wake wengi.Wanawake walichukuliwa kama mali ya mwanamume. Jamii ilitosheka tu iwapo mwanamume aliyafurahia maisha kwa kutimiziwa haja zake zote na wake zake.Jamii haikujali hisia za wale mabibi iwapo yule mume hakuweza kuwatimizia haja zao za kimwili kindakindaki. Mume aliyeoa bibi mmoja anamithilishwa na mende mdogo.Tunajua kuwa mende ni mdudu anayepatikana kwenye mazingira machafu.Tena mwanamume wa bibi mmoja analinganishwa na yule mende mdogo kabisa. Hii ni kutaka kuonyesha ya kuwa ni kama hatia kuoa bibi mmoja. Matamshi haya yametolewa wazi tena hadharani kudhibitisha ufifizaji. Badala ya kupunguzwa, yaonekana kuongezwa makali.

4.2.2. Methali Za Mkabala wa Kiuchumi

Methali zifuatazo sita zilimtambulisha mwanamume katika mkabala wa kiuchumi. Jamii nzima ya Agikuyu ilijihuzisha zaidi na shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, uhunzi, ufugaji, uwindaji (usasi) na uchongaji. Shughuli hizi zote za kiuchimi, zilitawaliwa na wanaume. Wanawake hawakuhuzishwa hata kidogo katika shughuli hizi. Zifuatazo ni methali sita za mkabala wa kiuchumi.

i). *Gutiri munini mukia*

ii). (Hakuna mwanamume wa umri mdogo anayestahili kuitwa maskini).

iii). *Njamba nyinyi ndinyakagwo*

iv). (kijana mwanamume hadharauliwi).

v). *Mwanake wina indo ndoihanaga*

vi). (Barobaro mwenye mali hasumbuki kumtongoza msichana).

vii). *Uthaka wa mundurume ti magego*

viii). (Utanashati wa mwanamume si meno).

ix). *Uhii niumagwo no utumia ndumagwo*

x). (wavulana hukua na kua wanaume, lakini wanawake licha ya umri hawabadiliki).

xi). *Njamba ikuaga na matanya*

xii). (Mwanamume hufa akiwa bado na matumaini na matarajio ya kutajirika).

4.2.2.1 Mkakati wa Urejelezi

Methali ya kwanza inatoa wazo kuwa jamii ya Agikuyu haikumhesabu mwanamume yeyote yule wa umri mdogo kuwa maskini kwa sababu waliamini kuwa bado kulikuwa na nafasi yeye kufanikiwa kiuchumi. Jamii iliamini kuwa mwanamume hangekufa maskini. Kulikuwa na wazo ganda kuwa yule mwanamume ambaye hajafanikiwa bado nafasi ya kufanikiwa ilikuwako. Hii ilitiwa nguvu na methali nyingine iliyosema.

"Utari muhe ni muigire"

(Yule ambaye bado hajafanikiwa, mali yake imewekwa kando na.

Siku ikifika atakabidhiwa).

Mkakati wa urejelezi umejitokeza wazi katika methali hii ya kwanza. Methali imewarejelea wanaume kama matajiri. Methali inatoa wazo kuwa hakuna mwanamume yeyote wa umri mdogo anayestahili kuitwa maskini. Huku ni kumpendelea mwanamume dhidi ya mwanamke. Mwanamume anapewa sifa chanya ya kutokuwa maskini. Umaskini unaonekana kuwa udhaifu na hivyo mwanamume hahusishwi nao. Dhana ya ubaguzi inayojitokeza ni kuwa wanaume wanapendelewa kihadhi, ya kwamba wao hawastahili kuitwa maskini wakiwa wangali wachanga, eti kwa sababu wana nafasi ya kupata utajiri. Jamii pia inaonekana kuwahusisha wavulana na utajiri, wakiwa wangali wa umri mdogo.

Methali ya pili ina maana kuwa mvulana barobaro hadharauliwi. Ilikuwa ni marufuku kumdharau mwanamume, awe mdogo au mkubwa, katika jamii ya Agikuyu. Jamii iliamini kuwa mvulana mdogo anapoendelea kukua kwa umri, huenda akawa tajiri wa kutajika katika jamii. Pia, wavulana ndio warithi wa mali ya familia, viongozi katika familia na mshauri wa jamii. Mkakati wa urejelezi unajitokeza mara tu umuhimu wa mwanamume katika jamii unapoanza kusisitizwa kwa kuambiwa kuwa mvulana mdogo asidharauliwe. Huu ni ubaguzi kwa sababu jamii haitaki kukubali kuwa mwanamume aweza kuwa fukara. Methali inapoonya dhidi ya kumdharau mvulana mdogo, inashabihiana na methali ya waswahili inayosema, “Usione wembamba wa reli, gari la moshi linapita”

Nomino “*Njamba”* inatumika kumrejelea mwanamume. Nomino hii ina maana ya “Shujaa”. Kwa hivyo, licha ya umri, mvulana mdogo bado anatambuliwa na jamii kama shujaa. Kulingana na kamusi ya Karne ya 21 ya Mdee, J.S. na Njogu, K. Shujaa ni mtu mwenye ujasiri, mtu awezaye kukabili mambo ya hatari bila hofu. Hivyo ndivyo jamii inavyomrejelea mwanamume. Matumizi ya nomino “ *Njamba”*ni ya kimaksudi kutaka kumpa mwanamume sifa ya nguvu na mamlaka.Wanawake katika jamii ya Agikuyu hawakupata nafasi ya kutoa maoni yao, kama alivyofanya Khazija katika Mohamed (1990: 1). Nafasi na majukumu aliyotwikwa mwanamke hayakumwezesha kujumuika na wenzake ili wazungumze juu ya unyanyasaji huu. Kiuchumi wanawake hawakujiweza na hivyo, wanaume waliutawala uchumi wote wa jamii.

Methali ya tatu inasema kuwa mvulana barobaro aliye na mali hakuchukua muda mrefu kumtongoza msichana. Hii ni kwa sababu mali yake ilimtetea. Methali hii inawarejelea wanawake kama makahaba waliovutia na mali badala ya mapenzi. Dai hili linatiwa nguvu na methali nyingine ya kikikuyu inayosema,

> "*Muiritu muthaka ahitukagira thome wa ngia".*
> (Msichana mrembo hupitia nje ya nyumba ya maskini na asipate wa kumtongoza).

Tunapata taswira ya kwamba ili mvulana ampate bibi mrembo kwa urahisi , ilibidi awe na mali. Bila mali, Kupata bibi ni shida, na ukipata, huenda si yule mrembo, au si yule uliyemtaka wewe. Methali hii inatoa wazo kuwa mali ilichukua nafasi ya mapenzi. Methali hii inamchora mwanamke kama mtu anayevutiwa na mali badala ya mapenzi. Mwanamume alihitaji kuwa na mali na wasichana wote wangemfuata bila kujali umri wake au ukoo. Methali hii inatoa wazo kuwa mwanamke hana msimamo, hafuati mapenzi wakati wa ndoa ila yeye hufuata mali. Huenda hii ndiyo sababu baada ya kuolewa, mwanamume humchukua bibi yake kama mojawapo ya mali yake.

Mkakati wa urejelezi haujajipambanua wazi katika methali ya nne, lakini umejipambanua katika methali ya tano. Methali inasema wavulana hukua na kuwa wanaume lakini wanawake hawabadiliki licha ya umri. Hapa wanawake wanadhalilishwa kwa kuambiwa ya kuwa tangu wakiwa wadogo hadi kuwa wazima, hawana mabadiliko yoyote isipokuwa ya kunenepa kimwili. Kiakili, kisaikolojia, na jinsi wanvyofanya mambo kijumla, hawabadiliki. Kwa upande ule mwingine, wavulana wanapoendelea kukua na kuwa wanaume wanapata mabadiliko makubwa. Nomino *"Uhii*" inarejelea ile hali ya wavulana kabla ya kupashwa tohara. Jina hili "*uhii*" ni jina la madharau la kurejelea ile hali ya wavulana, lakini tunaambiwa kuwa baada ya kukua na kupashwa tohara, wanabadilika kabisa na kuwa wanaume. Wanaachana na hali ya utoto.

Methali inarejelea hali ya wanawake kama "*utumia*". Hii ni ile hali ya kuwa mwanamke. Kwa dharau, wanawake wanasemekana hawatoki kutoka hali hii, wao hubaki kuwa wanawake wakati wote; wakiwa wadogo na hata baada ya kuwa wakubwa. Methali hii inawabagua wanawake kwa kuwarejelea kama wasiobadilika kamwe licha ya umri wao. Wanaume wanapendelewa kwa kuonyeshwa kuwa wao hubadilika jinsi wanavyobadilika kiumri.

Methali ya sita inatuarifu kuwa shujaa hufa akiwa angali na matarajio ya kufanikiwa. Shujaa anayerejelewa hapa ni mwanamume wala si mwanamke. Jamii iliamini kuwa mwanamume ambaye bado hajafanikiwa kupata mali, alikuwa bado na nafasi na matarajio ya kutarajirika katika mustakabali wake. Iwapo angekumbana na mauti kabla bado hajafanikiwa, hapo ndipo jamii ilitumia methali hii kusema kuwa amefariki akiwa bado na matarajio. Methali hii haikuwalenga wanawake. Hii ni kwa sababu wanawake hawakutarajiwa kumiliki chochote. Mali yote yalikuwa katika himaya ya mwanamume. Huu ni unyanyasaji wa kimenke ingawa jamii ilikuwa imekuabali kuwe hivyo. Ubaguzi wa wazi dhidi ya mwanamke unadhihirika.

4.2.2.2 Mkakati wa Nomino

Wodak (2001:54) alielezea kuwa nomino huchunguza mielekeo inayoambatanishwa na wahusika, sifa hasi au chanya za lugha kuwaakisi wahusika. Nomino huonyesha maana inayoambatanishwa na urejelezi fulani. Katika methali ya kwanza, makakati wa nomino umejitokeza wazi. Methali inasema kuwa hakuna mwanamume wa umri mdogo ambaye anastahili kuitwa maskini. Hii ni kwa sababu yule mwanamume bado ako na muda wa kuchuma na kupata mali. Nomino "*munini"*, ikimaanisha mdogo, ni jina la heshima la kumrejelea mvulana ambaye bado hajakomaa. Nomino hii imetumika kimaksudi kumrejelea mwanamume kwa lugha isiyo na ukali. Hii ni kuonyesha jinsi utamaduni wa mkikuyu ulivyomtambulisha mwanamume. Nomino "*mukia*" ina maana ya maskini. Pia nomino hii imetumiwa maksudi badala ya nomino "*Muthini"* ambayo ina maana ya maskini. Katika ya nomino hizi mbili, "*Mukia*" ndiyo nomino ambayo imepunguza makali ya neno maskini. Nomino "*Muthini"* ina makali sana na ndiyo sababu haikutumiwa katika methali hii. Hapa tunaona mwanamume akipendelewa na utamaduni wa jamii, na kupewa sifa chanya.

Mkakati wa nomino umejipambanua katika methali ya pili inayosema kuwa mwanamume wa umri mdogo na aliye hodari hadharauliwi. Methali inaonya dhidi ya kuwadharau wanaume kwa misingi ya umri. Hata awe wa umri mdogo, bado yeye ni mwanamume. Hata waswahili husema;

> "Mume ni mume, hata awe gumegume, ana sifa za mtume".

Methali imetumia nomino "*Njamba*" kumrejelea mwanamume. Nomino hii ina maana ya "Shujaa". Basi, methali inapomrejelea mwanamume kwa nomino "*Njamba"*,

inampa huyu mwanamume sifa chanya, na anawakilisha kundi zima la wanaume katika jamii. Methali inatuonyesha nafasi aliyopewa mwanaume katika jamii. Pia, inatufafanulia jinsi mwanamume anavyotambuliwa katika jamii ya Agikuyu. Utamaduni ulimheshimu mwanamume kabisa hivi kwamba kulikuwa na matumaini makubwa kwa mwanamume kuwa siku moja atafanikiwa. Jamii inamchukulia mwanamume kama nguzo ya jamii. Jamii ilitoa onyo dhidi ya kumdharau mwanamume kwa misingi ya umri, sawa na methali ya Kiswahili inayosema;

"Usione wembamba wa reli gari la moshi linapita".

Mwanamke amejamiishwa kuikubali kauli hii, ya kuwa mwanamume ako pale, na nafasi yake na majukumu katika jamii yanaeleweka na wote.

Makakati wa nomino haujajitokeza wazi katika methali ya tatu. Methali ya nne inatueleza kuwa utanashati wa mwanamume si meno. Si kawaida wanaume kuangaliwa kwa misingi ya utanashati au umaridadi wao. Nomino "*uthaka"* iliyo na maana ya utanashati imetumika hapa kumpa mwanamume sifa chanya. Methali inaelezea kuwa unapotaka kuangalia na kuuona umaridadi wa mwanamume usiangalie meno. Nomino meno hapa limetumika kusimamia vitu vyote katika mwili wa binadamu vinavyoweza kuonekana kwa macho. Methali hii inawalenga wanawake. Inawajuza wanawake kuwa wanapotazama uzuri wa mwanamume, wasiangalia jinsi alivyovaa au jinsi mwili wake ulivyo kwa umbo. Mwanmume ni zaidi ya yanayoonekana kwa macho. Mwanamume si sura, mbali ni alicho nacho, yaani mali anayomiliki. Pia, mwanamume atathaminiwa kwa uhodari wake, bidii yake na uwezo alionao wa kuingoza jamii yake. Urembo kwa mwanamke ni aula, lakini kwa mwanamume, mali na maadili mema ndio chambo cha kuwanasa wasichana. Kwa hivyo, utanashati wa mwanamume haukupimwa kwa mizani ya sura yake au umbo lake, bali ulipimwa kwa misingi ya bidii yake na mali aliyonayo.

Wanawake nao hutahadharishwa wasije wakajikita katika kutafuta urembo tu. Methali inayowaonya ni;

"Uthaka nduriagwo"

(Urembo hauliwi).

Hii ina maana kuwa urembo peke yake kwa mwanamke hautamfaidi sana. Lazima ule urembo uambatanishwe na bidii kazini, kuhudumia famili yake, kuwa mtiifu kwa

bwana yake na awe na maadili mema. Methali hii ilitumiwa kuwafanyia wanaume kampeni za kupata bibi. Wanawake wanaambiwa wasiangalia umbo la mwanamume au sura. Kwa hivyo, mwanamume hata akiwa kilema au kiwete, atapata bibi, bora tu ajiweze kiuchumi.

Methali ya tano inasema kuwa wavulana hukua, wakabadilika na kuwa wanaume, lakini wanawake hawabadiliki licha ya umri. Methali hii imetumiwa kuwadhalilisha wanawake na kuwabagua. Wanaume wamepewa sifa chanya huku wanawake wakirundikiwa sifa hasi.

Nomino "*uhii*" imetumika kwa njia ya madharau kurejelea hali ya mvulana ambaye bado hajapatana na kisu cha ngariba. Lakini, hata baada ya kuwarejelea wavulana kwa hiyo nomino inayoonyesha dharau, methali inatuambia kuwa wale wavulana baada ya kukua na kupashwa tohara, hubadilika na kufuzu kuingia katika kiwango cha kuitwa wanaume kamili. Wanaachana na yale mambo ya utoto na kuanza mambo ya utu uzima. Jamii inawakubalia kuoa, kumiliki mali, kuriithi mali na hata kuongoza jamii. Ni furaha kubwa kwa vijana kuvuka lile daraja la kuwa watoto na sasa kuitwa watu wazima, ambako wanatwikwa majukumu katika jamii.

Kwa upande ule mwingine, methali inatupa wazo kuwa mwanamke, kutoka utotoni hadi uzeeni, hana mabadiliko yoyote. Hii haimaanisha kuwa habadiliki kimwili, bali ni kijamii. Mwili wa wanamke utakua, tangu akiwa mtoto, awe msichana mkubwa, aolewe, apate watoto, azeeke mpaka afikie kifo. Lakini, jamii haitambui mabadiliko hayo. Jamii humwangalia na kuchukulia mwanamke kama mtoto licha ya umri wake. Hata baada ya kuolewa na kupata mtoto, mwanamke anabaki na yale majukumu yake ya nyumbani ya kupika, kuosha, kuwahudumia watoto wake na kumtumikia bwana yake. Hakupata nafasi ya kupewa jukumu la kuongoza, kumiliki mali au kurithi mali. Jamii ilimwona tu kama mtoto ambaye lazima aongozwe wala si kuongoza. Nomino "*utumia*", pia imetumiwa kimadharau kurejelea hali ya kuwa mwanamke. Utamaduni ulipendelea mwanamume dhidi ya mwanamke.

Mkakati wa nomino unapitikana katika methali ya sita inayosema," mwanamume shujaa hufa akiwa bado na matarajio ya kufanikiwa kiuchumi". Kwa kumpendelea mwanamume, utamaduni wa mkikuyu humwona mwanamume kama kiumbe ambaye lazima afanikiwe maishani. Yule atafikia mauti yake kabla ya kufanikiwa, utamaduni

unasema kuwa amekufa akiwa na matumaini ya kufanikiwa. Nomino "*Njamba"*, inayomaanisha shujaa imetumika kuwarejelea wanaume wote katika jamii kwa njia chanya. Mwanamume amepewa sifa ya kuitwa shujaa. Shujaa ni mtu mwenye ujasiri, awezaye kukabili mambo ya hatari bila hofu. Utamanduni unatupa taswira ya mwanamume ambaye ni shujaa, anayeyakabili yote yanayoikumba jamii. Mwanamume ni kiongozi na mlinzi wa jamii. Hii ndiyo sababu ya utamaduni kutuchorea picha ya mwanamume shujaa.

4.2.2.3 Mkakati wa Ubishi

Mkakati wa ubishi unahusika hasa na kufafanua ubaguzi unavyodhihirika katika matini teule. Mkakati huu pia hufafanua sababu za kuwepo kwa tofauti za usawiri. Mkakati huu utamsaidia mtafiti kudondoa vipengele mahususi vya lugha vitakavyothibitisha uwepo wa ubaguzi. Vipengele vitakavyodondolewa kutoka kwa matini vitajumuisha sentensi, nomino, virai na vishazi vinavyoakisi utambulisho wa mwanamume katika methali za wakikuyu.

Methali ya kwanza inatuarifu kuwa hakuna mwanamume wa umri mdogo anayefaa kuitwa maskini. Hapa mwanamume anasawiriwa kama mtu tajiri ambaye hapaswi kuwa maskini. Huu ni ubaguzi wa kumpendelea mwanamume. Dhana hii ya kwamba mwanamume hawezi kuwa maskini ni potovu kwa sababu wakati huo na hata sasa, kuna wanaume wengi ambao ni fukara kabisa, lakini methali inatoa dhana kuwa bado mwanamume ana muda wa kutafuta mali, hivyo asiitwe masikini. Methali hii inatiwa nguvu na methali nyingine ya kikikuyu inayosema,

"*Utari muhe nimuigirie*"

"Yule ambaye bado hajafanikiwa, siku inakuja ya fanaka"

Inaaminika kuwa wale ambao hawajafanikiwa bado kuna nafasi ya kufanikiwa, hivyo wasife moyo. Methali hii inawapendelea wanaume sana.

Methali ya pili inakaribiana sana na ile ya kwanza. Inasema kuwa mwanamume wa umri mdogo hadharauliwi. Mwanamume huyu amerejelewa kama "shujaa". Ubaguzi wa kimenke unadhihirika. Licha ya umri wake mdogo, mvulana asidharauliwe kamwe. Jamii iliamini kuwa mwanamke,licha ya umri wake mkubwa, mbele ya macho ya jamii ni dhalili. Kwa upande mwingine, mvulana, licha ya kuwa mtoto wa umri mdogo, mbele ya macho ya jamii, ndiye aliye na wazo la kusaidia jamii. Huu ni

ubaguzi wa kimenke. Jamii iliamini kuwa huyo mvulana mdogo atabarikiwa katika mustakabali wake awe tajiri wa kutajika na mtu wa kuheshimiwa. Hivyo, mtoto mvulana alipewa heshima na jamii yote. Yule wa kike hakuthaminiwa. Wakati mwingi hata haikujulikana kama yupo au hayupo. Uwepo wake haukuwa na maana.

Methali ya tatu inasema kuwa mwanamume mwenye mali anapohitaji kuoa hupata bibi kwa haraka bila shida kwa sababu ya mali yake. Wanawake wanapewa taswira ya kuwa kama washerati wanaofuata mali. Mwanamke amedunishwa kwa kuambiwa kuwa wanafuata mwanamume aliye na mali bila kuangalia mambo mengine. Maadili ya mtu ni muhimu kuliko mali. Huu ni ubaguzi wa kimenke. Methali hii inatiwa nguvu na methali nyingine ya jamii ya Agikuyu inayosema,

"*Muiritu muthaka ahitukagira thome wa ngia*"

"Msichana mrembo hupita karibu na nyumba ya masikini bila kutongozwa".

Methali hii ina maana kuwa mvulana aliyefikisha umri wa kuoa, na awe hana mali, atakutana na msichana mrembo, lakini hawezi kumtongoza kwa sababu ya hali yake ya kiuchumi. Tunapata taswira kuwa ili kupata bibi, ilibidi uwe na mali. Pesa ni mambo yote. Leo, tunao usemi unaotumiwa na watu wengi wa, "*mwanamume ni pesa*". Hii ina maana kuwa mwanamume akiwa na pesa, mambo mengi huwezekana tena kwa urahisi. Mwanamume bila pesa huwa ni balaa tupu.

Methali ya nne inatujuza kuwa utanashati wa mwanamume siyo meno. Hii ina maana kuwa uzuri wa manamume haupimwi kwa mizani ya umbo la mwili wake, bali kwa kile alicho nacho, yaani mali aliyonayo. Methali hii inawatetea wanaume wasiokuwa na sura nzuri. Wanawake wanaambiwa wasiangalie sura ya mwanamume, bali waangalie kile mwanamume alicho nacho. Methali ya kwanza na ya pili zinawatetea wale wanaume wasiokuwa na mali. Hivyo, methali hizi tatu zinawafanyia wanaume kampeni wasikose mabibi eti kwa sababu ya sura au kukosa mali. Huu ni upendeleo kwa mwanamume na kumnyima mwanamke uhuru wa kufanya uamuzi wake.

Methali ya tano inatuarifu kuwa wavulana hubadilika baada ya kupashwa tohara wakawa wanaume, lakini wanawake licha ya umri hawabadiliki. Methali hii inawadunisha wanawake kwa kuwanasibisha wasichana wadogo na akina mama wazee kuwa sawa. Methali inadai kuwa wanawake wote ni sawa licha ya umri wao. Wawe wadogo au wakubwa, wote mbele ya macho ya jamii ni sawa. Hii ni dharau

kwa wanawake. Wanawake wamesawiriwa kwa njia hasi. Hii ndiyo sababu jamii ilitoa mwongozo kuwa baada ya kifo cha kiongozi wa familia (baba), mtoto wa kwanza wa kiume katika familia hiyo ndiye huchukua usukani sio mama. Licha ya umri wa mama, atakuwa chini ya uongozi wa mtoto wake mdogo wa kiume. Wanawake wamedhalilishwa na kusawiriwa kama watu wasiokomaa hasa kiakili.

Methali ya sita inatoa wazo kuwa mwanamume hufa akiwa bado ana matumaini ya kufanikiwa. Methali imemsawiri mwanamume kama "*Njamba*" yaani shujaa.Mwanamume anapendelewa hata wakati hana mali, inasemekana bado kuna matumaini. Anapokufa akiwa maskini,tunaambiwa kuwa amekufa bado akiwa na matumaini. Hivi ni kusema kuwa jamii haikuamini kuwa mwanamume anaweza kuwa maskini hadi kufa. Katika kila hatua ya maisha ya kiuchumi kwa mwanamume, kuna methali ya kuitetea hali hiyo.

4.2.2.4 Mkakati wa Mkabala

Mkakati wa mkabala hujaribu kufafanua ni katika mkabala upi ambapo urejelezi, upachikaji wa majina na mabishano unaoegemea katika kusawiri ubaguzi, maelezo, ufafanuzi na utoaji wa idhibati za ubaguzi. Vitendo au uneni unaoonyesha ubaguzi hujadiliwa katika mkakati huu.

Methali ya kwanza inasema hakuna mwanamume wa umri mdogo anayestahili kuitwa maskini hata ikiwa hana mali. Methali hii imechukua mkabala wa kumsawiri mwanamume kama kiumbe asiyepungukiwa hasa na mali. Kulingana na maoni ya jamii, mwanamume ambaye hajafanikiwa kupata mali hutiwa shime kwa methali inayosema;

"Utari muhe ni muigire".

Yule ambaye hajafanikiwa, amewekewa mali yake na maulana.

Methali hii nayo huwaweka wanaume wasiokuwa na mali wakiwa na matumaini ya kwamba siku moja watafanikiwa. Utamaduni umemkweza mwanamume kiasi kwamba anapendelewa na kupewa sifa ambazo kweli hastahili. Badala ya kumwita mwanamume asiye na mali "maskini", anatafutia jina jingine anaitwa mtarajia. Methali ya pili ina wazo hilo pia ya kwamba mwanamume hawezi kuwa maskini. Methali inashauri kuwa si vyema kumdharau mvulana au mwanamume wa umri mdogo. Hii ni dhana ya kuwafanya wanaume waheshimiwe hata wale wa umri mdogo.

Huu ni mkabala wa kiume. Mwanamume anapewa nafasi ya juu akilinganishwa na mwanamke. Methali hii hutoa dhana kuwa hata ikiwa mvulana ni mdogo, jamii inamheshimu. Jamii humkweza mvulana mdogo na kumdhalilisha mwanamke wa umri mkubwa. Kwa ujumla, mkabala uliochukuliwa na methali hii ni wa kiume.

Methali ya tatu inatujuza kuwa barobaro aliye na mali hapotezi muda wake kuwatongoza wasichana. Hii ni kwa sababu wasichana ndio humtafuta kwa sababu ya mali yake. Methali hii imechukua mkabala wa kumsawiri mwanamke kama Malaya, anayevutiwa na mali ya mwanamume badala ya mapenzi. Mali, katika methali hii imepewa taswira ya kuwa kivutio cha wanawake katika ndoa. Mwanamume mwenye mali ataketi tu kitako na kuwangojea wanawake wajilete, naye achague anayempenda au atakaowapenda. Mwanamke amethalilishwa kabisa na kupewa taswira ya Malaya. Mwanamume mwenye mali naye amesawiri kama mfalme, anayetumikiwa na mali yake. Kwa ujumla, mkabala uliochukuliwa na methali hii ni wa kiume.

Methali ya nne inatuarifu kuwa utanashati wa mwanamume si meno. Methali hii ina maana kuwa uzuri wa mwanamume si umbo lake bali ni kile alicho nacho. Leo hii, kuna usemi unaopendwa na watu wengi unaodai "*mwanamume ni pesa*". Usemi huu unaotumika leo huwa na maana kuwa kile kilicho cha muhimu kwa mwanamume ni pesa alizo nazo, sio umbo, sura au hata kabila. Bila pesa, mwanamume haonekani kuwa na thamani. Methali hii imechukua mkabala wa kiume, unaomsawiri mwanamume kwa njia chanya, kwa kumtetea asiangaliwe umbo la mwili ausura, bali kile alicho nacho. Methali hii inawafanyia wanaume kampeni hasa wasiovutia kwa sura. Methali hii imeelekezwa kwa wanawake. Inawashauri wanawake wanapofikisha umri wa kuolewa, wasizingatia sura ya mwanamume, bali waangalia yale mali aliyonayo yule mwanamume.

Methali ya tano inasema kuwa wavulana hubadilika na kuwa wanaume baada ya tohara lakini wanawake hawabadiliki licha ya umri. Methali hii inachukua mikabala miwili. Mkabala wa kwanza ni wa kumsawiri mwanamme (mvulana mdogo) kama mrithi wa mali ya familia. Pakitokea kuwa mzazi wa kiume amefariki, mtoto wa kiume wa kwanza licha ya umri ndiye huriithi mali ya familia pamoja na uongozi. Mama yake, licha ya umri hubakia chini ya uongozi wa mwanawe. Hii ndiyo sababu methali inasema kuwa wavulana hukua na kubadilika kuwa mwanaume lakini wanawake hawabadiliki kamwe, huwa wa kuongozwa siku zote bila kupata nafsi ya

kuongoza. Mkabala wa pili uliochukuliwa na methali hii ni wa kiume, unaomsawiri mwanamke kama kiumbe dhalili, ambaye hajiwezi bila mwanamume. Ni kosa kumlinganisha mtoto mdogo wa kike na mama mkubwa wa umri mkuu. Pia ni kosa kumweka mama mzazi chini ya uongozi wa mtoto wake mdogo wa kiume. Mwanamke amepewa taswira ya kiumbe duni, dhaifu na kisichoweza kuongoza licha ya umri. Mwanamume naye amepewa sifa za nguli, yaani hata akiwa na umri mdogo, anasemekana ako na uwezo wa kuongoza familia.

Methali ya sita inatujuza kuwa mwanamume ambaye hajafanikiwa kiuchumi hufa akiwa bado na matumaini ya kufanikiwa. Methali hii imechukua mkabala wa kuwapa wanaume matuamini katika maisha, hasa wale bado hawajafanikiwa kupata mali. Methali hii ina ubaguzi kwa sababu inaelekezwa kwa wanaume tu sio wanawake. Hii ni kwa sababu jamii haikuiruhusu mwanamke yeyote yule kumiliki mali yoyote ile. Ikiwa kwa mfano mwanamke alipata mnyama kama vile kondoo au mbuzi ilibidi amkabidhi yule mnyama kwa bwana yake kwa sababu wanawake hawakuruhusiwa kumiliki mali. Methali hii iliwapendelea wanaume sana kwa kuwapa matumaini katika maisha.

4.2.2.5 Mkabala wa Kufifiza

Wodak (2001:73) alisema kuwa mkabala wa kufifiza huchunguza iwapo matamko ya ubaguzi yalitolewa kimaksudi au kisadfa. Pia mkakati huangalia kama uakisi huu ulikusudiwa hivyo au ulitokea bila kutarajiwa. Mtafiti katika kazi hii alichunguza tabia za wahusika, mambo yao na vipi yanavyojenga namna walivyosawiriwa. Methali ya kwanza inasema hakuna mwanamume wa umri mdogo anayestahili kuitwa maskini. Hii ni kwa sababu kuna muda kwa yule mwanamume wa kufanikiwa maishani. Kuna upendeleo kwa mwanamume pale ambapo jamii haitaki kukubali kuwa kuna mwanamume maskini. Yule mwanamume ambaye hana mali huambiwa bado kuna muda wa kufaniki. Utamaduni umemweka mwanamume mbele sana.

Methali ya pili inatuarifu kuwa si vyema kumdharau mvulana mdogo kwa sababu ya umri wake au mali aliyonayo. Jamii inaamini kuwa huyu mvulana baadaye atafanikiwa maishani. Jamii inaamini kuwa si vyema kumtukana mtoto kwa sababu hujui atakuwa nani baadaye, lakini si hoja kumtukana mzee kwa sababu tayari unajua yeye ni nani. Ufifizaji unajitokeza pale ambapo matamko haya ya ubaguzi yanaonekana kutolewa

maksudi na kwa uwazi. Yalitolewa yakielekezwa kwa wanawake, wanaoambiwa kuwa wasiwadharau vijana wa kiume wasiokuwa na mali. Wanaume katika methali hii wanasawiriwa kama viumbe maarufu. Viumbe ambao ni tofauti na wanawake.

Methali ya nne pia imekusudiwa wanawake. Inawaambia wanawake wasiangalie umbo la mwanamume au sura, bali waangalie kile ambacho mwanamume anacho kiuchumi. Methali hii inawafanyia wanaume kampeni hasa wasiokuwa na sura nzuri wasikose mabibi. Wanawake wanasawiriwa kama Malaya wanaoangalia mali tu bila kuzingatia mambo mengine kama vile maadili. Matamshi haya yalitolewa kimaksudi, yaliyodhamiriwa kuwakweza wanaume na kuwanyanyasa wanawake kwa kuwakataza kujiamulia nani wampende na nani wasimpende. Wanaume wamesawiriwa kwa njia ya kuwatambulisha kama watu wa kipekee, wasiokuwa na udhaifu na waliokamilika.

Methali ya tano inatujuza kuwa wavulana hukua na kubadilika kuwa wanaume baada ya tohara, ilhali wanawake hawabadiliki kutoka utotoni hadi utu uzima. Methali hii inawafifiza wanawake kwa kuwanasibisha wasichana wadogo na akina mama wazee. Wanawake wanapaswa kupewa heshima zao sio kudunishwa na kulinganishwa na watoto wao, kiakili na kinafsia. Matamshi haya yalifanyiwa hadharani, yakikusudiwa wanawake. Mwanamke anadhalilishwa kwa kuambiwa kuwa licha ya mwili kunenepa na miaka kuongezeka, kiakili na uwezo wa kutatua mambo habadiliki. Ndiposa jamii ikawa na methali nyingine ya kikikuyu inayosema;

"Atumia matiri rika"

Wanawake hawana rika.

Methali hii ina maana kuwa wanawake wote ni sawa licha ya umri. Wako sawa katika fikra na utendaji wa mambo. Mwanamume anaonekana kukwezwa. Utamaduni unampendelea sana. Mvulana mdogo anasemekana kubadilika kimwili na kimawazo hadi atakapokuwa mtu mzima. Wanaume wamesawiriwa kama watu weledi.

Methali ya sita inatoa wazo kuwa wanaume shujaa hufa wakiwa na matumaini. Methali hii inawasawiri wanaume kama mashujaa wanaofikia mwisho wa maisha yao wakiwa na matumaini ya kufanikiwa kimaisha. Mwanamume huchorwa wakati wote kama anayefaulu maishani na aliyekamilika hata pale hajakamilika. Utammadini hutoa sababu ya kutokamilika. Matamko haya yametolewa kwa njia ya wazi na kwa kukusudiwa . Methali hii inawasawiri wanaume kama mashujaa wanaopewa sifa nzuri.

Mwanamume anatukuzwa kupita kiasi. Upungufu wa mwanamme unapewa jina jingine na kuufanya usionekane kama udhaifu. Kwa mfano, mwanamume aliyepungukiwa na mali haitwi maskini, bali mtarajiwa. Anaambiwa bado kuna matumaini ya kufanikiwa na akifikia kufa kabla ya kufanikiwa, anaambiwa amekufa akiwa na matumaini.

4.2.3 Methali za Mkabala wa Kijamii.

Methali kumi na moja zilizojadiliwa hapa chini humtambulisha mwanamume katika jamii ya Agikuyu katika mkabala wa kijamii. Utamaduni wa Agikuyu uliwaenzi sana wanaume na kuwapendelea. Jamii ilimweka mwanamume mbele sana huku ikimdunisha mwanamke. Ubaguzi huu ulichukuliwa kama kaida ya jamii na jamii nzima ilikubali jinsi mambo yalivyokuwa. Katika maisha ya kijumla, kulikuwa na zile nafasi na majukumu yaliyotengewa wanaume na wanawake. Ilikuwa wazi kuwa majkumu yaliyotengewa wanawake yalikuwa ya kuwadhalalisha na kuwafanya umuhimu wao usitambulike katika jamii. Majukumu hayo yalikuwa ya kuwafunga pale nyumbani hivi kwamba hawakupata nafasi ya kujumuika na watu wengine huko nje.

Methali zifuatazo kumi na moja ndizo zinazomtambulisha mwanamume katika jamii ya Agikuyu katika mkabala wa kijamii.

1. *Gutiti njamba ya mwera umwe*.
   Hakuna jimbi wa mtamba mmoja.
2. *Gutiri mucii wi kahii utakarugwo mutwe*

   Kila familia iliyo na mtoto wa kiume itapata nafasi ya kupika kichwa cha kondoo.

3. *Mwana mugi akenagia ithe, nake mukigu aturagia nyina na maithori.*
   Mtoto mwerevu humfurahisha babake, naye mpumbavu humhuzunisha mamaye daima.
4. *Mucii uraga ngo ciagirirwo makumbiini*.
   Familia huzambaratika ngao zinapowekelewa juu ya maghala.
5. *Cia athuri nithure*.
   Ya wazee yamepambanuliwa.
6. *Cia mucii iri gacuguma gacio,gatathukagio ni mundurume ungi tiga mwene guo.*

Fimbo ya familia haitumiwi na mtu mwingine yeyote isipokuwa mwenye boma.

7. *Gitiro kia muka wene gitinagio athii.*
   Rhumba ya bibi ya mtu haichezewi wapita njia.
8. *Marakara ma arume matituraga ta ma aka.*
   Hasira za wanaume hazidumu kama za wanawake.
9. *Muici na mundumuka atigaga kieha akua.*
   Anayeshiriki wizi na mwanamke huishi kwa huzuni hadi huyo mwanamke atakapokufa.
10. *Muka wa mwathi ahingaga na kuguru etereire kigurumuki oke*.
    Bibi ya msasi halali usiku hadi bwanaye atakaporejea kutoka mawindoni.
11. *Nyoni ya njamba ndiri gitara*.
    Ndege wa kiume hana kiota.
12. *Muthuri utari kahii niwe wiriragira ngururu*.
    Mzee ambaye hana mtoto wa kiume hujifanyia mambo yake.

4.2.3.1 Mkakati wa Urejelezi

Mkakati wa urejelezi huangalia jinsi majina ya wahusika yalivyorejelewa kiisimu. Pia, mkakati huu huangalia kama kuna dhana yoyote ya ubaguzi wa kirangi, kihadhi au kimaumbile. Majina haya huchunguzwa yana sifa gani au maana gani.

Methali ya kwanza inatuarifu kuwa hakuna jogoo wa mtamba mmoja. Hii ina maana kuwa mwanamume asioe bibi mmoja. Methali hii inawaruhusu wanaume na kuwatia shime kuoa zaidi ya bibi mmoja. Utamaduni wa jamii ya Agikuyu uliwakubalia wanaume kuoa wake wengi mradi tu yule mume awe na uwezo wa kuwakimu. Wanawake walichukuliwa kama “mali” hivi kwamba mume mwenye wake wengi aliheshimiwa katika jamii na kuonekana kuwa mwenye mali mengi. Methali imewarejelea wanaume kama “*Njamba”* yaani shujaa. Kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu ya Tuki (2004), Shujaa ni mtu mwenye moyo dhabiti anayeweza kukabili mambo, hata kama ni ya hatari. Kwa hivyo, wanaume wamerejelewa kama shujaa, hii ikiwa ni kuwapa hadhi ya juu sana wanaume wote kwa jumla. Kwa kuitwa shujaa, tunachorewa picha ya mwanamume anayeweza kuyakabili mambo yote katika jamii, yawe ya hatari au ya usalama. Huyu ni mwanamume anayeweza kusimamia familia yake kikamilifu kisiasa, kiuchumi, kijamii, na hata ki-usalama.

Kumwita mwanamume shujaa ni kumtukuza na kumpa sifa ya juu sana. Hii ni sifa chanya kwa wanaume inayoonyesha jinsi jamii ya wakikuyu ilivyomtambulisha mwanamume. Wanawake nao wamerejelewa kama "*Mwera"* ikiwa na maana ya mtamba. Kulingana ma kamusi ya kiswahili sanifu ya Tuki (2004), mtamba ni mnyama ambaye ameshakuwa na kufikisha umri wa kuzaa lakini hajazaa bado. Kwa kuwarejelea wanawake kama mitamba ni kuwadhalilisha.Kwa kawaida, utawaona kuku mitamba wengi pamoja wakitawaliwa na jimbi mmoja. Hapa tunapata wazo kuwa wanawake ni viumbe wasioweza kujitawala na kila wakati hutaka kuwa chini ya himaya ya mwanamume. Wazo hili halina mashiko na limepitiwa na wakati.

Mkakati wa urejezezi haujitokezi wazi katika methali ya pili. Methali ya tatu inatujuza kuwa, mtoto mwerevu humfurahisha baba yake naye yule mpumbavu humhuzunisha mama yake daima. Kwanza, mtafiti aligundua kuwa nomino "mtoto" katika methali hii inarejelea mtoto wa kiume wala si yule wa kike. Methali hii kwa mara nyingi imehusisha werevu na wanaume, nao ujinga umehusishwa na wanawake. Huu ni ubaguzi wa hali ya juu kwa wanawake. Mvulana anayeonekana kuwa mwerevu anasemekana ni wa baba, naye yule anayeonekana kuwa mpumbavu anasemekana ni wa mama. Hata leo, jambo hili bado liko. Kuna baadhi ya watu katika jamii ya Agikuyu leo wanaowahusisha wale watoto werevu na baba zao, nao wale wapumbavu wanahusishwa na mama zao. Wazo hili ni potovu.

Methali imewarejelea wazazi wa kiume kama "*ithe*" nao wale wa kike kama "*nyina"*. Nomino hizi mbili zinazomaanisha "baba wa" na "mama wa" ni majina ya heshima ya kurejekea wazazi. Hivyo basi, mtafiti aligundua kuwa wazazi wote wawili walirejelea kwa njia ya heshima na chanya, jambo ambalo ni nadra sana hasa kwa wanawake. Ingawa mwanamke amekejeliwa kwa kuhusishwa na yule mtoto pumbavu, amerejerewa kwa jina la heshima kwa kuitwa "*nyina"* yaani "mama wa". Mtoto mwerevu anapohusishwa na baba yake ina maana kuwa mambo yote mazuri hutoka kwa baba, ambaye ni mmwanamume naye mwanamke anapohusishwa na yule ntoto mjinga, ina maana kuwa yote mabaya na ya kisirani hutoka kwa mama. "*Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye; Bali mwana mpumbavu ni mzigo wa mamaye",* *(* Mithali: 10: 1-)

Mkakati wa urejelezi hauonekani kuwa na uzito katika methali ya nne. Methali ya tano inasema kuwa mambo ya wazee huwa yamechunguzwa vyema na kupambanuliwa.

Methali hii inawarejelea wanaume kama wazee. Neno mzee ni jina la heshima la kumrejelea mwanamume hasa aliye na umri mkuu. Neno hili wazee, lilitumika kuwarejelea wanaume walioheshimika katika jamii na waliokuwa na umri mkuu. Wazee ndio waliochaguliwa kuwa wenyeviti wa halmashauri mbalimbali katika jamii. Kwa kawaida, wanawake hawakuruhusiwa kukaa katika vikao vya halmashauri. Methali hii inatuarifu kuwa mambo yote yanayowahusu wanaume huwa yamechunguzwa kwa makini sana. Hii ina maana kuwa wanaume ni watu wa makini, wanaofanya kila kitu kwa umakinifu na kwa mpango mwafaka. Wazo hili linapigwa jeki na methali ya waswahili isemayo, " *Palipo na wazee hapaharibiki neno*". Wazee huhusishwa na hekima.Wanaume katika methali hii wanerejelewa kwa njia chanya na wanapedelewa.

Kulingana na uchunguzi uliofanywa na mtafiti, mkakati wa urejezi haukujipambanua katika methali ya sita. Methali ya saba inasema kuwa rhumba ya bibi ya mtu haisakatwi na wapita njia. Methali hii imetumia mafumbo mazito ambayo yanahitaji mwenye hekima kuyafumbua. Methali ina maana kuwa mke ni wa bwana yake na haruhusiwi kufanya ngono na mtu mwingine yeyote isipokuwa bwana yake. Ubinafsi kwa upande wa wanaume unajitokeza wazi. Utamaduni umepinga mwanamke kushiriki ngono na mwanamume mwingine isipokuwa mumewe, ilhali utamaduni huo ndio unaomkubalia na kumpa ari mwanamume aoe bibi zaidi ya mmoja. Huu ni unyanyasaji kwa wanawake na kuwanyima uhuru wa kujiamulia.

Urejezi unaopatikana katika methali hii ni pale kitendo cha ngono kimerejerewa kwa njia ya staha na kuitwa "*Gitiro"*. *Gitiro* ni mojawapo ya ngoma za kitamaduni, iliyochezwa na wanawake walioolewa. Ngoma hii ilichezwa hasa wakati wa harusi. Wakati mwingine ngoma hii ilichezwa na wanawake kuwatumbuiza waume zao walioketi kitako wakinywa pombe ya kitamaduni. Nomino "*Gitiro*" ilitumika kupunguza makali ya nomino "ngono". Urejelezi mwingine ni pale nomino "*Muka*" imetumika. Nomino hii ni jina la madharau la kumrejelea bibi ya mtu. Hapa ubaguzi wa wanawake unajitokeza. Wanawake wanaonekana kurejelewa kwa njia hasi. Wanaume pia wamerejelewa kwa njia chanya kwa kuitwa "wapita njia". Ni wazi kuwa wanaume wanapendelewa huku wanawake wakidhalilishwa.

Methali ya nane inasema kuwa hasira za wanaume hazidumu kama za wanawake. Ni wazi hapa kuwa mwanamume amerejelewa kwa njia chanya kwa kuambiwa kuwa yeye si mtu wa kuweka hasira kwa muda mrefu. Mwanamke kwa upande wake anarejelewa kwa njia hasi kwa kuambiwa kuwa yeye huweka hasira kwa muda mrefu sana. Methali imerejelea wanaume kama "*arume*", inayomaanisha watu walio na ujasiri. *Arume* ni nomino mwafaka ya kuwarejelea wanaume kwa njia ya heshima na inayowapa hadhi ya juu. Kwa upande mwingine, wanawake wanarejelea kama "*aka".* Nomino *"aka*" ni jina la dharau la kuwarejelea wanawake. Ni jina lisilo na staha. Huu ni ubaguzi kwa wanawake. Wanaume wanarumbikiziwa sifa nzuri ya kutoweka hasira ndani yao kwa muda mrefu, nao wanawake wanadunishwa kwa kuambiwa wao huweka hasira kwa muda mrefu.

Methali ya tisa inatuarifu kuwa mwanamume akishirikiana na mwanamke katika wizi, yule mwanamume ataishi kwa hofu na wasiwasi hadi siku ile yule mwanamke atakapofariki. Hii ina maana kuwa wanawake sio watu wa kuaminika na hawana uwezo wa kuiweka siri. Baada ya kuiba, yule mwanamke anaweza kuifichua ile siri wakati wowote, hasa anapokasirishwa na yule mwanamume waliyeiba naye, au anapokabiliwa na hali ngumu au anapokabiliwa na vishawishi. Hapa wanawake wanarejelewa kama watu wasiokuwa na uwezo wa kuyadhibiti mambo magumu. Udhaifu wao unajitokeza kwa kushindwa kuhifadhi siri kwa muda mrefu. Pia, kuna methali nyingine ya kikikuyu inayosema;

"*Mundu muka na iguru itimenyagirwo*"
Mwanamke na hali ya anga hawatabiriki".

Methali hii inaitia nguvu ile ya kwanza kuonyesha kuwa mwanamke ni kigeugeu, hawezi kuwa imara katika mambo yake. Kuwa kigeugeu kunadhibitisha udhaifu wa mwanamke. Kuwanasibisha wanawake na hali ya anga ni kuwadunisha. Mwanamke anaendelea kupewa sifa hasi kwa kurejelewa kama "*muka",* nomino ambayo ni ya dharau ya kuwarejelea wanawake. Hali ya mwanamke ya kutoaminika ndiyo inayomfanya arejelewa kwa njia hasi na ya madharau.

Kwa upande mwingine, methali inatupa taswira kuwa mwanamume ni mtu aliye na uwezo mkubwa wa kuhifadhi siri. Hata akikabiliwa na vishawishi au hali ngumu, mwanamume hataitoa siri kamwe. Hapa tunamwona mwanamume akipewa sifa ya kuwa mtu dhabiti na imara katika mambo yake. Kinyume na mwanamke,

mwanamume anapewa sifa chanya ya kutokuwa kigeugeu, mtu aliye na msimamo imara na anayeweza kutabirika. Methali hii inamtambulisha mwanamume kama kiumbe maasumu, dhabiti na anayefanya mambo kwa mpango na inavyotakikana. Kwa upande mwingine, tumepewa taswira ya mwanamke ya mtu kimbaumbau mwenye tabia mauzauza. Mwanamke amelimbikiziwa sifa mbaya na hasi. Huu ni ubaguzi. Kuna methali ya wakikuyu inayoipa methali hii nguvu inayosema,

"Muici na Kihii akenaga kiarua"

Anayeshirikiana kuiba na mvulana ambaye hajapashwa tohara hupata afueni mvulana huyo atakapotahiriwa. Methali hii inanasibisha wanawake na wavulana ambao hawajapashwa tohara. Hao wawili ndio wasioweza kuweka siri, watu vigegeu wasioaminika. Kumfananisha mwanamke na huyu mvulana ni kumdunisha na kumdharau.

Methali ya kumi inatujuza kuwa mke wa msasi halali usiku bali hukesha, hadi bwana yake atakaporejea kutoka mawindoni. Wanyama waliwindwa usiku kwa sababu huo ndio wakati wao hutokea kutafuta chakula. Wakati wa mchana, wanyama huwa wamejificha huku wakilala. Kwa hivyo, kazi ya usasi ilifanywa usiku. Methali inatujuza kuwa bibi wa msasi hakuwa na budi ila kumngojea bwana yake mpaka atakaporejea usiku, hata ikiwa ni usiku wa manane.

Mkakati wa usemi wa urejelezi unajitokeza pale mwanamke amerejelewa kama "*muka"*. Jina hili ni la dharau la kumrejelea mwanamke. Ni jina lisilo na heshima na la kumdunisha. Isitoshe, methali inasema kuwa wakati mwanamke anapomngojea bwanaye usiku, huwa amefunga mlango kwa miguu yake. Hii ina maana kuwa hawezi kulala kabisa, ila huwa macho ili bwana akifika, abishe mlango mara moja tu na afunguliwe. Iwapo mwanamume angebisha mlango mara mbili tatu bila kufungulia, ilichukuliwa ya kuwa yule bibi alikuwa tayari amelala, na hiyo ilikuwa hatia ambayo ilimfanya yule bwana amwadhibu bibi yake vikali. Hivyo, mwanamke ilibidi ahakikishe hakushikwa na usingizi ili bwana yake akibisha mara ya kwanza amfungulie.

Kwa upande mwingine, bwana amerejelewa kama "*kigurumuki"*, ikiwa na maana ya mburukenge. Kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu ya Tuki (2004), mburukenge ni mnyama kama mamba mdogo, aishie nchi kavu,mwenye mwili mwembamba, miguu

mirefu na mkia mrefu. Mwanamume kupewa sifa za mburukenge, anayenasibishwa na mamba ni kumtukuza. Anapewa sifa chanya ya mtu hodari anayewinda usiku bila woga. Kule kuwinda usiku tunapata taswira ya mwanamume jasiri asiyekuwa na woga. Kule kunasibishwa na mburukenge, ambaye ni mnyama anayefanana na mamba kunaongeza taswira ya mwanamume jasiri.

Mkakati wa urejelezi unajitokeza katika methali ya kumi na moja. Methali inasema kuwa ndege wa kiume hana kiota. Kinyume na methali zile nyingine zote, methali hii inamtambulisha mwanamume kwa njia hasi. Kwanza, mwnamume amerejelewa kama ndege wa kiume. Ndege ni kiumbe mwenye mabawa na manyoya ambaye aghalabu huruka angani. Ndege ni kiumbe mdogo na dhaifu. Kumlinganisha mwanamume na ndege ni kumdhalilisha. Pili, ndege ni myama asiyekuwa na sifa yeyote, mdogo na asiye na nguvu. Kumfananisha mwanamume na ndege ni kumdharau. Methali inaposema ndege wa kiume hana kiota, ni fumbo linalomaanisha mwanamume ambaye hajaoa hana nyumba. Hii ina maana kuwa mwanamume yeyote asiyekuwa na bibi anaweza kula popote apendapo. Lakini yule aliyeoa, ana nyumbani na lazima alale kwake kila siku. Hapa tunapata taswira kuwa jamii haikumdhamini mtu aliyefikisha umri wa kuoa na bado hajaoa. Yaani jamii haikuwathamini sana waseja. Mseja alionekana kama mtu asiyekuwa na makao yake maalum, na hii ndiyo sababu anafananishwa na ndege wa kiume asiyekuwa na kiota.

Methali ya kumi na mbili inatujuza kuwa mzee ambaye hakubarikiwa na mtoto wa kiume hujifanyia shughuli zote. Methali hii imemrejelea mwanamume hapa kama *"mzee*", jina la heshima la mwanamume aliyekomaa kiumri. Mvulana naye amerejerewa kama "*kahii*", inayomaanisha mvulana mdogo ambaye hajafikisha umri wa kupashwa tohara. Urejelezi huu ni wa staha na chanya. Methali inatupa wazo kuwa hata ikiwa mzee amebarikiwa na watoto wa kike pekee bila mvulana alionekana kama mzee asiyekuwa na mtoto, na hivyo, yeye atajishughulikia kwa mambo yake yote. Mtoto wa kike hakuthaminiwa hata kidogo katika jamii ya wakikuyu. Kama ndoa ingekosa kupata mtoto wa kiume, ilibidi bwana aoe mke mwingine ajaribu bahati ya kupata mtoto wa kiume. Jambo hili linapatikana katika jamii nyingi za kiafrika. Katika tamthilia ya *Wingu Jeusi* ya Chacha Nyaigoti Chacha (1987), mhusika mkuu anamlaumu na kumshutumu mkewe kwa kumzalia. "Majanajike tu". Anafanya

usuhuba na mwanamke mwingine anayetarajia atamzalia mtoto wa kiume. Dhana hii ya mtoto wa kiume, ingawa ni potovu imeshikiliwa na jamii nyingi za kiafrika.

4.2.3.2 Mkakati wa nomino

Mkakati wa nomino una uwiano mkubwa na ule wa urejelezi. Wodak (2001:54) anaelezea kuwa nomino huchunguza mielekeo inayoambatanishwa na wahusika, sifa hasi au chanya za kuwaakisi wahusika. Madhumuni kuu ya mkakati wa nomino ni kuonyesha maana inayoambatanishwa na urejelezi fulani. Mkakati wa nomino unadhihirika katika methali ya kwanza pale wanaume wametajwa kama "*Njamba*" iliyo na maana ya shujaa. Jina hili lina maana chanya. Wanaume wamepewa sifa ya kuwa shujaa ilhali wanawake wamerejelewa kama mitamba. Mitamba ni kuku wa kike ambao hawajaanza kutaga mayai. Kuku wa kike wengi humtegemea jimbi mmoja kuwazalisha. Wakiwa pamoja, mitamba humtambua jimbi kama kiongozi wao. Hapa tunapata wazo kuwa wanawake hawawezi kujiongoza. Lazima wamtegemee mwanamume kuwaongoza.Wanawake wamepewa jina "*mtamba"* lenye maana hasi.

Mkakati wa nomino pia unadhihirika katika methali ya pili. Methali inaashiria kuwa kila familia iliyo na mtoto wa kiume lazima siku moja watapika kichwa cha kondoo. Ikiwa kichwa cha kondoo kitapikwa, hii ina maana kuwa kondoo amechinjwa. Kwa kawaida kondoo alichinjwa wakati wa sherehe. Hii ina maana kuwa familia yoyote ile, iliyo na mtoto wa kiume, itapata nafasi siku moja ya kuandaa sherehe kwao. Hapa tunaona watoto wa kiume wakirejelewa kwa njia chanya, huku kila familia iliyo na mtoto wa kiume akipewa matumaini ya kufanikiwa katika mustakabali wao.

Mkakati wa nomino upo katika methali ya tatu. Majina yote yaliyotumika yana maana chanya. Nomino hizi ni kama vile mtoto, baba na mama. Baba ni jina la heshima la mzazi wa kiume. Mama pia ni jina la heshima la mzazi wa kike. Mtoto ni kiumbe aliyezaliwa na baba ba mama. Methali inawabagua wanawake inapodai kuwa yule mtoto mwerevu humfurahisha babake, naye yule mpumbavu humhuzunisha mama yake siku zote. Ubaguzi unaojitokeza hapa ni kuwa sifa ya werevu inaambatanishwa na wanaume, nayo sifa ya ujinga inaambatanishwa na wanawake.

Mkakati wa nomino haujitokezi katika methali ya nne. Katika methali ya tano, mkakati wa nomino unajitokeza pale wanaume wamepewa jina lenye maana chanya, la "*wazee*". Wazee ni jina la heshima la kuwarejelea wanaume walio na umri mkuu na

wanaoheshimika. Methali yaeleza kuwa mambo ya wazee huwa yamechunguzwa vyema na kupambanuliwa kwa hekima. Ndio sababu waswahili pia walisema palipo na wazee hapaharibiki neno. Unominishaji katika methali hii ni chanya na wanaume wamepewa sifa ya kuwatukuza au kuwapa hadhi.

Mkakati wa nomino haujajipambanua kwa njia ya wazi katika methali ya sita. Katika methali ya saba, mkakati wa nomino umetumika pale ambapo kitendo cha ngono kimerejelea kwa njia chanya kwa kuitwa "*Gitiro"* yaani mojawapo ya ngoma za kitamaduni iliyochezwa na wanawake walioolewa. Nomino hii imetumika ili kupunguza makali ya neno ngono, ambalo kama lingetumika, methali hii ingekosa sitara. Nomino "*muka"* limetumika kwa njia hasi, inayoashiria ubaguzi kwa wanawake. Neno hili linarejelea mwanamke aliyeolewa lakini kwa njia ya madharau. Ni wazi kuwa majina yanayowarejelea wanawake ni ya dharau na ubaguzi.

Vilevile katika methali ya nane, wanawake wamelimbikizwa sifa mbaya huku wanaume wakipewa sifa nzuri sufufu. Wanaume wanarejelewa kwa nomino "*arume"* inayomaanisha wanaume au watu walio na ujasiri, huku wanawake wakirejelewa kwa nomino "*aka"* inayomaanisha "wanawake walioolewa". Nomino hii "*aka*" imetumika kwa njia hasi. Ni jina la kuwabeza wanawake na kuwabagua. Isitoshe wanawake wanasemekana kuwa wanaweka hasira moyoni mwao kwa muda mrefu wakilinganishwa na wanaume wanaotoa hasira moyoni mwao baada ya muda mfupi tu. Yote mabaya ni ya mwanamke nayo yale mazuri ni ya wanaume.

Methali ya tisa, sawa na ile ya nane imetumia nomino "*muka"* kuwarejelea wanawake kwa njia hasi. Methali inatuarifu kuwa mwanamume anayeshiriki wizi na mwanamke hana bahati. Ataishi kwa hofu na atapata afueni siku ile yule mwanamke atakapofariki. Tunapewa taswira ya mwanamke aliye kigeugeu, asiyeaminika, asiyetabirika na asiyeweza kuweka siri. Mtu wa moyo mwepesi. Asiyeweza kustahimili mazito. Methali ya kumi haina tofauti na ile ya tisa na ya nane. Matumizi ya nomino "*muka*" kurejelea mwanamke ni dhihirisho kuwa jamii haikumthamini mwanamke kamwe. Mwanamke ameendelea kurejelewa kwa njia hasi huku nomino zinazotumika kuwarejelea zikiwa ni zile za kuwabeza.

Methali ya kumi inatujuza kuwa msasi anapoenda mawindoni usiku, bibi yake ni kama mtumwa, hana haki ya kulala mpaka bwanaye atakaporejea. Bwana akichelewa hadi

usiku wa manane, bibi hana budi ila kumngojea. Huu ni utumwa. Wanawake wameendelea kugandamizwa na utamaduni unaompendelea mwanamume.

Mkakati wa nomino upo katika methali ya kumi na moja. Mwanamume, kinyume na methali zile nyingine amerejelewa kwa njia hasi kwa kuitwa ndege wa kiume, ambaye hana kiota na hulala popote. Hapa, wanaorejelewa ni wanaume ambao hawajaoa ingawa wamefikisha umri wa kuoa. Nomino kiota limetumika kurejelea makazi au makao. Hii inaonyesha kuwa jamii haikuwathamini wale wanaume wasiokuwa na makazi. Baada ya kuoa, hapo ndipo mwanamume alipopata makazi.

Methali ya kumi na mbili inamrejelea mwanamume kwa njia chanya. Nomino " *muthuri*" ina maana ya "mzee", jina la heshima la kumrejelea mwanamume. Mzee ni mtu aliye na umri mkubwa na mwenye hekima. Kwa kuwarejelea wanaume kwa nomino "wazee" ni kuwapa hadhi ya juu sana. Mtoto mdogo wa kiume katika methali hii amerejelewa kama "*kahii"*, jina la heshima la kumtaja mtoto mdogo wa kiume ambaye hajafikisha umri wa kupashwa tohara. Majina ya wanaume yaliyotumiwa katika methali hii yana maana chanya.

4.2.3.3 Mkakati wa Ubishi

Mkakati wa ubishi husaidia kufafanua na kudhihirisha uwepo wa ubaguzi katika methali teule za jamii ya wakikuyu. Mtafiti aliangalia jinsi ubaguzi ulivyodhihirika katika matini teule. Swali kuu alilozingatia mtafiti ni, je, ni kupitia kwa mbinu gani za mabishano ambapo watu maalum au makundi ya jamii hujaribu kuhahalisha ubaguzi? Dhana ambazo zinakosa ukweli, yaani falasia, pia zilichunguzwa katika utafiti huu.

Mkakati wa ubishi upo katika methali ya kwanza, pale ambapo wanawake wanabaguliwa kwa kurejelewa kama mitamba huku mwanamume anapewa sifa ya kuwa jogoo. Hapa mwanamume anapewa sifa ya uongozi nao wanawake na ndio wengi wanabaguliwa kwa kupewa sifa ya kuongozwa. Pia, mwanamume anatiwa shime asioe bibi mmoja bali aoe wengi. Kwa upande mwingine, mwanamke hapewi nafasi ya kuchagua anapenda nani. Nafasi na majukumu ya mwanamke baada ya kuolewa ni kumtumikia bwana yake, na kungojea bwana yake akioa bibi wa pili, wa tatu au na hata wa nne, awakubali wote bila swali. Wanaume waliwatumia wanawake kama mali inayomfanya aheshimiwe katika jamii. Pia, wanaume waliwatumia

wanawake kama vyombo vya kuwafurahisha na kuwatimizia haja zao za kimwili. Mwanamume aliyeoa bibi mmoja alikashifiwa kwa kuambiwa methali inayosema;

"*Mundu wa muka umwe ni tuhu wa kanyenje."*

Mume wa bibi mmoja ni bure.

Wanaume walisawiri kama mabwana nao wanawake kama watumishi.

Methali ya pili ina ubaguzi uliojitokeza wazi pale inaposema nyumba au familia iliyo na mtoto wa kiume lazima siku moja watapika kichwa cha kondoo, watapata nafasi ya kusherehekea. Ubaguzi dhidi ya watoto wa kike unajitokeza wazi. Watoto wa kiume ndio waliosawiriwa kama watakaofanya familia zao zisherehekee. Mtoto wa kike hakuthaminiwa na jamii. Hili ni wazo potovu kwa sababu siku hizi, kuna familia zinazoishi kwa majonzi kwa sababu ya watoto wao wa kiume. Badala ya sherehe, wao ni kuomboleza. Pia kuna baadhi ya familia ambazo hasina mtoto wa kiume, na mambo kwao ni shwari, raha mustarehe.

Methali ya tatu inaashiria ubaguzi wa hali ya juu dhidi ya wanawake. Methali inanasibisha mtoto mwerevu na baba yake, naye yule mtoto mpumbavu anahuzishwa na mama yake. Hili ni wazo potovu ya kuwa wanaume ni werevu kuliko wanawake. Hata leo, kuna baadhi ya jamii, na watu binafsi wanaowahusisha wale watoto werevu na baba zao nao wale wajinga ni wa mama zao. Methali hii inapendelea wanaume, wanaopewa sifa za kuwapa hadhi ya juu, huku mwanamke akidhalilishwa.

Mkakati wa ubishi haujitokezi wazi katika methali ya nne. Methali ya tano inasema ya kwamba, mambo ya wazee yamepambanuliwa. Hapa kuna mapendeleo kwa wazee. Lolote wanaume wafanyalo, jamii huliona kuwa sawa na lisilo na dosari au kasoro. Ubaguzi unajitokeza pale ambapo wanaume wanaonekana kupendelewa kwa kuambiwa kuwa mambo yao yote huwa maasumu. Methali inatujuza kuwa kabla mwanamume hajatoa neno kinywani mwake, au kabla hajatenda jambo lolote, huwa kwanza ametafakari vyema na kufikia uamuzi mwafaka.

Mkakati wa ubishi haujajipabanua vyena katika methali ya sita, lakini mkakati umetumika katika methali ya saba. Methali inatujuza kuwa Rhumba ya bibi ya mtu haichezwi au haichezewi wapita njia. Methali hii ni fumbo kuu lililofichika. Maana ya methali hii ni kuwa bibi wa mtu hakuruhusiwa kufanya tendo la ndoa na mwanamume mwingine yeyote yule isipokuwa bwana yake. Ubaguzi unadhihirika pale ambapo

mwanamke anarejelewa kama "*muka"* jina ambalo ni la madharau la kumrejelea bibi ya mtu au mwanamke aliyeolewa. Huu ni udhalilishaji wa mwanamke. Lugha ya sitara imetumika wanaporejelea tendo la ndoa kwa kutumia nomino "*Gutiro*" iliyo na maana ya ngoma ya kitamadumi iliyochezwa na wanawake walioolewa. Wanaume nao katika methali wamerejelewa kwa njia chanya kwa kuitwa *"athii*" yaani wapita njia. Hapa tunapata taswira ya kuwa yote yanayowahusu wanaume,jamii huyachukua kwa mwelekeo chanya. Hakuna lolote la mwanaume ambalo ni baya, na hata likiwa baya, jamii huliona likiwa zuri.

Ubaguzi unajitokeza wazi katika methali ya nane pale ambapo methali inawalaumu wanawake kwa kuweka hasira moyoni mwao wakulinganishwa na wanaume. Hakuna utafiti uliofanywa katika jamii ya wakikuyu kudhibitisha dhana hii, lakini kwa vile jamii huongozwa na T.Y.K., wanaume wanapendaelewa na kulimbikiziwa zile sifa nzuri. Ubaguzi mwingine unaonekana pale wanawake wanarejelewa kwa jina la dharau kama "*aka"* na wanaume wamerejelewa kama "*arume*" yaani wanaume au wenye ujasiri. Mwanamke anahusishwa na uovu. Pia, anaonekana kuwa mwenye moyo usio dhabiti, asiyeweza kuyasahau yaliopita agange yaliyomo na yajayo. Methali imetupa taswira ya mwanamke kuwa kiumbe dhaifu, naye mwanamume amechorwa kama mtu imara, aliye na uwezo wa kuyasahau yaliopita na kuganga yaliyomo na yajayo.

Methali ya tisa inadhibitisha ubaguzi wa hali ya juu inapotoa wazo kuwa mwanamume anayeshiriki wizi na mwanamke huishi kwa majonzi mpaka huyo mwanamke atakapokufa. Hii ni kwa sababu jamii iliamini kuwa mwanamke hana uwezo wa kuiweka siri kwa muda mrefu. Kwa sababu ya udhaifu wake, mwanamke ataitoa siri mara moja atakapokasirishwa na yule mwanamume waliyeiba naye, au anapokabiliwa na hali ngumu asioyoweza kustahimili. Tunapata taswira ya mwanamke kigeugeu, asiyeaminika na asiyekuwa na msimamo. Ubaguzi mwingine unapatikana pale mwanamke anapobezwa kwa kuitwa "*mundu muka*", jina ambalo si la sitara kumrejelea mwanamke. Ubaguzi huu pia unapatikana katika methali ya kumi.

Mkakati wa ubishi haupatikani katika methali ya kumi na moja. Mkakati huu unajitokeza katika methali ya kumi na mbili. Methali inatujuza kuwa mzee ambaye hakubarikiwa kupata mtoto wa kiume ndiye hujifanyia mambo yote kwa sababu hana msaidizi. Hapa tunapata dhana kuwa mtoto wa kike hana usaidizi wowote anaoweza

kuutoa kwa baba yake. Huu ni ubaguzi dhidi ya watoto wa kike. Dhana hii ya mtoto wa kike kuwa duni akilinganishwa na mtoto wa kiume ni potovu. Kwa sasa watoto wote ni sawa, na hutoa msaada sawa kwa wazazi wao.

Jamii nyingi za kiafrika hushikilia hii dhana kuwa mtoto wa kiume ni bora zaidi kuliko mtoto wa kike. Hii ni kwa sababu jamii nyingi za kiafrika hufuata mfumo wa T.Y.K. Jamii zote zinazofuata mfumo huu huamini kuwa lolote lifanywalo na mwanamume ni zuri – hata ikiwa ni uchawi.

4.2.3.4 Mkakati wa mkabala

Mkakati wa mkabala huangalia ni kwa mkabala upi ambapo urejelezi, upachikaji wa majina au mabishano ulizingatiwa katika kusawiri ubaguzi wa kimenke katika methali teule. Katika methali ya kwanza, mkabala uliochukuliwa ni wa kumsawiri mwanamume kama nguli. Methali inasema kuwa hakuna mwanamume wa mke mmoja. Methali hii inawatia shime wanaume kuoa wake zaidi ya mmoja, huku mwanamke akinyimwa uhuru wa kujiamulia mambo yawe vipi. Hivyo, mwanamume katika methali hii ni nguli, naye mwanamke amesawiri kama mtumwa asiyekuwa na haki yoyote. Kiumbe dhaifu anayetumiwa na mwanamume kama chombo cha kumtimizia haja zake za kimwili. Mwanamume katika methali amerejelewa kama shujaa, shujaa kwa wanawake, ndiposa anashauriwa aoe zaidi ya mke mmoja. Jamii ilitaka mwanamume awe na furaha na starehe wakati wote. Awe na wake wengi wakumtumikia, iwe fahari kwa mwanamume kuingia nyumba yoyote ile ya mmoja wa mabibi zake, wakati wowote anaotaka, na kupata chochote anachotaka. Kazi kubwa ya mwanamke aliyeolewa ilionekana kuwa ni kumshtarehesha mume wake. Jamii zima ilikuwa imekubaliana na dhana hii. Mwanamume akawa amewekwa juu sana naye mwanamke amedunishwa.

Mkabala uliochukuliwa pia katika methali ya pili ni wa kuumeni, yaani mwanamume amepewa nafasi ya juu sana akilinganishwa na mwanamke. Methali inasema kuwa familia iliyo na mtoto wa kiume itapata nafasi siku moja ya kufurahi na kusherehekea. Hii ina maana kuwa ile familia ambayo haikubarikiwa na mtoto wa kiume haina nafasi kamwe ya kufurahi na kusherehekea. Katika jamii za kiafrika, mtoto wa kiume hudhaminiwa sana. Tamthilia nyingi na riwaya zilizoandikwa kuhusu ndoa huonyesha kuwa ndoa ambayo haikubarikiwa na watoto wa kiume ilisemekana kuwa hawajapata

mtoto bado, hata wakiwa na watoto wengi wa kike. Hii ni kwa sababu, mtoto wa kike hakuhesabiwa kama mtoto katika ndoa.

Methali ya tatu imechukua mkabala wa kumsawiri mwanamume kama mtu mwenye hekima na busara akilinganishwa na mwanamke. Methali inasema kuwa mtoto mwerevu humfurahisha baba yake, naye yule baradhuli humhuzunisha mama yake siku zote. Werevu unahusishwa na wanaume nao ujinga unahusishwa na wanawake. Mwanamume ameendelea kuonekana kama kiumbe bora akilinganishwa na mwanamke. Hata nafasi na majukumu yaliyopewa mwanawake si sawa na yale ya wanaume. Majukumu yaliyohitaji maarifu na ujuzi yalipewa wanaume. Yale majukumu mepesi yasiyohitaji maarifa wala ujuzi wowote yakapewa wanawake.

Methali ya nne imechukua mkabala wa kuumeni. Inawasawiri wanaume kama walio na uwezo wa kujenga na kutengeneza makao ya familia. Methali inasema kuwa baada ya vijana wanaume kuoa, hapo ndipo mambo ya familia walikozalia huanza kusabaratika. Hii ni kwa sababu, kabla ya kuoa, vijana hawa ndio waliotumika kuzilinda familia zao. Walitumia mikuki na ngao. Punde tu walipooa, waliacha kazi ya ulinzi na kuweka ngao zao juu ya ghala. Kuanzia hapo, ile familia inakosa ulinzi dhabiti. Wanawake vijana hawakuhusishwa katika ulinzi. walionekana dhaifu na wasioweza kustahimili vita dhidi ya mahasidi wao.

Methali ya tano inawasawiri wanaume kama watu wenye makini katika kutenda mambo. Huu ni mkabala wa kiume. Methali inadai kuwa mambo yote ya wazee huwa yamechunguzwa vyema na kupambanuliwa bila kufanya kosa. Wanaume wanaonekana kufanya mambo yao kwa makini sana na utaratibu mwafaka. Mwishowe, mambo yao yanakuwa shwari bila kasoro. Hata pale mwanamume atakosea, jamii haitaliona lile kosa; kwa mfano, tembo inapotumiwa na wanaume, huonyeshwa uume, lakini tembo hiyo hiyo inapotumiwa na wanawake, ilionyesha utovu wa nidhamu. Hii ni kwa sababu jamii haikukubali wanawake kulewa.

Mkakati wa mkabala haukujidhihirisha wazi katika methali ya sita na ya saba. Methali ya nane imechukua mkabala wa kuwasawiri wanaume kama viumbe maasumu. Methali inawataja wanaume kama watu waliokamilika. Methali inasema kuwa hasira za wanaume hazidumu kama za wanawake. Wanawake huweka hasira katika mioyo yao kwa muda mrefu sana, huku mwanamume akichukua muda mfupi tu kutulia na

kutoa hasira moyoni mwake. Methali hii inawadunisha wanawake na kuwabagua. Sifa mbaya tu ndizo wanazopewa wanawake huku wanaume wakipewa zile nzuri. Wanawake wamebaguliwa katika methali hii kwa matumizi ya jina "*aka"*. Nomino hii ni jina la madharau la kuwarejelea wanawake walioolewa. Mwanamume amerejelewa kwa nomino yenye staha ya "*arumne"* inayomaanisha, wenye ujasiri. Kwa jumla, methali imechukua mkabala wa kuumeni. Methali hii pia imewasawiri wanawake kama watu dhaifu, wenye mioyo migumu isiojua kusamehe. Hasira humtoka binadamu baada ya kumsamehe aliyemkasirisha. Tumepewa taswira ya wanawake wasiojua kusamehe.

Methali ya tisa inamsawiri mwanamume kama mtu dhabiti katika mambo yake, anayeweza kuaminika na aliye na msimamo. Kwa upande mwingine, mwanamke amesawirriwa kama kigeugeu, asiyeaminika, asiyekuwa na msimamo na asiyetabirika. Methali inatuarifu kuwa mwanamume anayeshiriki wizi na mwanamume huishi kwa huzuni hadi yule mwanamke atakapokufa. Kwanza, mwanamume haamini kuwa yeye anaweza kufa kabla ya yule mwanamke. Methali inachukulia kuwa mwanamke ndiye atakayetangulia kufa. Pili, mwanamke anabaguliwa kwa kusawiriwa kama kigeugeu, asiyekuwa na msimamo na asiyeaminika. Mambo yanapomwendea mrama, mwanamke ataitoa siri bila kusita. Kwa jumla, methali imemsawiri mwanamke kama asiye na msimamo naye mwanamume kama aliye na msimamo dhabiti.

Methali ya kumi imemsawiri mwanamume kama mtu jasiri, anayeenda kuwinda usiku, huku bibi akisawiriwa kama mtumwa, ambaye hawezi kulala mpaka bwana yake atakaporejea kutoka mawindoni. Methali yatuarifu kwamba bibi ya msasi halali hadi mumewe atakaporejea kutoka usasini. Mkabala uliochukuliwa katika methali hii ni wa kumsawiri mwanamume kama mtu jasiri na mtawala, naye mwanamke anasawiriwa kama mtumwa. Huu ni mkabala wa kiume. Ilibidi mwanamke amngojee bwana yake hadi atakaporejea kutoka usasini usiku, hata ikiwa ni usiku wa manane.

Mkakati wa mkabala haujajidhihirisha katika methali ya kumi na moja. Methali ya kumi na mbili imechukua mkabala wa kuumeni. Methali inasema kuwa mzee ambaye hakubarikiwa na mtoto wa kiume hujifanyia shughuli zote kama vile kuwinda, kuchunga, ulinzi wa familia na kulinda mimea shambani. Jambo hili lilitokea kwa sababu jamii iliamini kuwa hakuna msaada wowote ambao mtoto wa kike anaweza toa kwa babake. Mtoto wa kike hakuchukuliwa kama mtoto. Katika ngano ya kipokomo

inayoitwa "*mtema kuni*", kulikuwa na mwanamume aliyeitwa Komara. Pamoja na bibi yake, walijaliwa kupata watoto wa kike pekee. Katika hadithi imeandikwa, "ndoa yao haikubarikiwa na watoto ila walizaa wasichana tupu". Ni wazi kutokana na mila za Wapokomo kuwa mtoto wa kike hakuhesabiwa kama mtoto. Hakupewa nafasi yoyote. Methali hii ya kumi na mbili imechukua mkabala wa kuumeni kwa kumtukuza mwanamume na kumdhalilisha mwanamke kiwango cha kutomtambua kabisa.

4.2.3.5 Mkakati wa Kufifiza

(Wodak (2001: 73) anasema kuwa mkakati wa kufifiza huchunguza iwapo matamko haya ya ubaguzi yalitolewa kimaksudi au kisadfa tu. Pia mkakati unachunguza kama uakisi huu ulikusudiwa hivyo au ulitokea bila kutarajiwa. Mtafiti katika kazi hii alichunguza tabia za wahusika, maumbo yao na vipi yanavyojenga namna wanavyosawiriwa. Methali ya kwanza ina mkakati wa kufifiza. Methali inasema kuwa hakuna jimbi wa mtamba mmoja. Nomino jimbi limetumiwa kurejelea mwanamume naye mtamba ni mwanamke. Matamko haya hayakutolewa kisiri. Yalitolewa kwa njia ya wazi na kwa maksudi, huku nomino jimbi/jogoo ikitumika kiubaguzi kumtukuza mwanamume. Mwanamume anapewa sifa ya kuwa jogoo, yaani aliye na uwezo akilinganishwa na mtamba yaani mwanamke. Methali inatuarifu kuwa wanaume wanapaswa kuoa bibi zaidi ya mmoja ili wamtumikie ipasavyo. Hii ni kusema kuwa mwaamume ndiye aliyestahili kufurahia ndoa wala sio mwanamke. Mwanamke alitumika tu kama chombo cha kumtimizia mumewe haja za kimwili na kumzalia watoto.

Mkakati wa kufifiza haujajidhihirisha wazi katika methali ya pili, lakini upo katika methali ya tatu. Methali inasema kuwa mtoto yule mwerevu humfurahisha baba yake, lakini yule mpumbavu humhuzunisha mamaye siku zote. Mwanamke hapa anapewa taswira ya kiumbe mjinga huku mwanamume akitukuzwa kwa werevu. Mtoto mwerevu anahuzishwa na baba yake ilhali yule mjinga anahusishwa na mamaye. Kufifiza kunajitokeza kwa jinsi mume anavyokwezwa huko mke akidharauliwa.

Dhana hii ya mtoto mwerevu kunasibishwa na baba yake katika jamii ya Agikuyu huenda inapigwa jeki na maandishi kutoka kitabu kitakatifu cha Biblia katika mithali 10:1;

"...Mwana mwenye hekima humfurahisha babaye; Bali mwana mpumbavu ni mzigo wa mamaye". Mwanamke amefifizwa kwa kuchorwa kama baradhuli.

Mkakati wa kufifiza haujajipanua wazi katika methali ya nne. Katika methali ya tano mkakati pia haujajidhihirisha. Methali ya sita, mkakati wa kufifiza unajitokeza pale mwanamume amechorwa kama kiongozi wa familia yake mwenye uwezo mkuu, huku mwanamke akiwa amepewa nafasi ya kuwa kama mtumishi au chombo. Methali inasema kuwa mwanamke aliyeolewa hana ruhusa kamwe kushiriki ngono na mwanamume mwingine yeyote isipokuwa bwanaye. Ingawa haya ni maadili mema, hakuna sheria inayomkataza mwanamume kushiriki ngono na mwanamke asiye mke wake. Jamii inapotoa sheria kwa mwanamke, kwa mwanamume inanyamaza ndi! Hivi ni kusema mwanamume ameachiwa uhuru wa kujiamulia atende au asitende. Matamko haya ya ubaguzi yalikusudiwa. Hayakutokea kwa sadfa.

Methali ya saba inatoa wazo kama hilo la methali ya sita. Methali inasema kuwa ngoma ya bibi ya mtu haichezewi wapita njia. Ufifizaji umetumika hapa ambapo neno "ngono" limepunguzwa makali kwa kuitwa *ngoma*, nayo nomino "wanaume" limerejelewa kama "wapita njia". Dhana ni ile ile tu ya kuwa bibi ya mtu aliruhusiwa kushiriki tendo la ndoa na bwana yake pekee. Kwa upande mwingine, bwana hajawekewa masharti yeyote. Wanaume wanapendelewa huku mwanamke akinyimwa uhuru wa kujiamulia. Huu ni ufififzaji na ubaguzi.

Methali ya nane inatuarifu kuwa wanaume hawaweki hasira moyoni kwa muda mrefu kama wanawake. Methali hii inawakweza wanaume kwa kuwapa sifa nzuri huku wanawake wakidunishwa kwa kupewa sifa mbaya ya kutosahau yaliyopita na kuganga yaliyomo na yajayo. Mwanamke anachorwa kwa njia ya uhasi naye mwanamume kwa njia ya uchanya. Mwanamke amefifizwa kwa kuchorwa kama mtu mwenye moyo mgumu usiojua kusamehe na kusahau. Matamko ya ubaguzi katika methali hii yalidhamiriwa hadharani. Mwanamke amefifizwa kwa kupewa sifa mbaya.

Methali ya tisa imemdunisha mwanamke sana na kumdharau kwa kiwango cha kwanza. Methali inasema kuwa mwanamume anayeshiriki wizi na mwanamke huishi kwa kihoro hadi yule mwanamke atakapofariki. Kulingana na methali hii, mwanamke anasemekana kuwa mtu asiyeweza kuweka siri kwa muda mrefu. Mwanamke amefifizwa kwa kuchorwa kama kiumbe dhaifu, kigeugeu na asiyeaminika. Matamko haya yamefanywa hadharani na kimaksudi. Mwanamume amepewasifa ya mtu mwenye moyo dhabiti, anayeaminika, anayeweza kuihifadhi siri kwa muda mrefu. Kufifiza kunajitokeza pale ambapo mwanamke anadunishwa naye mwanamume anakwezwa. Katika muktadha huu, mwanamume hajioni kama anayeweza kutangulia kufa kabla ya mwanamke. Mwanamume anajikweza na kuona kuwa atakayekubana na mauti kwanza ni mwanamke. Tunapewa taswira ya mwanamume aliye shujaa katika mambo yote.

Methali ya kumi inatuarifu kuwa bibi wa msasi halali usiku, bali hukesha hadi mumewe atakaporejea kutoka mawindoni. Ufifizaji unajitokeza pale mwanamke anaposawiriwa kama mtumwa, asiyekuwa na uhuru wake, ambaye lazima akeshe na hajui bwana atarejea saa ngapi. Mwanamke amebaguliwa na kusawiriwa kwa njia hasi. Mume naye kwa upande mwingine, amechorwa kama nguli, asiyekuwa na woga. Anaenda kuwinda usiku kwenye giza. Anaonekana akirejea nyumbani usiku sana, bila dalili zozote za woga.

Ufifizaji unajitokeza pale wanaume wanaposawiriwa kama mashujaa wanaofanya shughuli za hatari bila woga. Usiku kuna hatari nyingi kama vile kushambuliwa na wanyama wa pori. Wanaume wanatenda matendo ya kishujaa, huku wanawake wakitaka kuhuzishwa na kufaulu tu. Wanaume nao hupenda kusababisha kule kufaulu. Hii ni dhana ya kufifiza. Mwanamke katika methali ametajwa kwa njia hasi na ya dharau kwa kuitwa *“muka”,* jina ambalo si la heshima kumrejelea mwanamke aliyeolewa kuteua jina kama hilo lisilo na sitara kumtaja mwanamke ni mojawapo ya vipengele vya mkakati wa kufifiza.

Methali ya kumi na moja ilichunguzwa na mtafiti, lakini mkakati wa kufifiza haukupatikana. Methali ya kumi na mbili inatoa wazo kuwa mzee ambaye hakubarikiwa kupata mtoto wa kiume ndiye hujifanyia shughuli zote kwa vile jamii haikuwahesabu watoto wa kike na haikuwapa jukumu lolote. Ndoa bila mtoto wa kiume haikuheshimiwa na ilisemekana haina watoto, hata ikiwa ina wengi wa kike.

Mwanamume aliye katika ndoa kama hii alishauriwa aoe bibi mwingine atakayemzalia mtoto wa kiume. Huu ni ufifizaji. Mwanamke amedharauliwa kiasi cha kutothaminiwa katika jamii. Onyango (2007), akimnukuu Atheuser katika Janks & Ivaniks (1992:308) anasema tafiti nyingi kuhusu fasihi ya watoto zinamsawiri mwanamke kwa njia hasi. Mwanamume naye hupewa hadhi ya juu. Hii ndiyo sababu shirika la "Short Stories Across Africa" lilisisitiza kwamba ngano za watoto zinapoandikwa, idadi ya wahusika wa kike ni muhimu na kusawiriwa kwao kuzingatie misingi muhimu ya kimenke ya wakati huu.

4.2.4 Methali za Mkabala wa Kimaumbile.

Methali za mkabala wa kimaumbile ni zile zinazomtambulisha mwanamume kulingana na maumbile yake. Kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu ya Tuki (2004), maumbile ni tabia au umbo la asili la kiumbe; pia ni hulka. Methali zifuatazo sita ni zile zinazomtambulisha mwanamume kutokana na umbo lake, au tabia zake za asili. Umbo la mwili la mwanamume si sawa na la mwanamke. Mwili wa mwanamume huweza kustahimili magumu na hata huwa na nguvu kuliko mwili wa mwanamke. Hulka za wanaume pia ni tofauti zikilinganishwa na zile za wanawake. Methali hizo saba ni:-

1. *Kirema arume nikigariure*.
   Kinachowashinda wanaume huwa kimeshughulikiwa vilivyo.
2. *Nyama (Ngari) (Njamba) ndiriagwo ni wira*.
   Shujaa hauawi na kazi
3. *Njamba ti ikere*
   Kuwa shujaa si kuwa na mwili mnene.
4. *Hunyu ni umwe na arume.*
   Ni kawaida ya wanaume kuparara
5. Arume mari rwamba
   Miili ya wanaume hucheneta/washa
6. *Gutiri mundurume muka wa uria ungi.*
   Hakuna mwanmume aliyeolewa na mwanaume.
7. *Wiyumiririe wa kahii ti wa kairu.*
   Mwanamume jikaze,mtoto wa kiume si wa kike.

4.2.4.1. Mkakati wa Urejelezi

Mkakati wa urejelezi huchunguza urejelezi wa wahusika katika matini. Kinachoangaliwa ni majina ambayo wahusika wamepewa, namna walivyorejelewa kiisimu, iwapo kuna dhana yoyote ya ubaguzi wa kimaubile, kirangi, kihadhi au kikabila. Katika mkakati huu, tunajiuliza maswali kama vile,wahusika wamepewa majina gani? Majina haya yana maana gani? Ni sifa gani zinazoambatanishwa na majina haya? Mkakati huu pia humchunguza mhusika kama mwanajamii. Iwapo amepewa jina hasi, huenda anayerejelewa si yeye kama mtu binafsi, bali anawakilisha kundi au jamii anayotoka.

Methali ya kwanza inatujulisha ya kuwa jambo au tatizo lolote lile ambalo huwashinda wanaume huwa limeshughulikiwa kabisa. Methali hii inawarejelea wanaume kama "*Arume*" kumaanisha "wenye ujasiri". Nomino hii ndiyo hutumiwa kuwarejelea wanaume katika hali ya kuwatukuza. Wanarejelewa kwa njia chanya kwa kulimbikiziwa sifa ya ujasiri. Sifa ya ujasiri inatupa taswira ya mwanaume kuwa kiumbe asiyeogopa, anayekabiliana na hali zote, ngumu na hatari, kwa ujasiri. Jambo lolote lile, au tatizo lolote lile,linalowashinda wanaume, huwa limeshughulikiwa kwa mapana na marefu. Methali hii inamsawiri mwanamume kama asiyekata tamaa kwa urahisi, na anayejizatiti kuhakikisha amefaulu katika maazimio yake. Jamii inamsawiri mwanamume kama asiyeshindika. Mwanamume anahusishwa na kufaulu. Neno kushindwa halipatikani katika msamiati wa wanaume. Kwa kupewa sifa ya ujasiri, wanaume wanapendelewa, na huu ni ubaguzi. Hakuna mwanamume anayehusishwa na udhaifu. Kimaumbile, mwanamume anahusishwa na kusababisha mambo yafanyike na yafaulu. Kushindwa si kwa wanaume.

Methali ya tatu inatupa wazo kuwa mwanamume shujaa hajulikana kulingana na misuli yake. Mwanamume huenda hana tafu zinazoonekana kwa macho, lakini matendo yake ni ya yule mwenye tafu zinazoonekana. Methali hii inatujuza kuwa tusimhukumu mwanamume kulingana na umbo lake, bali tuangalie matendo. Methali hii inawapigia debe wanaume ambao umbo lao la mwili ni ndogo. Methali inatahadharisha kuwa huenda wale wanaume wasiokuwa na misuli ndio walio na utendakazi mkubwa kuliko wanaoonekana kuwa na misuli. Methali hii ina dhana ya ubaguzi wa kimaumbile. Tunatahadharishwa dhidi ya kuwabagua na kuwasawiri wanaume kwa misingi ya maumbile ya kimwili. Hii ni kwa sababu huenda

unayemdhania ndiye,siye.Umbo la mwili litakuhadaa. Methali hii inatoa kauli moja na ile inayosema utanashati wa mwanamume sio meno.

Katika methali ya nne, tunapata ujumbe kuwa ni kawaida ya wanaume kuparara. Mtu huparara kwa sababu ya kufanya kazi. Methali hii inatupa taswira ya mwanamume mwenye bidii kazini. Huyu ndiye hana nafasi ya kuketi, kuoga na kujipaka mafuta kwa sababu anatumia muda wake mwingi kazini. Hivyo, methali hii inamchora mwanamume kama mwenye bidii kazini na mkakamavu. Mwanamume pia amerejelewa kama "*arume"* yaani "wenye ujasiri". Wanaume sio waoga na pia hawaogopi kazi yoyote ile, iwe ngumu au ya hatari. Mwanamume ambaye kila wakati alionekana safi, asiyekuwa na hali ya kuparara, hakuchukuliwa kama mwanamume wa kawaida. Tabia za kuoga kila wakati na kuwa safi kila wakati ni tabia za wanawake. Hii haina maana kuwa wanaume ni wachafu, bali ina maana kuwa wakati mwingi mwanamume yuko kazini.

Methali ya tano inatuairifu kuwa miili ya wanaume hucheneta. Hii ina maana kuwa wanaume si watu wa kuchezewa. Wana uwezo wa kukuletea madhara. Methali hii huelekezwa kwa wanawake. Wanaambiwa kuwa wanapoingiliana na wanaume wajue kuwa miili yao hucheneta, yaani wana uwezo wa kusababisha madhara katika mwili wa mwanamke. Methali hii inawasawiri wanaume kama watu wasio na mzaha katika kazi yao. Anayetaka kuingiliana na wanaume awe tayari kwa lolote lile litakalotokea. Wanaume hapa wamepewa sifa chanya inayowasiri kama watu wasiokuwa na mzaha katika yote wanayotenda. Wao ni wakakamavu na dhabiti katika matendo yao.

Methali ya sita inatueleza kuwa hakuna mwanamume aliye bibi wa mwanamume mwingine. Methai hii ina maana kuwa wanaume ni mnyimi, hasa kwa mwanamume mwenzake. Si rahisi mwanamume kumsaidia mwanamume mwenzake. Ubahili huu unaonekana katika methali nyingine ya kikikuyu inayosema,

"*Matumbi ma njamba matituranaga*"

Mayai ya jogoo hayawezi kuangua kifaranga

Methali hii ina maana kuwa jogoo wawili au zaidi hawawezi kupata yai litakaloangua kifaranga. Aidha, wanaume wawili hawawezi kupata mtoto. Ili mtoto apatikane lazima kuwa na mwanamke na mwanamume. Mwanamume amerejelewa kama "*mundurume*" ambalo ni jina la heshima la mwanamuume lakini mwanamke anarejelewa kama

"*muka*". Huku mwanamume akirejelewa kwa njia chanya, mwanamke anarejewa kwa njia hasi. Huu ni ubaguzi wa kumdunisha mwanamke na kumkweza mwanamume methali hii inaelekezwa wanaume, ili mwanamume asimtegemee mwanamume mwingine kwa msaada. Methali inatupa taswira kuwa mwanamke ndiye anayestahili msaada kutoka kwa mwanamume. Mwanamke anachukuliwa kama asiyejiweza kivyake, lazima pawe na mwanamume wa kumuauni. Mwanamke amepewa taswira ya mtu dhaifu.

Maumbile ya mwanamume si sawa na ya mwanamke. Mungu aliumba jinsia hizi mbili kwa njia tofauti. Waliumbwa hivi kwamba jinsia moja huvutiwa na jinsia hiyo nyingine. Hivyo, wanaume wawili hawawezi kukaa pamoja katika hali ya ndoa, ni lazima pawe ni mwanamume na mwanamke. Hii ndio sababu wanaume wanaowaoa wanaume wenzao, na wanawake wanaowaoa wanawake wenzao huwa wamekiuka kaida za jamii. Usenge ni ukiushi kaida katika jamii nyingi za kiafrika. Ushoga ni matokeo ya usasaleo, mambo ambayo waafrika wanaiga kutoka kwa wazungu. Sio mambo yote tuliyoletewa na wazungu huwa na faida kwetu.

Methali ya sita inatuarifu kuwa mtoto wa kiume si sawa na mtoto wa kike. Utamaduni wa jamii ya wakikuyu haukumtambua mtoto wa kike kamwe. Hata walipozungumzia juu ya "mtoto" walimaanainsha wa kiume sio wa kike. Ndoa iliyobarikiwa na watoto wa kike pekee ilisemekana kuwa bado hawajabarikiwa na mtoto isipokuwa wasichana tu. Hata sherehe zilizofanywa baada ya mtoto wa kike na wa kiume kuzaliwa zilikuwa tofauti. Tohara nayo ilipashwa wavulana kwa njia tofauti na wasichana. Wakati wa kuoa na kuolewa, msichana hakuwa na uhuru wa kumchagua mchumba. Mvulana ndiye aliyepewa uhuru wa kumchagua mschana ampendaye. Hata baada ya kuolewa, msichana hakuwa na uwezo wa kumkataza bwanaye kuoa mke wa pili na hata wa tatu.

Ubaguzi wa kimenke unajitokeza wazi katika methali hii. Mtoto wa kiume anasawiriwa kama aliye na thamani kubwa akilinganishwa na wa kike. Familia iliyokuwa na watoto wa kiume, hata ikiwa ni mmoja iliheshimiwa. Ndoa ambayo haikubarikiwa na mtoto wa kiume ilisemekana kuwa haijakamilika na mume alihimizwa aoe mke mwingine atakayemzalia mtoto wa kiume atakayekuwa mrithi. Baada ya mzazi wa kiume kufariki, mama hakuruhusiwa na utamaduni kurithi mali ya mumewe. Hata watoto wasichana hawakurithi chochote. Ilibidi mtoto wa kiume wa nyumba hiyo, hata akiwa ndiye mdogo zaidi, ndiye aliyerithi mali yote ya babaye.

Akiwa hakuwa na mtoto wa kiume, basi yule mwanamume alisemekana kuwa amekufa bila mrithi. Huu ni ubaguzi wa kimenke.

4.2.4.2 Mkakati wa Nomino

Mkakati wa nomino una uwiano mkubwa na ule mkakati wa urejelezi. Mkakati huu huchunguza mielekeo inayoambatanishwa na wahusika, sifa hasi na chanya za lugha iliyotumika kuwaakisi wahusika. Pia mkakati huu huangalia kama kuna sifa au vipengele vya kitabia vinavyoambatanishwa na wahusika ambavyo vinaweza kuwa vinachangia katika uhasi au uchanya wao. Madhumuni makuu ya mkakati huu ni kuonyesha maana inayoambatanishwa na urejelezi fulani.

Methali ya kwanza inatujulisha kuwa kile kinachowashinda wanaume huwa kimeshughulikiwa vilivyo. Nomino "*arume*" limetumika kuwarejelea wanaume kwa njia chanya. Nomino hii ni jina la heshima la kuwarejelea wanaume. Wanaume wamerejelewa kwa mwelekeo chanya, inayowatambulisha kama watu jasiri na nguli. Mwanamume anapewa sifa ya kutoshindwa na chochote na kile kinachomshinda huonekana si cha kawaida. Mwanamume husawiriwa kama kiumbe mwenye uwezo mkuu, hekima na busara.

Methali ya pili inasema kuwa mwanamume shujaa hawezi kushindwa na kazi yoyote ile. Mwanamume katika methali hii amesawiriwa kama shujaa, sifa ambayo ni ya kumtukuza mwanamume. Pia,methali hii inatupa taswira ya mwanamume asiyewezwa na kazi yoyote ile, iwe ngumu au hatari. Methali hii huwa ni ya kuwahimiza wanaume wafanye kazi bila kukata tamaa, hata wakati kazi imekuwa ngumu. Jamii humhusisha mwanamume na kufaulu. Hivyo, mwanamume amedhamiriwa kufanya kazi ili kuikimu familia yake. Ni kazi ya mwanamume kuhakikisha kuwa familia yake imepata riziki kila siku. Methali hii huwahimiza wanaume wafanye kazi kwa bidii bila kukata tamaa.

Methali ya tatu inatuarifu kuwa mwanamume sio umbo la mwili bali ni matendo. Mwanamume aweza kuwa wa miraba minne lakini bure. Mwingine awe hana mwili mkubwa. Kwa kweli waswahili walisema, "usione wembamba wa reli, gari la moshi linapita. Methali hii inawaambatanisha wanaume na mielekeo chanya. Jamii inatahadharishwa dhidi ya kumhukumu mwanamume kwa misingi ya umbo la mwili,

bali waangalie matendo. Methali hii inamtambulisha mwanamume anayejiweza na shujaa.

Methali ya nne inatuarifu kuwa wanaume huwa wakati wote wameparara kwa sababu ya kazi. Methali hii inawasawiri wanaume kama watu wenye bidii kazini na wasio walegevu. Kule kuparara hutokana na aina ya kazi wanayoifanya wanaume. Ni kweli kuwa kazi za wanaume ni ngumu na nyingine ni za hatari. Mwanamume anatarajiwa kufanya kazi kwa bidii bila uzembe ili aweze kuikimu familia yake. Nafasi ya mwanamume ya kuoga, kujipaka mafuta na kupumzika ni nadra sana kupatikana. Mwelekeo ulioambatanishwa na wanaume katika methali hii ni chanya; wanaume wanachorwa kama wenye bidii na wenye matendo mithaki. Kuwarejelea wanaume kwa nomino "*arume*" ni kuwatukuza kwa vile neno hili lina maana ya "wenye ujasiri". Wanaume wote wanapewa sifa ya kuwa jasiri.

Methali ya tano inatujuza kuwa wanaume hucheneta, yaani ngozi yao hucheneta. Methali hii ina maana kuwa ukiwachezea wanaume watakudhuru. Methali hii huelekezwa wanawake, wanaotahadharishwa dhidi ya kuwachezea wanaume. Kwa kupewa sifa hii, wanaume wanasawiriwa kama viumbe wasiokuwa na mzaha katika yote watendayo. Ukuruba wa mwanamke na mwanamume huishia na mwanamke kuadhirika, hasa ikiwa atapata mimba na yule mwanamume akose kumuoa. Mwanamume amesawiriwa kwa njia ya kumtukuza na kwa mielekeo chanya.

Methali ya sita inatujuza kuwa hakuna mwanamume aliye bibi ya mwanamume mwingine. Mwelekeo unaoambatanishwa na wanaume katika methali hii ni chanya. Methali hii ina maana kuwa haiwezekani wanamume wawili waoane na wapate watoto. Dhana hii ya wanaume wawili kuoana ni dhana geni, ambayo imefika hapa Afrika kutoka ulaya. Ni dhana ambayo hata haikufikirika katika jamii za Afrika. Methali inatoa wazo la kwanza kuwa haiwezekani mwanamume kuoa mwanamume mwenzake. Huu ni Usenge, ambao ni mwiko katika utamaduni wetu. Ni mwiko hata kufikiria kuwa jambo hili linawezekana. Wazo la pili la methali hii ni kuwa mwanamume alidhamiriwa kumuoa mwanamke ili wapate watoto. Methali hii inapigwa muhuri na methali nyingine ya kikikuyu inayosema;

"*Matumbi ma njamba matituranaga.*"

"Mayai mawili ya kiume hayawezi kuungana kupata mtoto".

Methali hii inadhamiriwa kuwafikia wanaume wajue kuwa wa kuoa ni mwanamke sio mwanamume; nao wanawake walilengwa na methali hii wajue kuwa wanaume ndio watakaowaoa. Maumbile ya mwanamume ndiyo humfanya asioe mwanamume mwenzake.

Methali ya saba inatuambia kuwa mtoto wa kike si sawa na wa kiume. Mtoto wa kiume huthaminiwa sana kuliko yule wa kike. Methali hii inatupa mwelekeo hasi kwa mtoto wa kike na mwelekeo chanya kwa mtoto wa kiume. Utamaduni wa jamii ya wakikuyu una mwongozo kuhusu utambulisho wa mtoto wa kiume na yule amebaguliwa na kudhahilishwa,jambo ambalo jamii imelikubali liwe hivyo. Hii ni kwa sababu jamii ya wakikuyu hufuata mfumo wa T.Y.K. wote, wake kwa waume, wazee kwa vijana walikubali mwelekeo huu na hakuna aliyelalamika.

Mtoto wa kiume amerejelewa kama "*kahii*", nomino ambayo ni ya heshima ya kumrejelea mtoto wa kiume ambaye bado hajapashwa tohara. Pia, msichana amerejelewa kama "*kairitu"*. Nomino hii ni jina la heshima la kumrejelea mtoto mdogo wa kike ambaye hajafikisha umri wa kupashwa tohara au kuolewa. Mtoto wa kiume hutukuzwa sana na kutwazwa na utamaduni. Hii ni kwa sababu mtoto wa kiume ndiye anayetegemewa katika ulinzi wa jamii, wakati wa vita, na mwisho, ndiye mrithi wa mali yote ya familia.

4.2.4.3 Mkakati wa Ubishi

Mkakati huu wa ubishi hujihusisha na kufafanua jinsi ubaguzi unavyodhihirika katika matini teule. Swali ambalo tutajiuliza katika mkakati huu ni; Je, ni kupitia mbinu gani za mabishano ambapo watu maalum, au makundi ya jamii, hujaribu kuhalalisha ubaguzi, na kutetea unyanyasaji kwa wenzao? Mkakati hueleza jinsi ubaguzi unavyojitokeza katika matini teule.

Methali ya kwanza inatujuza kuwa chochote kile, au lolote lile, litakalowashinda wanaume huwa limeshughulikiwa ipasavyo. Wanaume hapa wanasawiriwa kama watu wenye uwezo mkubwa, na wasioshindwa kwa urahisi kutatua matatizo yanayowakumba au kukumba jamii kwa jumla, na iwapo kuna litakalowashinda basi huenda likawa si jambo la kawaida. Ubaguzi unadhihirika katika methali hii pale ambapo mwanamume ndiye anayesemekana kuwa hakuna linalomshinda kwa urahisi. Methali inawasawiri wanaume kama viumbe wasiokuwa na udhaifu, walio kamilika na

wenye uwezo. Kwa mwanamke ingawa hajatajwa hapa, ni wazi kuwa anasawiriwa kama kiumbe dhaifu, asiyekuwa na uwezo mwingi. Tunapata taswira ya mwanamume ambaye huendeleza mambo yote na kutatua matatizo yote ya jamii kwa jumla.

Methali ya pili inatujulisha ya kwamba mwanamume shujaa hawezi shindwa na kazi. Methali hii huelekezwa wanaume kuwatia motisha wasiogope kufanya kazi kwani kazi haiui mwanamume. Methali hii inawabagua wanawake kwa sababu haiwahusishi kamwe na kutoshindwa na kazi. Wanaume tu ndio wanaohimizwa kutoogopa kufanya kazi. Wanaume pia wanaonekana kupendelewa katika methali hii kwa kurejelewa kama "*njamba"* yaani shujaa. Hii ni kuwapa wanaume sifa na kuwatukuza. Wanawake wamebaguliwa kwa kuachwa nje wasiogope kufanya kazi.

Mkakati wa ubishi haujajidhihirisha vyema katika methali ya tatu. Methali ya nne inatupa wazo kuwa kwa sababu ya kazi wanayoifanya wanaume, wakati mwingi huwa wameparara. Hii ni kwa sababu mwanamume hufanya kazi kwa saa nyingi na hana muda mwingi wa kuoga na kujipaka mafuta. Mwanamume lazima afanye kazi muda mrefu ili aweze kuikimu familia yake. Methali hii inatupa dhana kuwa mwanamume aliyeparara ni yule mwenye bidii, na asiyeparara ni mzembe. Hapa tunaona pia wanawake wamebaguliwa kwa kutotajwa kama wenye bidii. Mwenye bidii ni mwanamume, na hasa aliyeparara kwa kufanya kazi kwa bidii. Methali hii pia inawafanyia wanaume kampeni hasa wale wasiokuwa na sura nzuri kwa kukosa kujiweka vizuri.

Mkakati wa ubishi pia haujajidhihirisha katika methali ya tano. Methali ya sita inatujuza kuwa hakuna mwanamume aliye bibi ya mwanamume mwingine. Methali hii ina maana kuwa mwanamume hawezi kumwoa mwanamume mwenzake awe mkewe. Methali hii huelekezwa wanaume wakitahadharishwa dhidi ya mwanamume kumwoa mwanamume mwenzake. Methali hii ilibuniwa miaka mingi sana iliyopita, na leo hii inatimilika. Kuna huu mfuno mpya kutoka magharibi ambapo wanaume wanaoa wanaume wenzao na wanaishi kama bwana na bibi. Jamii ya Wakikuyu, wakiongozwa na wazee wenye busara walikuwa wameliona jambo hili miaka mingi sana iliyopita, na ndiposa wakaibuni methali hii. Methali hii inawarejelea wanaume kwa njia chanya kwa kuwaita "*mundurume*", ambalo ni jina la heshima la mwanaume. Methali inaporejelea mwanamke, nomino "*muka*" inatumiwa, jina la dharau la kumrejelea

mwanamke aliyeolewa. Huu ni ubaguzi. Kuna nomino zenye sitara zinazoweza kutumiwa kuwarejelea wanawake walioolewa badala ya nomino ya dharau.

Methali ya saba inatujuza kuwa mtoto wa kiume na wa kike si sawa. Jamii inamthamini sana mtoto wa kiume na kumpuuza mtoto wa kike. Ubaguzi huu umejitokeza wazi na uko katika utamaduni wa jamii. Mtoto wa kiume huthaminiwa sana kwa sababu usalama/ulinzi wa jamii humtegemea mtoto wa kiume, ndiye mrithi wa mali ya familia, na ndiye tegemeo la jamii nzima katika nyanja ya uongozi na ushauri. Tangu kuzaliwa kwake, mtoto wa kiume hufurahia kupendelewa na kila kitu kuhusu mtoto wa kiume huchukuliwa kwa njia ya maana sana na jamii nzima. Katika kujamiishwa kwa watoto hawa wawili, wa kike na wa kiume hujua nafasi na majukumu yao katika jamii. Yule wa kike hugundua kuwa amepewa nafasi na majukumu duni yakilinganishwa na ya yule wa kiume. Yule wa kiume naye hugundua kuwa ametwazwa na kupewa nafasi ya mbele kuliko yule wa kike. Wote hukua na kunenepa wakijua hayo yote.

Ubaguzi huu dhidi ya mtoto wa kike hufanywa kwa njia ya wazi bila kufichwa na kila wote katika jamii wanajua na wamekubali iwe hivyo. Wanawake kwa jumla wamebaguliwa na kudhalilishwa. Mtoto msichana na mwanamke mzima wote huwa sawa mbele ya macho ya jamii. Hata katika jamii ya Wakalenjin, neno mtoto hurejelea wanawake na watoto. Mwanamke, licha ya umri mkubwa, mbele ya macho ya jamii ni dhalili, na kwa upande mwingine, mvulana, licha ya kuwa mtoto wa umri mdogo, mbele ya macho ya jamii, ndiye aliye na wazo litakalosaidia jamii.

4.2.4.4 Mkakati wa Mkabala

Katika mkakati huu, tunajiuliza ni katika mkabala upi ambapo urejelezi, upachikaji wa majina na mabishano unaoegemea katika kusawiri ubaguzi. Vitendo au uneni unaoonyesha ubaguzi hujadiliwa katika mkakati huu. Mkabala uliochukuliwa katika methali ya kwanza ni wa kumsawiri mwanamume kama nguli. Methali inasema kuwa kitakachowashinda wanaume huwa kimeshughulikiwa vilivyo. Hapa tunapata dhana kuwa hakuna linashowashinda wanaume, na iwapo kutakuwa na kitu cha kuwatatiza, huenda kiwe si kitu au jambo la kawaida. Tunapata taswira kuwa mwanamume ni shujaa, asiyeshindwa na lolote kwa urahisi. Wanaume wanaonekana kupendelewa na methali hii na hutambuliwa na jamii kama mashujaa au nguli. Hii ni sifa ya juu sana

kupewa wanaume. Mwanaume huchukuliwa ndiye mambo yote katika jamii. Kwanza, familia yake humtegemea kwa riziki ya kila siku, ahakikishie jamii yake usalama, atoe uongozi na mwongozo mwema wa jamii, aishauri jamii kwa njia inayofaa na ndiye mrithi na msimamizi wa mali ya jamii. Mwanaume hutumia lugha inayoonyesha ushujaa, matendo yao ni ya kishujaa. Majukumu aliyopewa mwanamume ni yale ya kumfanya aonekane na ajihisi kuwa bora na wa thamani kuliko mwanamke. Pombe inapotumiwa na wanaume huonyesha uume, lakini inapotumiwa na wanawake huonyesha utovu wa maadili. Huu ni ubaguzi.

Methali ya pili inatueleza kuwa mwanamume shujaa hawezi akafa kwa sababu ya kazi. Methali hii inachukua mkabala wa kumsawiri mwanamume kama mtu mwenye bidii na asiyekuwa mlegevu katika kazi. Methali pia inawatia shime wanaume kuwa wasilegee kazini kwani kufanya kazi hakutawadhuru kamwe, badala yake kutawaletea manufaa.Katika methali, mwanamume amerejelewa kama "*njamba"*, yaani shujaa. Hii ni sifa ya kumtukuza mwanamume. Mwanamume alitarajiwa asiwe goigoi. Awe na uwezo wa kukidhi mahitaji yote ya aila yake. Mwanamume lazima ajifunge kibwebwe kuitafutia aila yake riziki ya kila siku. Mwanaume anachukuliwa kama mhimili wa aila yake. Mwanamume lazima ajifunge kibwebwe kuitafutia aila yake riziki ya kila siku. Mwanamume anachukuliwa kama mhimili wa aila yake.

Mkakati wa mkabala haujajipanua katika methali ya tatu. Methali ya nne inatujuza kuwa ni kawaida ya wanaume kuparara kwa sababu ya kazi wanayofanya. Hapa tunapata dhana kuwa mwanaume wakati wote huwa kazini akiitafutia aila yake riziki. Muda wa kuoga, kuketi na kustarehe hakuna. Hivyo mwanamume wakati wote utampata kazini. Mkabala uliochukuliwa na methali hii ni wa kumsawiri mwanamume kama mtu mwenye bidii kazini, ambaye si mzembe na asiyekuwa na muda wa kupoteza. Hii ni sifa nzuri kwa wanaume. Kuna methali nyingine ya kikikuyu inayotia nguvu methali hii ya nne. Methali yenyewe inasema kuwa mguu ulio na umande si sawa na mguu ulio na jivu. Hii ina maana kuwa mguu wenye jivu ni wa mtu mzembe, anayeamka asubuhi na kuketi karibu na moto. Nao mguu wenye umande ni wa mtu ambaye aliamka asubuhi na mapema na kuenda kutafuta riziki. Huyu ni mtu mwenye bidii, asiye mvivu.

Methali ya tano inadai kuwa wanaume wana ngozi inayocheneta. Hii ina maana kuwa ukimchezea mwanaume atakuumiza. Methali hii ilielekezwa kwa wanawake. Ilidhamiria kuwaonya wanawake dhidi ya kuwachezea wanaume kwa sababu mwishowe wao ndio wataadhirika. Kwa mfano, mwanamume atamringa mwanamke na akose kumwoa. Pia, baada ya kumpa talaka mwanamke, mwanamume huwa na nafasi nzuri ya kupata bibi mwingine kulingana na mapenzi yake, wa rika yake au msichana mdogo. Lakini mwanamke akitalikiwa, itakuwa bahati nasibu kupata mume, na akipata, huenda ikawa ni mzee, au aliyeshindwa kujipanga maishani. Methali hii pia inachukua mkabala wa kuwasawiri wanaume kama watu hatari, ambao si vizuri Kuwachezea. Methali inawataka wanawake kuwaheshimu wanaume na kujichunga sana wanapoingiliana nao.

Methali ya sita inasema kuwa hakuna mwanamume aliye bibi ya mwanamume mwingine. Hii ina maana kuwa hakuna mwanamume anayetarajiwa kuwa chini ya mamlaka ya mwanamume mwingine. Methali hii imechukua mkabala wa kuwasawiri wanaume kama viongozi au watawala. Wanaume wanatakiwa kutawala au kuongoza. Katika kila jamii, wanaume ndio waliotwikwa jukumu la utawala. Pia kila aila huongozwa na mwanamume. Methali hii inatupa dhana kuwa wanaume ni watu wanaojipenda, ambao hawawezi kuwasaidia wanaume wenzao. Mwanamume ako tayari kutoa msaada wake kwa mwanamke lakini hawezi kumuauni mwanamume mwenzake. Hii ni kwa sababu wanaume wanajiamini kuwa wana uwezo, na wasiokuwa na uwezo ni wanawake.

Methali ya saba inasema kuwa mtoto wa kike si sawa na wa kiume. Mtoto wa kiume huchukuliwa kuwa bora zaidi kuliko yule wa kike. Tangu utotoni, watoto hulelewa na kujamiishwa wakijua kuwa yule mtoto wa kiume hudhaminiwa na jamii kuliko yule wa kike. Methali hii imechukua mkabala wa kuumeni, unaowatambua wanaume na kuwadhalilisha wanawake. Mwanamume amethaminiwa na jamii hivi kwamba mwanamke hana nafasi kamwe. Mali yote humilikiwa na mwanamume. Akiaga dunia, mrithi ni mwanamume bila kujali umri. Uongozi wa familia ni wa mwanamume. Atakayerithi uongozi pia ni mwanamume bila kujali umri. Ushauri na mwelekeo wa jamii upo katika mikono ya mwanamume.

4.2.4.5 Mkakati wa Kufifiza

Mkakati wa kufifiza huchunguza iwapo matamko ya ubaguzi yalitolewa kimaksudi au kusadfa tu. Pia, mkabala huu unachunguza kama uakisi huu ulikusudiwa hivyo au ulitokea bila kutarajiwa. Methali ya kwanza inasema kuwa kinachowashinda wanaume huwa kimeshughulikiwa. Hii ina maana kuwa wanaume wana uwezo mkubwa na si rahisi kushindwa kutenda au kutatua tatizo lolote. Methali hii ilidhamiria kuwatukuza wanaume kuwa wao ni mashujaa, wasioshindwa kwa urahisi. Wanaume wanahusishwa na kusababisha kufaulu ilihali wanawake wanapenda kuhuzishwa na kufaulu. Hii ni dhana ya kufifiza. Wanaume wamesawiriwa kama wanaotenda matendo ya kufaulu tu. Mwanamume ametwazwa. Hii ni mmojawapo ya vipengele vya mkakati wa kufifiza. Tunapomtukuza mwanamume kiwango hiki na kumlimbikizia sifa sufufu, ni dhana moja wao ya kumfifiza mwanamke.

Methali ya pili inasema mwanamume shujaa hawezi kufa kwa ajili ya kufanya kazi. Kwanza, kumrejelea mwanaume kama “shujaa” ni mbinu mojawapo ya ubaguzi wa kumtukuza mwanaume. Shujaa ni mtu ambaye ana moyo dhabiti aliye na uwezo wa kuyakabili mambo, hata kama ni ya hatari. Ni mtu jasiri, nguli na nyamaume. Mwanamume kupewa sifa hizi zote ni kumtukuza sana, na hivyo kumfifiza mwanamke. Methali hii imeelekezwa wanaume, kuwapa motisha wasiogope kufanya kazi, kwani wao ndio tegemeo kuu la jamii. Jamii huwategemea wanaume kutekeleza majukumu mengi ikiwemo kutoa usalama wa jamii na riziki ya kila siku. Matamko katika methali hii ni ya wazi na yalidhamiriwa. Hivyo, mkakati wa kufifiza ni wazi katika methali hii.

Katika methali ya tatu, tunajuzwwa kwamba kwa mwanamume shujaa, usimwangalie umbo, bali uangalie vitendo. Hii ina maana kuwa wanaume shujaa wanajulikana kutokana na vitendo vyao wala si kwa umbo la mwili wao. Methali hii ilielekezwa wanaume na wanawake, wasiwe wakiwahukumu wanaume kulingana na umbo la mwili bali waangalie matendo ya mwanamume. Methali hii inawafanyia wanaume kampeni na kuwapigia debe hasa wale wenye miili midogo, wasije wakadharauliwa na wanaume wenzao au wanawake. Hii ni dhana ya kuwapendelea wanaume. Wanaume huwekwa mbele wakati wote. Hii ni dhana ya kufifiza kwa upande wa wanawake.

Methali ya nne inatujuza kuwa ni kawaida ya wanaume kuparara. Hii ina maana kuwa wanaume ni watu wenye bidii ambao hutumia muda wao mwingi wakifanya kazi. Methali hii huelekezwa wanawake wasije wakaangalia usafi kwa mwanamume. Mwanamume ana muda mfupi sana wa kuoga na kustarehe. Wanawake ndio wanaelekezwa methali hii wakiambiwa kuwa wasiangalie jinsi mwanamume anavyoonekana kwa nje, bali waangalie kile mwanamume alicho nacho. Sawa na methali ya tatu, methali hii inawapigia wanaume debe kwa wanawake, kuonyesha kuwa mwanamume ni mtu mwenye bidii, aliye kazini kwa muda mwingi akitafuta riziki. Ni kweli hata leo, kuna wanawake wengi ambao hukaa nyumbani na kuwangojea waume zao walete chumo la siku. Ni nadra kumpata mwanamume anakaa nyumbani naye bibi ndiye aliyetoka kutafuta chumo.

Mkakati wa kufifiza haujajitokeza wazi katika methali ya tano. Methali ya sita inasema kuwa hakuna mwanamume aliye bibi ya mwanamume mwingine. Hii ina maana kuwa si sawa mwanamume kuwa chini ya mamlaka ya mwanamume mwingine. Mwanamume amepewa taswira ya kuwa ndiye kiongozi na mwenye mamlaka. Hii ni dhana ya ufifizaji. Jamii ya wakikuyu ilitoa mwongozo ulioonyesha kuwa watakaoongoza na kutawala ni wanaume na sio wanamwake. Hii ni kwa sababu jamii inaongozwa na taasubi ya kiume. Mwanamke pia anafifizwa kwa kurejelewa kwa jina la dharau sana, na huu ni ufififzaji. Matamko hayo yanafanywa hadharani na kwa maksudi.

Methali ya saba inasema kuwa mtoto wa kike si sawa na yule wa kiume. Matamshi yamefanywa kwa uwazi bila kuficha,hadharani na kwa maksudi. Huu ni ufifizaji. Mtoto wa kike amefifizwa huku yule wa kiume akitukuzwa. Jamii ya wakikuyu, kama zilivyo jamii nyiyngi za kiafrika zinazofuata mfumo wa kuumeni au itikadi ya T.Y.K, humthamini mtoto wa kiume sana kuliko yule wa kike. Jamii nyingi hazisitambui ndoa ambazo hasina mtoto wa kiume. Katika ndoa kama hizi, mwanamume hushauriwa kuoa mke wa pili atakayemzalia mtoto wa kiume. Hii ni kwa sababu mtoto wa kiume ndiye mriithi wa mali yote ya familia na pia yeye ndiye hutwaa uongozi baada ya baba kufariki. Mama na watoto wa kike kawaida hawarithi chochote. Kwa upande wa uongozi, wote huwa chini ya uongozi wa mtoto wa kiume, bila kujali umri wake. Hii ni hali ya juu sana ya kumfifiza mwanamke. Jamii nyingi humchukua mama na watoto wa kike wote kuwa sawa. Hii ni tashtiti. Hivyo, mtoto wa kiume hujua tangu akiwa

mdogo kuwa atarithi mali na uongozi. Hivyo atakapokuwa mkubwa, huwa amepata umilisi wa mambo haya kwa sababu jamii huwa imemwandaa vyema na pia baba yake humfundisha siku nenda siku rudi.

4.2.5 Methali za Mkabala wa Kisaikolojia

Kulingana na kamusi ya Kiswahili sanifu ya TUKI (2004), saikolojia ni elimu inayohusiana na ufahamu na utendaji kazi wa nafsia au akili ya mwanadamu. Kuna methali kadhaa katika lugha ya kikikuyu zinazohusiana na ufahamu na utendakazi wa nafsia wa mwanamume, zinazomtambulisha mwanamume kwa njia ya kumtukuza, kamuenzi na kumsawiri kama kiumbe maasumu, nguli na asiyeshindwa na lolote. Jamii ya wakikikuyu ina utamaduni ambao umemweka mwanamume mbele sana. Umempa mwanamume sehemu ya juu sana hivi kwamba hawezi kulinganishwa na mwanamke. Ufahamu huu umewaingia wanajamii wote, wake kwa waume na wamekubaliana na hali ilivyo. Methali saba zifuatazo ndizo humtambulisha mwanamume katika jamii ya wakikuyu katika mkabala wa kisaikolojia.

1. *Anake ni cienyu cia Ngai*
   Barobaro wana nguvu za kiungu
2. *Mundurume ni Ngai ya keri*
   Mwanamume ni mungu wa pili
3. *Mwana ndetagia ithe nyama*
   Mtoto haitishi baba yake nyama
4. *Thutha wa arume nduoyagwo ruoya*
   Palipopitia wazee hupati chochote
5. *Nyau nguru inyuaga iria.*
   Paka akizeeka hunywa maziwa.
6. *Arume hau niho turi*
   Wanaume hapo tulipo ndipo tunapostahili
7. *Kuhoya kwa arume ni maitho*
   Wanaume huomba kwa kutumia macho sio mdomo.

4.2.5.1 Mkakati wa Urejelezi

Mkakati huu wa urejelezi huchunguza urejelezi wa wahusika katika matini.Kinachoangaliwa hapa ni majina waliyopewa wahusika na namna walivyorejelewa kiisimu. Pia mkakati huu huchunguza iwapo kuna dhana yoyote ya ubaguzi wa kimaumbile, kirangi, kihadhi au kikabila. Tunajiuliza, Je, wahusika wamepewa majina yepi? Yana maana gani? Majina haya yanaambatanishwa na sifa gani? Mhusika huchunguzwa kama mwanajamii. Ikiwa amepewa jina lenye maana hasi, basi huenda anayerejelewa si yeye kama mtu binafsi, bali anatumiwa kuwakilisha kundi zima katika jamii anayotoka.

Mtafiti aligundua kuwa mkakati wa urejezi umejipambanua katika methali ya kwanza. Methali inasema kuwa barobaro wana nguvu za kiungu. Hii ni kwa sababu barobaro ndilo kundi katika jamii ya wakikuyu waliotarajiwa kuwa na nguvu zaidi kuliko kundi jingine lolote, wawe jasiri na shujaa, na hivyo walipewa jukumu la kulinda jamii dhidi ya uvamizi wowote kutoka kwa mahasidi wao. Usalama uliwekwa katika mikono ya barobaro hao. Barobaro hao wamerejelewa kama "*Anake*, jina la heshima la kumrejelea mvulana aliyebaleghe, amepashwa tohara, lakini bado hajaoa. Kwa kuwa Mungu ndiye mwenye nguvu zote na anayetulinda dhidi ya maafa yote, barobaro hawa wanapewa sifa ya kuwa na nguvu, karibu na za Mungu, na usalama wa jamii huwa mikononi mwao. Barobaro hawa wamesawiriwa kwa njia chanya na kupewa sifa za juu sana za kuwaweka wa pili kutoka kwa Mungu. Kuna dhana ya ubaguzi wa kimaumbile inayojitokeza. Mwanamume kwa sababu ya maumbile yake kuwekwa wa pili kutoka kwa Mungu ni kumpendelea sana. Amepewa sifa za kumtukuza, zinazoonyesha yuko karibu sana na Mungu kuliko mwanamke.

Methali ya pili ina uwiano mkubwa sana na ile ya kwanza. Methali inasema kuwa mwanamume ni Mungu wa pili. Methali hii imerewarejelea wanaume kwa njia chanya kwa kuwaita "*mundurume"*. Jina hili ni nomino ya heshima ya kumrejelea mwanamume katika utamaduni wa mkikuyu. Mwanamume amepewa sifa zote zinazoandamana na jina mwanamume. Pia, methali inapodai kuwa mwanamume ni Mungu wa pili, inampa mwanamume nafasi ya juu sana katika jamii ya kumweka wa pili kutoka kwa Mungu. Jamii inamuenzi mwanamume kiasi kwamba karibu wamtoshanishe na Mungu. Hii ni kwa sababu mwanamume ndiye anayetarajiwa kuyatekeleza yale majukumu muhimu sana katika jamii kama vile usalama, riziki,

uongozi, ushauri na uelekezi wa jamii kwa jumla. Kwa kufanya hivyo, mwanamke anafifizwa kwa kuonekana mnyonge na kupewa majukumu duni. Inaonekana kuwa anamtegemea mwanamume ili aishi. Mwanaume anatukuzwa na kupewa uwezo unaopewa nafasi ya pili kutoka kwa kudura ya mwenyezi Mungu. Huu ni ubaguzi wa kimenke. Mwanamke anabaguliwa kwa kusawiriwa kama kiumbe dhaifu ambaye lazima amtegemee mwanamume kwa mambo yote.

Methali ya tatu inasema kuwa si kawaida ya mtoto kuitisha baba yake nyama. Hii ina maana kuwa kuna zile ishara au dalili atakazoziona baba na ajue mwanaye anatamani nyama. Pia, kuna maneno atakayotumia mtoto, yatakayomfanya baba ajue kuwa mwanaye anahitaji nyama. Methali hii inaenda sambamba na ile ya Kiswahili inayosema "*dalili ya mvua ni mawingu*", na nyingine ya kikikuyu inayosema, "*mundu mugi ndari mihere ya uhoro,"(*Mtu mwerevu hutambua mambo kwa urahisi). Methali hii imerejelea mtoto kama "*mwana.*" Nomino hii inamaanisha mtoto. Ni jina la heshima na la staha kumrejelea mtoto. Jina hili "*mwana",*limetumika kumrejelea mtoto wa kiume tu sio wa kike. Kulingana na utamaduni wa jamii ya wakikuyu, (na hata jamii nyingine za kiafrika), jina mwana lilitumiwa kurejelea mtoto wa kiume. Mtoto wa kike aliitwa "mtoto wa kike". Katika hadithi ya kipokomo, inayoitwa "*mtema kuni*," kulikuwa na mwanamume aliyejulikana kama komora. Pamoja na bibi yake, walibarikiwa kupata watoto wa kike pekee Katika hadithi imeandikwa, "*Hawakubarikiwa na watoto ila walizaa wasichana watupu*". Hii ni kumaanisha jamii ya Wapokomo ilichukulia "mtoto" ni wa kiume wala si wa kike, sawa na jamii ya wakikuyu.

Baba amerejelewa kama "*ithe*". Jina hili ni nomino ya heshima la kumrejelea baba ya mtu. Mwanamume na mwana wamesawiriwa kwa njia chanya.Methali inasema baba hatangojea mpaka mwanawe amwitishe nyama. Kwa yale maneno mtoto atatumie au zile dalili utakazoziona baba, utambidi amchinjie mwanawe kondoo au mbuzi, au aende mawindo akatafute nyama. Mtoto wa kiume anaonekana kuenziwa sana na jamii ya wakikuyu. Anatunzwa na kuheshimiwa kuanzia utotoni hadi uzeeni. Mtoto wa kike anabaguliwa kwa kutotambuliwa kama "mwana". Tamthilia ya wingu jeusi ya Chache Nyaigoti Chacha (1987), mke anashtumiwa kuwa amezaa "majanajike tu". Huu ni urejelezi wa madharau kwa watoto wa kike. Huu ni ubaguzi wa kimenke. Mtoto wa kike anabaguliwa kwa sababu ya jinsia yake.

Methali ya nne inatujuza ya kuwa wanachofanya wanaume, wanafanya kwa ukamilifu bila kuacha doa lolote. Yaani wanafanya mambo yao kwa makini na busara hivi kwamba hukutokei dosari lolote. Methali imewarejelea wanaume kama "*arume*", iliyo na maana ya "wenye ujasiri". Mwanamume amesawiriwa kama mwenye ujasiri wa kutenda mambo na kukabiliana na yale yote yatakayotokea. Huu ni usawiri chanya. Mwanamume anapendelewa na kupewa sifa nzuri. Methali inapodai kuwa walichofanya wazee hakupatikani makosa, au tatizo walilotatua halipatikani kasoro, ni kuwapa wanaume sifa wasisostahili. Kwa sababu mwanamume ni binadamu ambaye anaweza kukosea. Utamaduni wa mkikuyu humchukulia mwanamume kama asiye wa kawaida. Mwanamke atafanya kosa lakini mwanamume hakosei. Wanawake wanabaguliwa huku wanaume wakipewa sifa na kutukuzwa.

Methali ya tano inatujulisha ya kuwa paka akizeeka hunywa maziwa. Hii ni kwa sababu hana uwezo wa kuwinda panya kwa sababu ya umri. Methali hii ni fumbo kuu, ambalo likifumbuliwa lina maana kuwa mwanamume akizeeka, anahitaji wasichana wadogo kumtimizia haja za kimwili. Methali hii inaonyesha jinsi wanaume wanavyojipenda na kuyajali maslahi yao wenyewe. Hakuna methali ya kuyajali maslahi kama haya kwa wanawake. Kwa kuwarejelea wanaume kama paka, huu ni urejelezi chanya kwa sababu paka ni myama wa nyumbani. Paka ni myama mdogo wa jamii ya chui. Chui ni mnyama anayeogopwa, aliye na sifa za ujasiri na uhodari. Chui hula nyama. Paka kwa upande mwingine huishi nyumbani pamoja na binadamu. Ingawa yeye hula panya, anajulikana kwa sifa ya usafi. Anapenda kuishi kwenye mazingira safi. Hii ndiyo sababu ya kumlinganisha mwanamume na paka, aliye na sifa nzuri.

Methali hii ilitungwa kwa minajili ya kulinda mwanamume na mahitaji yake ya kimwili anapozeeka. Mwanamke hakutiliwa maanani. Huu ni ubaguzi. Ubaguzi wa kijinsia. Mwanamke anatumika hapa kama chombo cha kumtimizia mwanamume haja zake na kumfurahisha. Isitoshe, wanawake wanaotakiwa kuwatumbuiza na kuwachangamsha hawa wazee ni wale wa umri mdogo, walio na damu moto. Huu ni ubinafsi kwa wanaume.

Methali ya sita inasema kuwa wanaume wameshikilia sehemu yao na wako sawa. Hii ina maana kuwa wanaume wanajihisi wanautawala ulimwengu na kila kitu kilicho ulimwenguni wakiwemo wanawake. Methali hii ni ya usasa. Marejeleo ya wanaume kama "*arume"* iliyo na maana ya "wenye ujasiri" ni chanya, yanayoonyesha jinsi mwanamume anavyotambuliwa katika utamaduni wa mkikuyu. Mwanamume anajihisi ako sawa katika nafasi anayoshikilia katika jamii. Ametosheka na majukumu anayotekeleza katika jamii. Ni kinaya kwa methali hii kudai hivi ilhali leo hii kuna wanaume wengi wameshindwa kukidhi mahitaji ya familia zao. Hii ni kutokana na hali ya kiuchumi kupanda sana na wanaume wengi kujingiza katika ulevi wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.

Methali ya saba inasema kuwa wanaume hutumia macho kuomba wala si maneno. Methali hiii ina maana kuwa wanaume si kawaida yao kutumia mdomo kudai wanachotaka, bali hutumia macho na anayehusika atajua au atagundua kile mwanamume anachotaka. Kwa mfano, wanaume wanapoalikwa kwa karamu na mmoja wao, wataketi sebuleni kitako wakisubiri mwenyeji awaletee kinyaji. Hawatadhubuti kuitisha, bali macho yao yataelezea yote. Hapa, wanaume wamerejelewa kwa njia chanya kwa nomino "*arume"* inayomaanisha "wenye ujasiri". Hii ni sifa nzuri kwa wanaume. Wanaume wanapendelewa.

4.2.5.2. Mkakati wa Nomino

Mkakati huu una ulingano mkubwa na mkakati wa urejelezi . Mkakati huu huchunguza mielekeo inayoambatanishwa na wahusika, sifa hasi na chanya za lugha zinazowaakisi wahusika. Mkakati wa nomino hudhamiria kuonyesha maana inayoambatanishwa na urejelezi fulani. Katika mkakati huu, mtafiti atachunguza iwapo kuna sifa au vipengele vya kitabia vilivyoambatanishwa na wahusika katika methali vinavyochangia uhasi au uchanya wao.

Mkakati wa nomino unajidhihirisha wazi katika methali ya kwanza. Methali inatujuza kuwa barobaro wana nguvu za kiungu. Methali hii inawatukuza barobaro kwa hali ya juu sana kiasi cha kulinganisha nguvu za barobaro na zile za Mungu. Kurejelea hawa barobaro kuwa na nguvu nyingi ni kuwatukuza na kuwasawiri kwa njia chanya. Hii ni sifa ya hali ya juu sana wanayopewa barobaro. Kuwarejelea kwa nomino "*Anake"* pia ni kuwapa heshima kamili. Nomino hii "*Anake"* ni jina la heshima la kuwarejelea

wavulana wakubwa ambao tayari wamepatana na kisu cha ngariba lakini bado hawajaoa. Hawa barobaro kupewa sifa ya nguvu zao kuwa karibu sawa na za Mungu ni kuwatunuku sifa sufufu ambazo kwa hakika hawastahili. Methali hii inatuonyesha jinsi jamii ya wakikuyu ilivyowatambulisha wanaume na kuwastahi. Wanaume wamepewa nafasi ya kwanza kabisa katika jamii. Nomino "*Anake"* (barobaro) imetumika kujumuisha wanaume wote na kuwatukuza katika ujumla huo. Nomino Mungu, ni nomino ya kidini iliyo na maana ya mwenye kuumba ulimwengu na vyote vilivyomo ndani yake.

Methali ya pili inakaribiana sana na ile ya kwanza. Methali inasema kuwa mwanamume ni Mungu wa pili. Kumweka mwanamume nafasi ya pili kutoka kwa Mungu ni kumtukuza na kumuenzi mwanamume sana. Utamaduni wa jamii ya wakikuyu umemweka mwanamume sehemu ya juu sana. Mwanamume amerejelewa kwa njia chanya kwa nomino ya "*mundurume"*, yaani mwenye ujasiri. Jamii inamwona mwanamume kama Mungu wa pili kwa sababu ya majukumu na nafasi za mwanamume katika jamii. Mwanamume ndiye mwenye kuiongoza na kuishauri jamii. Mwanamume ndiye mrithi wa mali ya jamii. Majukumu yale yote muhimu yametwikwa mwanamume. Hii ndiyo sababu ya kumwona mwanamume kama Mungu wa pili.

Methali ya tatu inatuarifu kuwa mtoto haitishi baba yake nyama. Methali hii ina maana kuwa baba hujua mahitaji ya mtoto wake hata kabla mtoto hajayataja mahitaji yale kwake. Hii methali inamsawiri mwanamume kama kiumbe chenye hekima, hivi kwamba anaelewa mahitaji ya mwanawe. Tena, methali inamsawiri mwanamume kama mtu inayewajibika katika majukumu yake. Nomino "*mwana"* ikiwa na maana ya mtoto wa kiume pekee wala si wa kike. Jamii ilimbagua kabisa mtoto wa kike hivi kwamba wanapozungumzia kuhusu "mtoto", huyu ni wa kiume wala si wa kike. Isitoshe, mtoto wa kike alipohitaji chochote, hangemwitisha babake. Alimwendea mama yake. Mtoto wa kike hata hangepata nafasi ya kukutana na baba yake kwa urahisi kwa sababu wakati wa mchana, anamsaidia mama kazi za nyumbani, naye baba, ameondoka pengine kwenda malishoni pamoja na watoto wa kiume. Ifikapo jioni baba anakaa "*Thingira*" wakiwa na watoto wake wa kiume naye mama yuko jikoni pamoja na watoto wa kike. Ilikuwa nadra baba kukutana na mtoto wa kike.

Mkakati wa nomino haujajidhihirisha wazi katika methali ya nne. Methali ya tano inatuarifu kuwa paka akizeeka hunywa maziwa. Hili ni fumbo, linalomaanisha kuwa mwanamume akizeeka, hutamani kufanya mapenzi na wasichana wadogo, walio na damu moto, ili wachangamke na wajihisi kurudiwa na ujana. Nomino iliyotumika hapa ya paka inawanasibisha wanaume na paka. Paka ni mnyama wa nyumbani, anayependa kuishi katika mazingira safi. Paka ni mnyama mstaarabu anayeishi kwa nyumba pamoja na binadamu. Mwanamume analinganishwa na huyu paka kwa sababu yeye pia ni mstaarabu sana. Maziwa hapa yametumika kijazanda kumaanisha ngono. Mwanamume akizeeka huwa bado ana hamu na uwezo wa kufanya mapenzi. Kwa upande mwingine, mwanamke akizeeka huwa anapoteza kabisa hamu ya kufanya mapenzi. Hali hii ndiyo humlazimu mwanamume kutafuta njia mbadala wa kujitosheleza hamu yake ya kimwili. Methali hii ina mwelekeo chanya kuhusu wanaume. Wanaume wanapendelewa kwa kupewa sifa nzuri. Jamii iliwapendelea wanaume na ndiyo sababu ya kubuni methali kuonyesha kuwa mwanamume anatakiwa kuwa na starehe maisha yake yote hadi kufa.

Methali ya sita inatuarifu kuwa wanaume wametosheka na sehemu walioshikilia katika jamii na pia wametosheka na nafasi na majukumu yao. Methali hii inatumika kama majigambo kwa wanaume, wanaodai kuwa wako jadidi katika sehemu walioshikilia katika jamii. Kwa kurejelewa kama *"Arume*", iliyo na maana ya wenye ujasiri, wanaume wamerejelewa kwa njia chanya. Msimamao huu wa wanaume kujihisi kuwa wako imara katika jamii yao huonyesha ya kuwa wanafurahia nafasi hiyo yao katika jamii. Utamaduni wa mkikuyu umependelea sana mwanamume na kumnyanyasa mwanamke kwa njia nyingi. Mkakati wa nomino haujajidhihirisha wazi katika methali ya saba.

4.2.5.3. Mkakati wa Ubishi

Mkakati huu hufafanua ubaguzi unavyodhihirika katika matini iliyochaguliwa. Swali ambalo mtafiti atajibidiisha kujibu ni, je, ni kupitia mbinu gani za mabishano ambapo watu maalumu au makundi ya kijamii hujaribu kuhalalisha ubaguzi na kutetea unyanyasaji kwa wenzao? Pia, makakti huu hufafanua sababu za kuwepo kwa ubaguzi huu. Mkakati huu utamsaidia mtafiti kudondoa vipengele mahsusi vya lugha vitakavyodhibitisha uwepo wa ubaguzi.

Methali ya kwanza inatujulisha kuwa barobaro ni sehemu moja ya Mungu. Methali hii ina maana kuwa wakikuyu kama jamii wanatambua barobaro kama walio wa pili kutoka kwa Mungu kwa njia mbalimbali. Jamii hutegemea kulindwa na barobaro dhidi ya mahasidi wao. Barobaro pia ndio hutegemewa katika kuiendeleza jamii na kurithi mali yake. Kwa kuwa ndio wenye nguvu na ari, kundi hili la jamii ni nguzo kuu la jamii ya wakikuyu. Ubaguzi wa kimenke unadhihirika wazi katika methali hii. Wanaume wamepewa sifa ya juu sana ya kuwekwa wa pili kutoka kwa Mungu. Wanaume hutetea ubaguzi huu dhidi ya wanawake na kuonyesha kuwa hivyo ndivyo inavyotakiwa kuwa.

Kupitia kwa asasi mbalimbali za jamii, wanaume wameuendeleza ubaguzi huu na kuonyesha kuwa ni haki yao kuwa na uwezo kama ule na kuchukua nafasi na majukumu waliotunukiwa na jamii. Kumlinganisha mwanamume na sifa za mwenyezi Mungu ni kumpa hadhi ya juu sana asiyostahili. Mwanamume anasawiri kwa njia chanya kama mwenye nguvu nyingi yaani shujaa. Taswira inayojitokeza hapa ni kuwa mwanamume ndiye mambo yote katika jamii, na bila mwanamume basi hakuna jamii.

Methali ya pili inadai kuwa mwanamume ni Mungu wa pili. Maelezo ya methali hii yanalingana sambamba na yale ya methali ya kwanza. Mwanamume amesawiriwa kwa njia chanya kama Mungu wa pili. Hii ina maana kuwa mwanamume hutekeleza majukumu mengi na ya maana karibu na yale yanayotekelezwa na Mungu. Huu ni ubaguzi wa kiwango cha kwanza dhidi ya mwanamke.

Methali ya tatu inatujulisha kuwa mtoto haitishi baba yake nyama. Matumizi ya jina "*Mtoto"* katika methali hii inamrejelea mtoto wa kiume wala si wa kike. Mkakati wa ubishi unajitokeza wazi hapa kwa kumbagua mtoto wa kike. Jamii nyingi za kiafika pia huchukulia mtoto ni yule wa kiume tu. Jamii nyingi za kiafrika zinashikilia taasubi ya kiume, na wanaamini kuwa lolote lifanywalo na mwanamume ni zuri – hata liwe ni uchawi. "Nyama" imetumiwa katika methali hii kusimamia mambo yote mazuri. Hii ina maana kuwa baba atamtimizia mwanaye mambo yote mazuri bila ya kungoja mwanaye aitishe. Methali hii inamsawiri mwanamume kama mtu anayewajibika sana na asiyengojea kukumbushwa majukumu yake. Anatimiza majukumu yake kwa wakati bila kukumbushwa. Baba mzazi anayafahamu mahitaji ya mwanaye yote na anayatimiza bila kungojea kukumbushwa na yeyote. Mwanamume hapa anaonekana kupewa sifa nyingi sana zinazofanya aonekane kuwa anapendelewa na jamii.

Methali ya nne inasema kuwa palipopitia wazee, hupati chochote. Hii ina maana kuwa wazee wanafanya mambo yao kwa makini sana hivi kwamba hakuna dosari lolote ambalo hutokea. Ikiwa ni mazungumzo, wanayafanya kwa kina. Ikiwa ni kutatua mambo yaliyomo, wanatatua kwa njia mwafaka. Katika kusuluhisha mambo yote ya kijamii, wazee huchukua mstari wa mbele na mambo yote huwa shwari. Wanaume wanonekana kupendelewa na lolote wafanyalo huchukuliwa kuwa zuri na linalofaa. Wanawake hawapewi nafasi ya kulikosoa au kulipa changamoto. Huu ni ubaguzi dhidi ya wanawake, ambao wanaonewa na kuonekana kana kwamba hawana mchango wowote katika maamuzi ya kijamii. Yote wameachiwa wanaume.

Methali ya tano inasema kuwa paka mzee hunyua maziwa. Methali hii ni fumbo inayomaanisha kuwa mwanamume akizeeka, huoa msichana mdogo amtumikie na kumhudumia. Hivyo, paka ametumika kijazanda kusimamia mwanamume nayo maziwa yametumika kijazanda kusimamia msichana wa umri mdogo. Mkakati wa ubishi unajitokeza pale ambapo mwanamume anaonekana kupendelewa dhidi ya mwanamke. Maslahi ya mwanamume yanashughulikiwa hadi akiwa mzee, bila kujali hisia za yule msichana mdogo anayeolewa na yule mzee. Bila shaka yule mzee wa umri mkuu hatamtimizie yule msichana haja zake za kimwili kikamilifu, na hivyo huenda msichana yule akatafuta barobaro wa kumtosheleza kimwili kikamilifu.

Kwa upande mwingine, yule msichana akifanya hivyo, huu utaitwa uasherati. Atalaaniwa na jamii nzima na kuitwa Malaya. Huu ni uonevu na ubaguzi kwa wanawake. Mwanamume akifanya mapenzi nje ya ndoa, huo si umalaya, lakini mwanamke akifanya mapenzi nje ya ndoa, Jamii nzima humkemea na kumwita Malaya, kosa ambalo huonekana vigumu kusamehewa. Hii ni kwa sababu Jamii ya wakikuyu huongozwa na taasubi ya kiume na kuamini kuwa lolote lifanywalo na wanaume ni zuri hata liwe uchawi au uzinzi. Jamii yenye mfumo wa kuumeni inamkweza mume na kumpa nafasi ya kwanza, ilhali mwanamke anasawiriwa kuwa chini ya mume, na ya kwamba aliumbwa kumtumikia mume. Huu ni ubaguzi wa kimenke.

Methali ya sita inasema kuwa wanaume wametosheka na sehemu wanayoshikilia katika jamii na wanasema kuwa hapo ndipo wanapostahili.Wanaume wamechukua nafasi na majukumu muhimu katika jamii hasa majukumu ambayo yameshikilia uchumi, siasa na ulinzi.Wanaume wana nguvu na uwezo mkubwa dhidi ya

wanawake .Wanawake hubaguliwa kwa kupewa majukumu yasiyokuwa na umuhimu mkubwa kama vile kupika, kuosha nguo, kutema kuni, kuchota maji na kadhalika. Majukumu haya hayana umuhimu wowote kisiasa au kiuchumi. Jamii imehalalisha ubaguzi dhidi ya wanawake kwa kuwapa majukumu duni katika jamii. Wanawake walinyanyaswa kwa sababu taasisi za kijamii zilifuata taasubi ya kiume inayowapendelea wanaume na kuwanyanyasa wanawake.

Methali ya mwisho inasema kuwa wanaume hutumia macho yao kuomba si mdomo.Hapa wanaume wanachukulia kwa njia ya kipekee.Wanachukuliwa kama viumbe wasio wa kawaida, walio na uwezo wa kipekee. Wanapohitaji kitu, hawatumii mdomo bali hutumia macho yao tu. Mwanaume huchukulia kuwa kuomba ni kuonyesha ukosefu au udhaifu fulani. Hivyo anapohitaji kitu, hatatumia mdomo wake kuomba asionekane kuwa na udhaifu ,bali atatumia macho yake kukiangalia anachohitaji au kumwangalia yule anayehitaji msaada kutoka kwake. Methali hii hasa huelekezwa wanawake, wanaohitajika kuyajua mahitaji ya waume zao bila kungojea mume kuitisha. Huu ni unyanyasaji wa wanawake. Mwanamume anapewa nafasi ya mbele sana hivi kwamba hata anapohitaji, mwanamke amtimizie mahitaji yale kabla ya mume kuyataja. Huu ni ubaguzi wa kimenke. Ubaguzi unajitokeza pale mwanamume anataka atimiziwe mahitaji yake na mwanamke bila yeye (mwanamume) kuyataja mahitaji yake. Huu ni unyanyasaji wa hali ya juu.

4.2.5.4 Mkakati wa Mkabala

Mkakati wa mkabala huchuguza ni katika mkabala upi ambapo urejelezi,upachikaji wa majina na mabishano unaoegemea katika kusawiri ubaguzi. Mkakati huu hutoa maelezo, ufafanuzi na utoaji wa idhibati za ubaguzi. Vitendo au uneni unaoonyesha ubaguzi hujadiliwa katika mkakati huu. Majukumu ya wake na wanaume yalijadiliwa katika utafiti huu.

Methali ya kwanza inasema kuwa barobaro ni sehemu ya Mungu, au wana nguvu za kiungu. Methali hii inatuonyesha umuhimu wa barobaro katika ulinzi wa jamii. Wao ndio waliotumika wakati wa vita. Walilinda jamii ipasavyo. Pia jamii ilitegemea barobaro katika kuiendeleza jamii baada ya kuoa. Isitoshe, mali ya jamii ilirithiwa na barobaro hao. Majukumu haya yote na ya muhimu yaliifanya jamii kuwachukulia barobaro kuwa na umuhimu mkubwa na kuwapa nafasi ya pili kutoka kwa Mungu.

Methali hii imechukua mkabala wa kumsawiri mwanamume kama kiumbe cha kipekee, karibu na malaika, asiye na mawaa. Mkabala uliochukuliwa na methali hii ni wa kiumeni, yaani mwanamume amepewa nafasi ya juu akilinganishwa na mwanamke. Hii ni kwa sababu wanaume wana majukumu mengi na ya muhimu kuliko ya wanawake.

Methali ya pili inatuambia kuwa mwanamume ni Mungu wa pili. Hii ina maana kuwa majukumu yanayotekelezwa na wanaume katika jamii ni mengi na ya umuhimu hivi kwamba anaonekana kama mungu wa pili. Maelezo ya methali hii ni sawa na ya methali ya kwanza. Methali hii imechukua mkabala wa kumsawiri mwanamume kama mungu wa pili. Huu ni mkabala wa kuumeni, mkabala unaompa mwanaume nafasi ya kwanza na ya juu sana akilinganisha na mwanamke. Mkabala huu umesawiri ubaguzi wa mwanamke kwa kuwapa wanaume nafasi ya pili kutoka kwa Mungu.

Methali ya tatu inasema kuwa mtoto haitishi baba yake nyama hapa tuelewe kuwa mtoto aliyerejelewa hapa ni wa kiume si yule wa kike hapa inachukuliwa kuwa baba anajua mahitaji yote ya mwanaye na hatangoja hadi mtoto amwitishe bali humtimizia yote bila kukawia. Methali hii inamsawiri mwanaume kama mtu aliye na hekima sana na busara anayejua mahitaji ya mtoto wake. Mkabala uliochukuliwa na methali hii ni wa kuumeni unaomtambua mwanaume kwa njia chanya,bila kumjali mwanamke. Jina “mtoto” limetumika kimaksudi kumrejelea mtoto wa kiume wala si yule wa kike. Huu ni ubaguzi.

Mkakati wa mkabala haujajipambanua katika methali ya nne. Methali ya tano inasema kuwa paka akizeeka hunywa maziwa. Paka na maziwa zimetumika kijazanda kumaanisha mzee /mwanaume na msichana mtawalia. Mwanaume akizeeka huhitaji msichana wa kuoa ili amtumikie na kumchangamsha . Mkabala uliochukuliwa na methali hii ni wa kumsawiri mwanamume kama nguli. Mwanaume anachukuliwa kuwa shujaa hivi kwamba hata baada ya kuzeeka bado ana hamu na uwezo wa kufanya mapenzi. Isitoshe, wakati huu amezeeka, anahitazji msichana mwenye damu moto itakayomchangamsha katika umri wake mkuu. Huu ni ubaguzi wa kimemke , ambapo mwanaume anajipenda , atimiziwe haja zake za kimwili kikamilifu bila kujali hisia za mwenzake, ambaye umri wake ni mdogo .

Methali ya sita inatujulisha kuwa wanaume wako sawa na wametosheka na nafsi walioshikilia katika jamii. Hii ni methali ya kisasa, inaoonyesha hisia za wanaume kutokana na nafasi walioshikilia katika jamii na majukumu wanayotekeleza. Methali hii imechukua mkabala wa kumsawiri mwanaume kama nguli, anayejifaragua kuwa ametosheka na mamlaka na majukumu aliyonayo. Mwanaume hapa anaonyesha ubinafsi. Kujinaki huku kunaashiria kuwa anaufahamu kuwa amemnyanyasa mwanamke. Huu ni ubaguzi wa kimenke. Mwanamume,katika jamii ya wakikuyu anajua kuwa hakuna mashindano kati yake na mwanamke. Utamaduni wa mkikuyu umemweka mwanaume mbele sana na kumnyanyasa na kumdunisha mwanamke. Jamii ya wakikuyu imeshikilia kwa dhati taasubi ya kiume , inayoamini kuwa wanaume ni aula akilinganishwa na mwanamke .

Methali ya saba inatujuza kuwa wanaume huomba wanachohitaji kwa kutumia macho. Kwa kujinaki kwao, wanaume hawataki kuonekana kama wanaohitaji msaada, hivyo hawatatumia midomo yao kuomba , bali watanyamaza, na kuangalia tu, huku yule mwenye kutoa huo msaada akitarajiwa kujua mahitaji ya mwanaume. Methali hii imechukua mkabala wa kumsawiri mwanaume kama nguli, anayehudumiwa na kutumikiwa akiwa katika starehe zake. Huu ni mkabala wa kuumeni, pale ambapo mwanaume anajihisi kuwa yeye ni mwanaume kweli, anayejihitaji kutumikiwa bila yeye kutumika. Wanaotarajiwa kuwatumikia wanaume katika methali hii ni wanawake. Huu ni ubaguzi. Wanawake wanachukuliwa kama watumwa. Wanatarajiwa kuwatumikiwa wanaume na kuwafurahisha . Wanaume wamesawiriwa kwa njia chanya.

4.2.5.5 Mkakati wa Kufifiza

Wodak (2001:73) anasema mkakati wa kufifiza huangalia iwapo matamko ya ubaguzi yalitolewa kimaksudi au yalitokea kisadfa tu. Na je, uakisi huu ulikusudiwa hivyo au ulitokea bila kutarajiwa? Mtafiti aliangalia matamshi na maumbo ya wahusika na jinsi na vipi yanavyojenga jinsi wanavyosawiriwa.Mkakati wa kufifiza unajitokeza wazi katika methali ya kwanza. Methali inasema kuwa barobaro ni sehemu moja ya Mungu. Methali hii inatupa wazo kuwa jamii inawaamini barobaro sana, nayale majukumu waliyopewa barobaro yanawafanya waonekana kama Mungu wa pili.Majukumu hayo ni pamoja na kuimarisha usalama wa jamii nzima, kuendeleza jamii kupitia kwa uzazi, kurithi mali yajamii pamoja na majukumu mengine.

Kule kuwaweka barobaro mbele sana na kuwatukuza ni mojawapo wa vipengele vya mkakati wa kufifiza.Barobaro wanasawiriwa kwa njia chanya na kupewa sifa nzuri ya kuwa karibu na Mungu.Mwanamume ametwazwa sana. Matamko haya yaliotolewa hadharani na kimaksudi, yakiwa na lengo la kumtukuza mwanamume na kumdhalilisha mwanamke. Hii ni mbinu mojawapo ya kumfifiza mwanamke. Wanaume katika methali hii wamesawiriwa kama mashujaa, wanaotenda matendo ya kishujaa.

Methali ya pili ina uhusiano mkubwa sana na ile ya kwanza. Methali inasema kuwa mwanamume niMungu wa pili. Hii ina maana kuwa mwanamume anatekeleza majukumu mengi sana naya muhimu katika jamii kiasi cha kuonekana kuwa wa pili kutoka kwa Mungu. Methali hii, kama ile ya kwanza, inamtukuza mwanamume sana. Mwanamume amesawiriwa kwa njia chanya. Kumweka mwanaume kama Mungu wa pili kuna maana kuwa mwanamume hutenda yote na hufanikiwa katika yote aliyotenda. Hivyo mwanamume anahusishwa na kusababisha kufaulu. Hiki ni kipengele kimoja cha mkakati wa kufifiza.

Mkakati wa kufifiza hayajajitokeeza wazi katika methali yya tatu. Methali ya nne inatujuza kuwa pale wazee wameepitia, huwezi kupata chochote. Methali hii ina maana kuwa lolote lililotendwa na wazee huwa halina dosari. wazee hapa ikiwa na maana ya wanaume wa umri mkubwa, sio akina mama. wanaume wanapewa sifa ya kuwa na umakinifu katika mambo yao yote wanayofanya. Hii ni sifa chanya. Matamko haya yanatolewa kwa njia ya wazi na hakuna sadfa yoyote. Yalikusudiwa vile yalivyo. Hii ni dhana ya kufifiza. Mambo yote yanayofanywa na wanaume huwa shwari bila kasoro.

Methali ya tano inatujulisha kuwa paka mzee hunywa maziwa.Mkakati wa kufifiza unajitokeza wazi katika methali hii. Kwanza, mwanamume analinganishwa na paka. Paka ni myama anayeishi na binadamu kwa nyumba. Ingawa paka hula panya, ana sifa ya kupenda kuishi kwenye mazingira safi nayeye mwenyewe ni safi. Paka anapenda maziwa. Nomino maziwa imetumika kijazanda hapa kusimamia wasichana wadogo. Kwa hivyo, methali ina maana kuwa mwanamume akizeeka, hupenda kuoa msichana wa umri mdogo atakayemburudisha na kumchangamsha kwa damu yake iliyo moto. Mwanamume hapa anatukuza naye mwanamke akitwezwa kwa kulinganishwa namaziwayanayonywewa napaka. Pia, mwanamke amesawiri kama chombo

kinachotumika kumstarehesha mwanamume aliyezeeka na kumfanya ajihisi kijana. Hapa mwanamke amefifizwa kwa kutumiwa kama chombo cha kuleta starehe kwa mwanamume. Wanawake wanadunishwa. Wanaonekana kama wao wana jukumu la kumtumikia mwanamume. Huu ni ubaguzi, unyanyasaji na madharau kwa wanawake.

Methali ya sita inasema kuwa wanaume wametosheka na nafasi wanayoshikilia katika jamii. Methali hii imetumika kama majigambo ya wanaume kwa vile walivyo napale walipo. Wanaume wameshikilia nyadhifa muhimu katika jamii. Wao ndio wanaoongoza kisiasa, wameshikilia sekta ya uchumi,ulinzi uko katika himaya yao na uongozi wa jamii kwa jumla. Mwanamume anapojigamba hivi,anamdhalilisha mwanamke na kumfanya aonekane asiye na lolote wala chochote. Hii ni dhana ya kufifiza. Mwanamke amefifizwa kiwango kwamba hana lolote la kujidai nalo. Ubaguzi huu, unaojitokeza wazi unadhihirisha kuwa mambo haya yanasemwa na kutendwa hadharani bila kufichwa.Yanasemwa na kutendwa kama yalivyokusudiwa mwanamke anapewa nafasi kidogo sana na duni katika jamii.

Majukumu anayotarajiwa kutekeleza ni yale yasiyokuwa na umuhimu wowote kisiasa na kiuchumi. Majukumu yao ni kama vile kuteka maji, kupika chakula, kuosha nguo, kutafuta kuni na pia kuwatunza watoto na bwana yake. Ni wazi hapa kuwa mwanamke amefifizwa kwa kupewa majukumu yasiokuwa na umuhimu mkubwa katika jamii. Mwanamke anafifizwa kwa kuchorwa kama mtumwa, anayemtumikia mwanamume.

Mkakati wa kufifiza haujajipambanua kwa njia ya wazi katika methali ya saba.

4.3 Majukumu ya Kimenke

Majukumu ya Kimenke ni, “mienendo na mielekeo inayodhaniwa kuwa sahihi kwa waume na wake katika utamaduni fulani… kadhalika, jinsi mtu anavyojisawiri kibinafsi kama mwanamke au mwanaume. (Golombok na Fivush 1994:3). Kipury (1983), anasema kuwa tabia za watu hujengeka kwenye misingi ya utamaduni wao. Kwa hivyo, mila na miiko ya jamii huzingatiwa katika kutambua mienendo na tabia hizo. Maadili mbalilimbali ya kijamii ndiyo huongoza mienendo ya watu.

Dhana ya majukumu ya Kimenke kwa msichana katika mazingira halisi ni kuwa awe mwanamke, aolewe, apate watoto, aitunze familia yake na amtumikie bwana yake. Majukumu ya mvulana wa kawaida ni akifika utu uzima, ajiunge na jeshi, aoe, awe

na familia, ailinde jamii na kuiongoza. (Trousdole, 1995). Kwa mujibu wa Tuyizere (2007) majukumu ya Kimenke ni mienendo inayohusiana na kazi katika muktadha wa kijamii. Majukumu yamegawanywa kulingana na jinsia na yana mipaka maalum. Mafunzo mengi ya kidini yanaendeleza na kusisitiza majukumu ya asili ya Kimenke. Taasisi nyingi za kidini zinapinga mabadiliko yoyote. Kwa mfano, kanisa katoliki haliwatawazi wanawake kuwa makasisi, nalo kanisa la kiangilikana huwatawaza wanawake kuwa maaskofu, ingawa wachache sana. Hakuna Mufti wa kike katika dini ya Kiislamu. (Uk. 125).

Utafiti huu ulibainisha majukumu ya Kimenke yaliyojitokeza katika methali arubaini na tano za jamii ya wakikuyu zilizoteuliwa kwa misingi ya matumizi ya lugha. Mtafiti aliyabainisha majukumu ya Kimenke kulingana na mtazamo wa kiuchumi, kisiasa na kijamii.

4.3.1. Kiuchumi

Utafiti huu uliangazia majukumu ya kiuchumi yaliyofanywa na watu wa jinsia fulani ili kujikumu kimaisha. Katika methali arubaini na tano zilizoteuliwa na kuchanganuliwa, wanaume ndio waliotwikwa jukumu la kuikimu familia kwa hali na mali. Katika methali "*Njamba Ndiriagwo ni wira*(mwanamume shujaa hawezi kufa kwa sababu ya kufanya kazi), mwanamume yuko tayari kufanya kazi yoyote ile, hata iwe ya sulubu muradi tu aikidhi familia yake. Methali nyingine '*muka wa mwathi ahingaga na kuguru etereire kigurumuki oke" (*bibi wa msasi halali hadi mumewe atakaporejelea kutoka mawindoni) inatuonyesha kuwa kazi ya usasi ilifanywa usiku . Mwanaume alihatarisha maisha yake kwenda kuwinda usiku ,katika msitu wenye wanyama hatari , ili aitafute familia yake riziki. Bibi hayuko tayari kuandamana na bwanaye , bali hukaa kwa nyumba akisubiri bwanaye hadi atakaporejelea.

"Uthaka wa mundurume ti magego"

(Utanashati wa mwanamume si meno), ni methali inayotujulisha kuwa mwanamume hajishughulishi mno kujipodoa na kujirembesha bali yeye hujishughulisha na kutafuta riziki ya familia ya kwa hali zote. Amali alizozifanya mwanamume hazingempa nafasi ya kustarehe nakujirembesha kwa mavazi. Amali hizo ni kama vile kuwinda, kuchunga wanyama, kuilinda familia na pia uchongaji. Kazi hizi zilimhitaji mwanamume kuzitekeleza kila siku. Methali hii ilitumika kuwaonya wanajamii hasa

wanaume wasihalalishe uzembe, na kushughulikia mambo yasiyoleta faida katika maisha. Bidii kazini ilienziwa sana. Wenye bidii hasa wanaume waliheshimiwa na walishauriwa waoe mabibi wengi. Msichana mzembe hakupata mchumba. Nyanja ya kiuchumi inadhihirisha tofauti ya kimajukumu kwa uwazi kwa mujibu wa kijinsia. Wanaume walitengewa yale majukumu yaliyohitaji nguvu nyingi na yaliyokuwa hatari. Mwanamke hakuruhusiwa kazi za wanaume kama vile, uhunzi na usasi zilipewa umuhimu mkubwa kuliko kazi za wanawake.

4.3.2 Kisiasa/Uongozi/Utawala

Katika utafiti huu, nomino "uongozi" imetumika kumaanisha utawala wa kisisasa katika jamii.Katika methali zilizoteuliwa na kuchanganuliwa, uongozi wa kisiasa kwa jumla ulidhihirika. Uongozi ulisambazwa miongoni mwa wake na waume.Uongozi niile hali ya mtu kupewa fursa na mamlaka kudhibiti uongozi wake kwa wale walio chini yake. Katika methali zilizoteuliwa, ni wazi kuwa uongozi ulipewa mwanamume. Methali nyingi zilimtambulisha mwanamume kama jasiri au shujaa, ni hii ni sifa ya kiongozi.Nomino nyingi zilizotumika kumrejelea mwanamume zilimrejelea kwa njia chanya na kumsawiri kama mwenye uwezo mwingi dhidi ya mwanamke. Methali nyingi zilionyesha taswira ya mwanamume shupavu, jasiri na mwenye hekima.Baadhi ya nomino zilimrejelea mwanamume kwa njia ya kumpa sifa na kumtukuza ni kama vile:-

Arume– wenye ujasiri
Mundurume –mwenye ujasiri
Njamba –shujaa
Athuri – wenye kupambanua
Muthuri – anayepambanua
Mwanake – barobaro

Nomino hizi zilitumika kumrejelea mwanamume kwa njia chanya. Zinaonyesha nafasi aliyoshikilia mwanamume katika jamii.Mwanamume ndiye aliyetwikwa jukumu la kuongoza jamii. Kila familia iliongoza na baba, na iwapo baba angetupa mkono wa buriani, uongozi ulitwaliwa na mtoto mkubwa wa kiume katika ile aila. Ilikuwa balaa mwanamume kufa kabla hajapata mtoto wa kiume kwa sababu atakosa wa kurithi mali na utawala. Kwa upande mwingine, mwanamke aliwachiwa utawala wa watoto hasa wale wa kike na pia uongozi pale jikoni. Ndiye aliyeamua apikie familia yake nini na

apike vipi. Uongozi wa mwanamke ulikuwa wa kiwango cha chini sana. Yeye alishugulikia upishi, usafi wa nyumba, kuchota maji na kutafuta kuni.

Kwa kuwa jamii ya wakikuyu ilizingatia itikadi ya kuumeni, mamlaka, madaraka na uwezo wote zilikuwa chini ya baraza la wazee. Uongozi ulipokezwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Vizazi viwili vilivyojulikana sana kwa umaarafu wake ni kizazi cha *Maina* na kizazi cha *Irungu*. Ungozi uligawanywa katika ngazi, kuanzia ile ya chini hadi ile ya juu kabisa kama ifuatayo:

a) Halmashauri ya jamii (*ndundu ya mucii*)
b) Halimashauri ya kijiji *(kiama gia itura*)
c) Halimashauri la eneo (*kiama kia rugongo*)
d) Halmashauri ya wanachama kutoka halmashauri za maeneo tofauti.

Wavulana wa miaka kati ya ishirini hadi arubaini waliunda baraza lavijana (*njama ya ita*) iliyokuwa na jukumu la kuilinda jamii dhidi ya uvamizi wowote kutoka kwa mahasimu.

Methali iliyogonga ndipo umuhimu wa mabaraza haya ya wazee ni isemayo:-

> "*Ita ritari ndundu rihuragwo na njuguma imwe"*
> (watu wasiokuwa pamoja hutawanyika kwa urahisi).

Methali hii ni sambamba na ile ya Kiswahili inayosema, "umoja ni nguvu utengano ni udhaifu." Katika halimashauri hizi, wazee ndiowaliochukua nafasi zote. Wanawake walihusishwa kwa nadra sana.

4.3.3 Maisha ya Ndoa

Jukumu la ndoa lafaa liwahusishe mke na mume. Katika methali zilizoteuliwa mwanamume amechukua uongozi katika uhusiano wa ndoa. Methali nyingi zimeonyesha kuwa bibi (mwanamke) hakuwa na mamlaka yoyote katika ndoa. Wakati wa kumchagua mchumba, mwanamume ndiye aliyepewa nafasi ya kumchagua msichana ampendaye amwoe. Msichana hakupewa nafasi ya kuchagua. Baada ya kuolewa, mwanamume ndiye aliyekuwa na uwezo na mamlaka ya kuamua kama ataoa bibi mwingine au wengine ama abaki na huyo mmoja. Methali zifuatazo zinadhihilisha ukweli huu:-

- *Mundu wa muka umwe ni tuhu wa kanyenje.*

(Mwanamke wa bibimmoja ni bure kabisa)

- *Mwanake wina indo ndoihanaga*

(barobaro mwenye mali hapotezi muda kuwatongoza wasichana – wao hujileta tu).

- *Gutiri njamba ya mwera umwe*.
  (hakuna jimbi wa mtamba mmoja).
- *Nyau nguru inuaga iria*
  (paka akizeeka hunywa maziwa).

Mwanamume ambaye hakufanikiwa kupata mtoto wa kiume na bibi yake alishauriwa aoe bibi mwingine atakayemzalia mtoto wa kiume kwa sababu ya urithi. Hata ingawa kukosa mtoto wakiume huwa ni udhaifu wa mwanamume kisayansi, mwanamke ndiye akiyerundikiwa lawama hii na ndiposa mume alikubaliwa kumchukua bibi wa pili au hata wa tatu. Mwanamume alimmiliki mwanamke alyemwoajinsi anamilikimali yake.Kile kitendo cha kulipa mahali kilimpa mwanamume hisia kuwa "amemnunua" yule bibi na sasa ni mali yake. Kwa vile mwanamume ndiye humwoa mwanamke na kumchukua nyumbani kwake, hivyo kuoa ni mmojawapo ya majukumu ya kiume.

4.3.4 Ulezi/Ujamiishaji

Utafiti huu ulishibitisha kuwa jukumu la ulezi lilikuwa la mwanawake. Wanawake walisawiriwa kama walezi wa familia huku mwanamume akiwa kiongozi wa familia. Mwanamke alihakikisha usafi nyumbani, upishi kwa familia, kuzaa na kuwalea watoto.Kamusi ya Kiswahili sanifu (Tuki:2004:207) inasema ulezi ni ule heli ya kumtunza na kumfundisha mtoto mpaka akue."

Baada ya kuzaliwa mtoto, mama alichukua jukumu la kumyonyesha na kumtunza, na ia kumhudumia kwa hali zote. Mama ndiye aliyetekeleza jukumu la ujamiishaji ili kuwatayarisha kwa majukumu yao ya ukubwani. Ikiwa mtoto ni wa kiume, afikapo miaka saba au mika nane hii, basi hapo ndipo alipoanza kuandamana na baba yake kwenda mahungani. Jukumu la baba la kumfundisha lilianza hapo. Baba alimfunza kuhusu utamaduni wajamii kwa jumla, uhunzi, usasi, uchongaji na majukumu mengine yaliyokuwa ya wanaume. Hivyo, kazi ya ulenzi ilifanwa na wazazi wote wawili, baba na mama. Jamii nzima kwa jumla ilihusika katika kuwalea watoto. Watoto walichukuliwa kama mali ya jamii na hivyo kila mwanajamii alitarajiwa kutekeleza jukumu lake la ulezi. Baadhi ya methali zinazoonyesha jukumu la ulenzi ni: -

- *Mari guoya mainukagira nyina, nao mari urume mainukagira ithe.*
  (Wenye uwoga huenda nyumbani kwa mama, nao wenye ujasiri huenda nyumbani kwa baba). Methali hii inaonyesha vijana wakati wa vita, washinde au wasishinde, wawe na ujasiri au woga, mwishowe huenda nyumbani kwa walezi wao.
- *Mwana wina ithe ndanyuaga muma*
  (mtoto aliye na baba yake hali kiapo).

Methali hii inaonyesha kuwa baba atamsimamia mtoto wake kwa sababu ndiye mzzi wake.

4.3.5 Ulinzi

Jukumu la kulinda jamii lilikuwa la wanaume. Wanawake walipewayale majukumu mapesi kama vile kupika, kuchota maji, kutema kuni na upishi, majukumu yasio ya hatari. Mwanamume, kwa sababu ya ujasiri wake aliyachukua majukuumu yale mazito naya hatari, kama vile ulinzi. Jamii ilitegemea barobaro na ndio waltoa ulinzi kwa jamii nzima kupitia hamashauri yao ya vijana *(njama ya ita)* "*ita*" ninomino ya kikikuyu iliyo na maana ya "kikosi cha askari au wanajeshi:. Baadhi ya methali zinazodhihirisha jukumu la ulinzi ni:

- *Anake ni cienyu cia Ngai*.
  (Barobaro ni sehemu ya Mungu)
- *Mundurume ni Ngai ya keri*
  (mwanamume ni Mungu wa pili)
- *Mari guoya mainukagira nyina, mariurume mainukagira ithe*.
  (wenye uwoga hurejea nyumbani kwa mama yao, nao wenye ujasiri hurejea nyumbani kwa baba yao).
- *Kahii ni ithigi ria mucii*.
  (mvulana ni ngao ya familia).
- *Njamba ni ithaga ria rika.*
  (mwanamume jasiri ni tunu kwa rika lake).

Utafiti huu ulidhibitisha kuwa wanaume walipewa jukumu la ulinzi kwa sababu ya sifa yao ya ujasiri, ushujaa, ukakamavu na werevu.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi.

Sura hii imejishughulisha na muhtasari wa ripoti yangu kwa kumlika malengo na makisio ya uchuguzi huu, Nimejadili jinsi nilivyotimiza madhumuni ya utafiti huu na pia kudhibitisha makisio yaliyoongoza kazi hii. Tamatini nimeonyesha vikwazo vilivyonikumba na kutoa mapendekezo anuwai kwa mujibu wa mambo yaliyoibuka kutokana na uchunguzi wangu.

5.2 Muhtasari

Ripoti hii ya mtafiti imegawanywa katika sura tano. Katika sura ya kwanza, mambo mbalimbali yanayopambanua mada ya utafiti yamefafanuliwa. Yaliyojumuishwa hapa ni pamoja na usuli wa mada, mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, maswali ya utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti. Isitoshe, upeo na mipaka ya utafiti huu pamoja na maelezo ya istilahi zimepambanuliwa katika sura hii. Sura ya pili imeshugulikia mapitio ya maandishi yaliyohusiana na mada ya utafiti. Mtafiti alishughulikia maandishi yaliyohusiana na chimbuko la tofauti ya nafasi ya mwanamume na mwanamke katika jamii, maandishi kuhusu utambulisho katika jamii,maandishi kuhusu utambulisho wa mwanamume na maandishi kuhusu methali. Mwisho, sura hii pia ilitoa msingi wa nadharia iliyotumika kuuongoza utafiti huu.

Sura ya tatu ilishughulikia kwa undani mbinu zilizotumiwa kukusanya data, data iliyopatikana na jinsi data hiyo ilivyochanganuliwa. Sura ya nne ndiyo kitovu cha utafiti huu. Sura hii iliangalia uchanganuzi wa data iliyokusanywa. Uchambuzi wa kina ulifanywa kuhusu utambulisho wa mwanamume katika methali za jamii ya Agikuyu zilizoteuliwa. Mtafiti alibainisha jinsi mikakati ya usemi ilivyodhihirika katika methali zilizoteuliwa. Majukumu na nafasi ya mwanamume katika jamii pia ilifafanuliwa kutoka kwa methali. Sura ya tano ilitamatisha utafiti huu. Kauli za mwisho za ripoti hii zimeelezwa hapa. Muhtasari wa kila sura umetolewa. Pia kuna matokeo, hitimisho, matatizo yaliyomkumba mtafiti na mapendekezo.

5.2.1 Malengo na Makisio ya Utafiti.

Katika utafiti huu**,** nilichunguza utambulisho wa mwanamume katika jamii ya Agikuyu nikitumia methali arubaini na tano za jamii hiyo kama matini. Uchunguzi wangu uliongozwa na nadharia ya Uchanganuzi Hakiki Usemi mkabala wa Kihistoria. Malengo ya utafiti huu yalikuwa:

Kwanza, kutadhmini na kubainisha mahusiano kwa mujibu wa jinsia katika jamii ya Agikuyu. Kwa kutumia mikakati ya usemi ya Wodak (2004), methali zilichanganuliwa na kudhibitisha madai haya.

Aidha nililenga kudhibitisha jinsi jamii ya A gikuyu inavyomtambulisha mwanamume kwa kutumia methali. Kwa kutumia methali arubaini na tano (45) zilizoteuliwa na kuchanganuliwa, ilidhibitika wazi jinzi mwanamume katika jamii ya Agikuyu anavyotambuliwa.

Isitoshe, uchunguzi huu ulidhamiria kubainisha majukumu na nafasi ya mwanamume kama inavyodhihirika kupitia kwa methali teule.

Matokeo yote ya utafiti huu yamedhibitishwa. Ilibainika wazi kuwa mahusiano kwa mujibu wa jinsia si mazuri kwani ni yale ya "Bwana na Mtumwa". Mwanamume ndiye bwana naye mwanamke ni mtumwa. Utafiti huu uligundua kuwa mwanamke alitarajiwa kumtumikia mwanamume wakati wote, jambo amalo liliwadhalilisha wanawake. Mwanamume alichukua nafasi ya kwanza katika shughuli zote za jamii ya Agikuyu. Mwanamke akawa yeye ni wa kuongozwa tu. Hii ndiyo sababu ya mahusino yale kuonekana kama yale ya mtumwa na bwana yake.

Baada ya kuchanganua zile methali zlilzoteuliwa, ilidhibitika wazi jinsi jamii ya Agikuyu ilvyomtambulisha mwanamume. Jamii husika ilimtambua mwanamume kama jasiri na asiye na woga. Mwanamume akarejelewa katika methali kama " *Mundurume*", ikiwa na maana ya mtu asiyekuwa na woga na mwenye ujasiri. Pia mwanamume alirejelewa kama "*Muthuri*", ikiwa na maana ya mtu mwenye busara na hekima. Mwanamume ni mtu aliyeheshimika katika jamii ya Agikuyu. Methali " *Hari athuri hatitangagwo mai"* yaani palipo na wazee hapana mzaha.

Utafiti huu uliweza kubainisha majukumu na nafasi ya mwanamume katika jamii ya Agikuyu. Utamanduni wa jamii ya Agikuyu ulimpa mwanamume nafasi ya mbele kuliko mwanamke. Pia majukumu aliyotunukiwa mwanamume ni yale ya hadhi na ya kumtukuza mwanamume. Majukumu aliyotwikwa mwanamume ni pamoja na kuchunga, kuchonga, kufua vyuma, kuongoza jamii, kutoa mashauri, kuilinda jamii pamoja na kuongoza sherehe muhimu katika jamii hasa zinazohusu kumwabudu Mungu. Mwanamke naye alitwikwa majukumu ambayo hayakumpa hadhi ya juu. Majukumu ya mwanamke yakawa ni kupika, usafi wa nyumbani, kutafuta kuni na maji, kufua nguo, kuwalea watoto na kuwatunza watoto na kumtumikia bwana yake.

5.2.2 Vikwazo

Kikwazo kikubwa kilichoukumba utafiti huu ni tafsiri ya matini kutoka lugha asili hadi lugha ya Kiswahili. Matini yote ilipatikana katika lugha ya Kikikuyu. Ilibidi mtafiti aitafsiri matini hiyo kwa lugha ya Kiswahili kwa kutumia tafsiri huru. Katika kutafsiri kuna baadhi ya istilahi za Kikikuyu ambazo ilikuwa muhali kupata kisawe chake katika Kiswahili. Hapa mtafiti alijikakamua kutafuta neno mwafaka la kusimamia istilahi hiyo. Huennda maana kamili iliyokusudiwa kupotoka kiasi.

Mtafiti alinyimwa kibali cha kutumia maktaba ya chuo kikuu cha Kenyatta, ambayo alitumaini ingekuwa dafina kuu kwa utafiti wake. Kunyimwa kibali cha kutumia maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta ulikuwa ni udhaifu wa mtafiti kutofanya maandalizi mema mapema. Ilimbidi mtafiti kupata baadhi tu ya makala aliyohitaji kupitia kwa mwanafunzi mmoja sahibuye na pia kutoka kwa mtandao. Kupata methali za Agikuyu zilizochapishwa kwa Kikikuyu na kutafsiriwa kwa Kiswahili ilikuwa tukizi.

Mtafiti pia alikumbana na changamoto ya kijamii, pale alipowapoteza wapendwa wake wawili kwa wakati mmoja. Wapendwa hawa wawili ndio waliomsaidia mtafiti kuiagua ndoto yake ya kazi hii.. Ilichukua kipindi kirefu kwa mtafiti kuliwaza na kuendelea na kazi.

Mwisho, mtafiti alikumbana na shida kubwa ya wasawiriwa na fedha. Baadhi ya wasailiwa wangu niliozungumza nao walikataa kunipa yale niliyoyahitaji kimaksudi na ilibidi nitumie fedha nyingi kupata yale niliyohitaji. Hata hivyo, kutofanya hivi kungesababisha mtafiti kukosa alichohitajiili kuikamilisha kazi yake. Baadhi ya

istilahi za lugha ya kikikuyu zilikuwa muhali kuzitafsiri au kupata visawe vyake. Hata hivyo. Mtafiti alijaribu kuleta uwiano kati ya lugha chanzi na lugha pokezi.

5.3 Mapendekezo

Mtafiti alibainisha kuwa mahusiano baina ya wanaume na wanawake yalikuwa ni yale ya “bwana na mtumwa”. Mwanamume alijihisi kuwa yeye ni bora kuliko mwanamke na alikuwa na uwezo mkubwa kuliko mwanamke. Mtafiti anapendekeza utafiti ufanywe kuhusu jinsi ya kuboresha na kuimarisha uhusiano huu wa kijinsia katika jamii ya Agikuyu.

Imebainika kutokana na utafiti huu kwamba mwanamume katika jamii ya Agikuyu anatambuliwa kwa njia ya kumuenzi na kumpa nafasi ya juu sana akilinganishwa na mwanamke. Mwanamume anatambuliwa kama shujaa, jasiri, mwenye busara na hekima na kiongozi. Kwa njia zote mwanamume anatazamwa kwa jicho la kumpendelea na kumtukuza kama kiumbe maasumu. Chomba (2005) alifanya utafiti kuhusu usawiri wa mwanamke katika methali za jamii ya Agikuyu. Ninapendekeza utafiti ufanywe kuhusu utambulisho wa mwanamume katika hadithi na nyimbo katika jamii ya Agikuyu. Pia jamii nzima ya Agikuyu kupitia kwa utamaduni wake wajaribu kurekebisha hali ilivyo katika kumtambua mwanamume.

Mwishowe mtafiti aligundua kuwa mwanamume alichukua majukumu na nafasi zilizo za umuhimu mkubwa katika jamii na kumwachia mwanamke majukumu na nafasi duni. Jambo hili ni wazi hasa pale mwanamume anapotambuliwa kama kiongozi wa jamii, mlinzi na anayetegemewa katika ushauri wa jamii. Mtafiti anapendekeza utafiti ufanywe kuhusu jinsi ya kuboresha ugawanaji wa sawa wa nafasi na majukumu ya kijamii katika jamii ya Agikuyu.

MAREJELEO

Abdalla, A. (1973). Sauti ya Dhiki. Nairobi: Oxford University Press.

Achebe, C. (1960). *Things Fall Apart.* Heinman, 1960.

Amuka, P. S. O. in Bukenya A. Kabira, M. Okambo, O. (1994). U*nderstanding OralLiterature.*Nairobi: NairobiUniversity Press.

Barra, G. (2010). *1000 Kikuyu Proverbs.* Nairobi: Kenya Literature Bureau,.

Bascom, W.R (1955). Verbal Art. *Journal of American Folklore 68: 245-52.*

Blum, K. (1991). Sociology in Changing World (2nd Edition). New York. Holt, Rinehart & Winston.

Chacha, N. C. (1997). *Mke Mwenza.* Nairobi *:*East Africa Educational Publishers.

Chomba, E. N. (2005). *Usawiri wa Mwanamke Katika Methali za Kikuyu. T*asnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Egerton.

Fairclough, N. & Wodak, R. (1997). *Critical Discourse Analysis.*London:In Van Dijk Teun A. (ed), *Discourse as Social interaction*, London, Thousand Oaks and New Delhi, pp.258-284.

Finnegan, R. (1970). Or*al Literature in Africa.* Nairobi *:* Oxford University Press.

Finnegn, R. (1992). *Oral Traditions & Verbal Arts*. London: Routledge press, New fetter lane.

Frosh, S. Phoenix , A and Pathman, R. (2002). *Young masculinities*. New York: Palgrave

Halliday, M.(1978). *Language as Social Semiotic*. New York. Edward Arnold.

www.efeas.uni-mainz..de

Isaac, A. O. (2011). *Faculty of Science Proposal Writing Format*, EgertonUniversity.

Jahadhmy A. A. (1997). *Kusanyiko la Mashairi. (Anthology of Swahili Poetry*). Nairobi: East African Educational Publisher Ltd.

King'ei, G. K. (1982). *Uhakiki wa Methali za Kikamba kwa kufuata Misingi ya Methali za Kiswahili*. Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kenyatta, J. (1938). Facing Mount Kenya. Nairobi. Kenway Publication, an Imprint of East African Educational Publishers Ltd.

Kipury, N. (2002). *Oral Literature of the Maasai. Nairobi:* East African Education Publishers Ltd.

Kithaka wa Mberia, (2004). *Natala.* Nairobi*:* Marimba Publications Ltd.

Kress, G. (1990) . *Critical Discourse Analysis.* Annual Review of Applied Lingustics, 11:84-97.

Lo Liyong, T. (1986). *Popular Culture of East Africa* . Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Madumulla, J.S (2005). *Proverbs and Sayings. Theory & practice*. Dar-es-salaam: Institute of Kiswahili Research, University of Dar-es-salaam.

Martin, Dennis-constant, (1995) The Choices of Identity, *social identity* 1:1, pp. 5-20

Massamba, D. P. B (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha. Dar es salaam:* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Tanzania.

Massamba, D. P. B. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha.* Dar es salaam*:* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es salaam, Tanzania.

Mathooko, J. M , Mathooko. F. M, Mathooko, P. M, (2007). *Academic Proposal Writing , A Guide to Preparing Proposals for Academic Research.* Nakuru*:* First Edition, Amu press.

Mdee, J. S., Njogu, K., Shafi, A. (2011). *Kamusi ya Karne ya 21. Kamusi ya Kiswahili Yenye Uketo Zaidi Katika Karne Hii.* Nairobi. Toleo la Pili. Longhorn Publishers (K) Ltd.

Mello, R.A. (1999). *Narrating Gender. Children's Response to Gender Roles Depicted in Orally told Forktales and Other Traditional Stories*. P.hd Dissertation. Lesley College.

Milroy, J (1987). *Observing and Analysing Natural Language*. London: Basil Blackwell..

Mugenda, O.M na Mugenda, A.G (1999). *Research Methods. Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi. Acts Press.

Mugo, E. N. (1982). K*ikuyu People. Brief outline of Their Customs & Traditions.*Nairobi*:* Kenya Literature Bureau.

Mtesigwa, P.C.K (1989). Methali ni nini? Makala Katika Kiswahili: *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Juzuu 56*. Dar es salaam. Chuo Kikuu Cha Dar es salaam.

Ndalu, A. (1997). *Mwangaza wa Kiswahili.*Nairobi: East African Educational Publishers Ltd.

Ndalu, A. na Kingei, K. G. (1999). *Kamusi ya Methali za Kiswahili.*. Nairobi*:* East African Educational Publishers Ltd.

Ndulute, C. (1987). *Notes on African Proverbs. Diffusion Morphology & Transmutation* (unpublished article).

Ndung'o, C.M. (1985). *Wanawake na Mabadiliko ya Kihistoria* . Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Ngugi, F. (1975). *The Changing Image of Women over Three Crucial Historical Phases*. Nairobi. Kenya Literature Bureau.

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari.* Nairobi*:* Phoenix Publishers Ltd.

Njogu, K. ,Momanyi, C. , Mathooko, M. (2006), *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi:

Nkwera, F.V.M (1978). *Sarufi na Fasihi. Sekondari na Vyuo*. Dar es salaam; Tanzania Publishing house.

Ogot, B.A. (1983). *Kenya Before 1900. Eight Regional Studies*. Nairobi: East African Publishing House Ltd.

Okindo , A. O. (1995). S*ura ya Mwanamke Katika Methali za Ekegusii*. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Egerton.

Okpewho, I. (1992). *Africa oral Literature* U.S.A Indiana Unniversity Press.

Onyango, J.O (2007). *Masculinities in Kiswahili Children's literature in Kenya.* Swahili Forum 14(245-254).

Parker, C. A. (1970). *Iwapo Nia kuna Njia. A study of the Content & Context of Proverbs in Swahili.* M.A Thesis, University of Washington, Dept' of Anthropology.

Ricoeur, P. (1992), *Oneself as Another.* Chicago&London.

Schipper, M. (1991). *Sources of All Evils: African Proverbs & Sayings on women*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Sietel, P. I. (1972). *Proverbs and the Structure of Metaphor*. P.H.D. Thesis, University of Pennyslvania, Ann Arbo Michigan.

Taylor, A. (1962). *The proverbs of index to* "the proverbs". Copenhargen: Rosen Kilde and Bagger.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Nairobi:* OxfordUniversity Press.
Twaweza Communications.

Uchendu, E.. *Forthcoming Masculinities and Nigeria Youths*. Nordic Journal of African Studies.

Utendi wa Mwanakupona (Unpublished)

Walibora, K. (2001). *Ndoto ya Amerika* Nairobi: Sasa Sema Publication.

Walibora, K. (2004a). *Mtu wa Mvua*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Walibora, K. (2004b). *Mgomba Chagarweni*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. W. (2001). *Kamusi ya Methali. Nairobi:* Longhorn Publishers, (Kenya) Ltd.

Wamitila, K.W. (2007). *Kamusi ya Methali. Nairobi:* Longhorn Publishers (Kenya) ltd, ,.

Wandera, S.P . (1996). U*sawiri wa Mwanamke Katika Ushairi wa Kiswahili* 1800-1900: *Uhalisia au Ugandamizwaji*? Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Egerton.

Wescott, R.W (1981). *From proverbs to Aphorism in Forum Lingusticum*, V.3

Wodak, R. , Meyer, M. (2004). *Methods of Critical Discourse Analysis* .New Delhi: SAGE publications India Prt Ltd.

Wodak, R., De cilia, R., Reisigl, M., and Liebhart, K. (1999). *The Discursive Construction of National Identity*. Edinburg*:* Edinburg University Press Ltd, 22 George Square.

VIAMBATISHO

Kiambatisho I

Maswali ya Mahojiano Kwa Wasailiwa Kumi na Wawili (12)

Sehemu A

1. *Awa/Maitu, njira kihumo kia ruriri rwa gikuyu na aciari ao a mbere mari ni a* ?.
   Baba/mama, nielezee asili ya jamii ya Agikuyu, na wazazi wao.
2. *Awa/Maitu, ndariria mitugo na miikarire ya agikuyu*.
   Baba/mama nielezee kwa undani mila na desturi za wakikuyu.
3. *Awa/.maitu,mundu ageragira itina iriku kuuma guciarwo nginya gukua?.*
   Baba/mama mtu alipitia hatua zipi za maisha tangu kuzaliwa hadi kufa?
4. *Awa/Maitu, kwari na utiganu uriku hari mambura ma guciarwo gwa kaana ga kahii na ma kaana ga kairitu?*
   Baba/Mama, eleza tofauti kati ya sherehe za kuzaliwa kwa mtoto wa kiume na wa kike?
5. *Awa/maitu, murerere wa kahii na kairitu wina utiganu uriku*? Baba/mama, kulikuwa na tofauti gani kati ya ulezi wa mtoto wa kiume na Yule wa Kike?
6. *Awa/Maitu, unduire wa mugikuyu woigaga atia hari uhoro wa mundurume na Mutumia?* Baba/Mama, utamaduni wa Agikuyu ulichukulia aje hali ya jinsia ?

Sehemu B

1. *Awa/Maitu, thimo ni kii?*
   Baba/mama, methali ni nini?
2. *Awa/maitu, Thimo ciari na bata uriku hali muturire wa mugikuyu*?
   Baba/mama methali zilikuwa na umuhimu gani katika maisha ya jamii ya kikuyu?
3. *Awa/maitu, njira thimo iria ciarongoreirie mundurume. na niki?*
   Baba/mama, taja baadhi ya methali zinazomrejelea mwanamume. na maana yake?
4. *Awa/maitu, thimo yatumagirwo gutugiria kana kunyarara mundurume?. Na niki?*
   Baba/mama, methali ilitumika kumtwaza au kutweza mwanamume, na kwa nini?.
5. *Awa/maitu,gweta thimo iria ciatugagiria mundurume.*
   Baba/mama, taja methali ambazo zinamtwaza mwanamume.
6. *Awa/maitu, mundurume anyararagwo niki, na akumagio niki?*
   Baba/mama kwa nini mwanamume adunishwe na kwa nini atwazwe?

Kiambatisho 2

Methali Zinazomtambulisha Mwanamume

Methali za mkabala wa kisiasa.

1.Mari guoya mainukagira nyina, nao mari urume mainukagira ithe.

2.Hari athuri hatitangagwo mai

3.Kahii kogi ta ithe kabaritaga ta migwi.

4Kahii ni ithigi ria mucii.

5Kahii ka mwathi kamenyaga kugereka.

6.Mbu ya arume itikagwo ni muthamaki

7.Maitho ma arume ti ma iranga

8.Mwana mukuru na ithe ni hamwe.

9.Mwana ndahuragwo ithe ari ho.

10.Njamba ni ithaga ria rika.

11.Ugi wa arume utemaga ta kahiu.

12.Wa kahii ti wa kairitu

13.Mundu wa muka umwe ni tuhu wa kanyene.

Methali za mkabala wa kiuchumi

1.Gutiri munini mukia

2.*Njamba nyinyi ndinyakagwo*

3.*Mwanamke wina indo ndoihanaga*

4.*Uthaka wa mundurume ti magego*

5. *Uhii niumagwo no utumia ndumagwo*

6. *Njamba ikuaga na matanya*

Methali za mkabala wa kijamii

1.Gutiti njamba ya mwera umwe.

2.Gutiri mucii wa kahii utakarugwo mutwe

3.Mwana mugi akenagia ithe, nake mukigu aturagia nyina na maithori.

4.Mucii uraga ngo ciagirirwo makumbiini.

5.Cia athuri nithure.

6.Cia mucii iri gacuguma gacio,gatathukagio ni mundurume ungi tiga mwene guo.

7.Gitiro kia muka wene gitinagio athii.

8.Marakara ma arume matituraga ta ma aka.

Muici na mundu muka atigaga kieha akua.

9.Muka wa mwathi ahingaga na kuguru etereire kigurumuki oke.

10.Nyoni ya njamba ndiri gitara.

11.Muthuri utari kahii niwe wiriragira ngururu.

Methali za mkabala wa kimaubile

1.Kirema arume nikigariure.

2.Nyama (Ngari) (Njamba) ndiriagwo ni wira.

3.Njamba ti ikeere

4.Hunyu ni umwe na arume.

5.*Arume mari rwamba*

6.Gutiri mundurume muka wa uria ungi.

7.Wiyumiririe wa kahii ti wa kairu.

Methali mkabala wa kisaikolojia

1.Anake ni cienyu cia Ngai

2.Mundurume ni Ngai ya keri

3.Mwana ndetagia ithe nyama

4.Thutha wa arume nduoyagwo ruoya

5.Nyau nguru inyuaga iria.

6.Arume hau niho turi

7.Kuhoya kwa arume ni maitho

Kiambatisho 3

Waliohojiwa

Tarehe 2/9/2013 siku ya Jumatatu saa nne asubuhi hadi saa tisa alasiri, katika kijiji cha subuku Gatuzi ndogo la Ndaragwa, kaunti ya Nyandarua, niliwahoji wawili wafuatao ambao ni bibi na bwana;

1.*Mbuguah wa Wanjau*

2.Wairimu wa Mbuguah

Asubuhi saa tano na nusu tarehe 4/9/2013, katika kijiji cha Ngufa, kaunti ya Nyandarua, niliwahoji wasawiriwa watatu mtawaliwa;

3. *Samwel Njenga Kinyanjui*

4. Martha Njoki Mwangi

Ijumaa tarehe 6/9/2013 saa nane alasiri, katika kijiji cha Lock Four, katika kaunti ya Nyandarua niliwahoji;

5. *Joyce Wangui Maina*

6. Waithira wa Gathecha

Tarehe 7/9/2013, Jumamosi saa mbli na nusu hadi saa kumi na moja, katika kijijim cha Gwa Kihara, niliwahoji wafuatao;

7. *Eliud Waruingi*

8. Mechack Muya Thuby

Jumatatu tarehe 9/9/2013, saa nne na robo, katika kijiji cha Gatahuwaga, niliwahoji wafutao;

9. *Ajericah Wanjeri*

10. Philip Githaiga Mwangi

Saa nane na nusu, Jumatano tarehe 11/9/2013, katika kijiji cha Mwiruti, nilimhoji;

11. *Maina wa Arthur*

Tarehe 13/9/2013, siku ya Ijumaa, saa tatu asubuhi, katika kijiji cha Mwaragania, nilimhoji;

12. *Ayub Kariuki wa Njai*